

**KUCHUNGUZA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA RIWAYA YA
KICHWAMAJI NA VUTA N’KUVUTE – UTAFITI LINGANISHI**

MOHAMMED SOUD JUMA

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA SEHEMU YA
MASHARTI YA SHAHADA YA UZAMILI YA (M.A KISWAHILI - FASIHI)**

YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA

2017

UTHIBITISHO

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa ameisoma kazi hii na anapendekeza kuwa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kukubali kupokea tasnifu hii ya **Kuchunguza Matumizi ya Lugha Katika Riwaya ya *Kichwamaji na Vuta n’kuvute* – Utafiti Linganishi**, na kwamba nimeridhika kuwa tasnifu hii imefikia kiwango kinachotakiwa na inafaa kuhudhurishwa kwa utahini wa shahada ya uzamili [M. A Kiswahili - Fasihi] ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.....
Prof. Emmanuel Mbogo

(Msimamizi)

.....
Tarehe

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga, kutafsiri, kupiga chapa au kunakili kwa namna yoyote ile ya tasnifu hii kwa njia yoyote kama vile kielektroniki, kurudufu nakala, kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

TAMKO

Mimi, **Juma, Mohammed Soud** nathibitisha kuwa tasnifu hii ni yangu mwenyewe haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya kutunukiwa shahada ya uzamili au shahada nyingine katika chuo kikuu chengine chochote ndani ya nchi wala nje ya nchi.

.....

Sahihi

.....

Tarehe

TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa wanafunzi wangu wa skuli ya Langoni Sekondari wa kidato cha nne 2016 pamoja na wanangu, ili iwe kwao ni chachu ya kujifunza zaidi na kuweza kufikia kiwango hiki na zaidi ya hiki.

SHUKRANI

Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu (SW) Muumba wa mbingu na ardhi kwa kunijaalia afya njema na uzima wa kimwili na kiakili na pia kubahatika kupata nafasi ya kusoma ya uzamili (M.A Kiswahili) kwa mwaka 2016 kwani fursa hii watu wengi hawajaipata.

Shukurani zangu za pekee zimwendee msimamizi wa utafiti huu Profesa Emmanuel Mbogo kwa kuniongoza, kunishauri, kunisimamia na kunipa changamoto mbalimbali hadi utafiti huu ukakamilika. Mwenyezi Mungu amlipe kila la kheri na amkinge na kila mabalaa ya dunia.

Pia napenda kuwashukuru wanafunzi wenzangu akina mwalim Othmani Suleiman Hamad, Bi Mwan-jabu Makame Ali, mwalim Ali Hassan na wale wote tuliokuwa tukikutana katika kituo chetu cha Skuli ya Mtopepo na wengine wote tulioshirikiana katika kuelekezana na kufahamishana na kupeana muongozo na moyo ili tusirudi nyuma na kuacha kusoma kwani kazi ilikuwa ngumu na nzito.

Vile vile ninawashukuru wana familia yangu wote kuanzia Baba yangu bwana Soud Juma na mama yangu Kazija Abdalla pamoja na ndugu zangu kwa mchango wao mkubwa walionipa wa kimawazo na hata fedha. Pia shukurani zangu za dhati ziwaendee wake zangu Bi Mwanajuma Mwinyijuma na Bi Asya Matao kwa uvumilivu wao katika kipindi chote hiki cha masomo kwa kuwaachia jukumu la malezi ya watoto peke yao.

Mwisho nitakuwa mpungufu wa shukurani kama sitowashukuru wale wote walionifadhili kwa namna moja au nyingine hadi nikaweza kukamilisha utafiti huu, kwa kile walichonisaidia wajuwe hawajatupa bali Mwenyezi Mungu atawaengezea zaidi duniani na akhera katika siku ya malipo. Amin.

IKISIRI

Utafiti huu unahusu Kuchunguza Matumizi ya Lugha Katika Riwaya ya *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute* – Utafiti linganishi. Tasinifu hii imekusudia katika kuonesha matumizi ya lugha kwenye kipengele cha tamathali za semi zilizotumika katika riwaya teule. Pia kuonesha namna waandishi hawa walivyofana na kutofautiana katika matumizi ya tamathali ya semi na namna zilivyoibua dhamira mbalimbali. Utafiti huu umeongozwa na nadharia kuu mbili. Nazo ni nadharia ya simiotiki ambapo imemwezesha mtafiti kubaini tamathali za semi mbalimbali. Na nadharia ya udhanaishi iliyoweza kuibua dhamira mbalimbali kutoka katika riwaya hizo teule. Kwa upande wa mbinu za kukusanyia data, mtafiti alitumia mbinu ya kimaktaba kwa kuanza kuvidurusu vitabu teule na kuyaelewa kwa undani maudhui yaliyokusudiwa na waandishi wa vitabu hivyo. Kisha mtafiti akarudia kuvisoma kwa umakini zaidi kwa kudondoa kila tamathali ya semi aliyoikuta na kuitayarishia jedwali lake maalumu. Baadae mtafiti akutoa dhamira zilizojitokeza kutoka katika tamathali za semi. Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa waandishi wote wawili wamefanana kwa kutumia tamathali za semi kumi na moja (11). Na mwishowe tamathali za semi hizo zimeweza kutoa dhamira ishirini na mbili (22). Na kubainika kuwa wamefanana katika tamathali za semi na wametofautiana kwa upande wa dhamira na hili limetokana na kuwa riwaya ya *Kichwamaji* ni fupi kidogo kulinganisha na riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

YALIYOMO

UTHIBITISHO	ii
HAKIMILIKI	iii
TAMKO	iv
TABARUKU	v
SHUKRANI.....	vi
IKISIRI	viii
ORODHA YA MAJEDWALI.....	xiv
ORODHA YA VIAMBATANISHI	xvii
SURA YA KWANZA.....	1
UTANGULIZI	1
1.1 Usuli wa Tatizo	1
1.2 Usuli wa Mada	8
1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti	8
1.4 Malengo ya Utafiti	9
1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti	9
1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti	9
1.5 Maswali ya Utafiti.....	10
1.6 Umuhimu wa Utafiti.....	10
1.7 Mipaka ya Utafiti	11
1.8 Mpangilio wa Kazi ya Utafiti	11
1.9 Hitimisho	12

SURA YA PILI	13
MAPITO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA NADHARIA.....	13
2.1 Utangulizi	13
2.2 Kazi Tangulizi Zinazohusu Ufanyaji wa Utafiti.....	13
2.3 Kazi Tangulizi Zinazohusu Fasihi Linganishi.....	14
2.4 Kazi Tangulizi Zinazohusu Riwaya kwa Ujumla	16
2.5 Kazi Tangulizi Zinazohusu Vitabu Teule.....	20
2.6 Mkabala wa Nadharia.....	26
2.6.1 Nadharia ya Simiotiki / Umatini	26
2.6.2 Nadharia ya Udhanaishi	29
2.7 Umuhimu wa Nadharia Hizi katika Utafiti.....	31
2.8 Ombo la Kitaaluma	31
2.8.1 Mapungufu.....	31
2.8.2 Makusudio	32
2.9 Hitimisho	32
SURA YA TATU.....	33
MBINU ZA UTAFITI.....	33
3.1 Utangulizi	33
3.2 Mbinu za Utafiti	33
3.3 Mpango wa Utafiti	33
3.4 Walengwa wa Utafiti.....	34
3.5 Uteuzi wa Sampuli	34
3.5.1 Mbinu za Uteuzi wa Sampuli.....	35
3.6 Mawanda ya Utafiti.....	35

3.7	Zana / Vifaa vya Utafiti	36
3.7.1	Ngamizi / Kompyuta	36
3.7.2	Kalamu na Karatasi	36
3.8	Ukusanyaji wa Data	37
3.8.1	Data za Msingi	37
3.8.2	Data za Upili	37
3.8.3	Mbinu ya Kimaktaba	38
3.9	Uchambuzi wa Data	39
3.10	Udhibiti wa Data	39
3.11	Hitimisho	40
	SURA YA NNE	41
	UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA.....	41
4.1	Utangulizi	41
4.2	Usuli wa Watunzi	41
4.2.1	Kezilahabi ni Nani?	41
4.2.2	Shafi A. Shafi ni Nani?.....	42
4.3	Tamathali ya Semi.....	42
4.3.1	Tamathali ya Semi ya Tashibiha.....	44
4.3.2	Tamathali ya Semi ya Tashihisi	46
4.3.3	Tamathali ya Semi ya Sitiari.....	48
4.3.4	Tamathali ya Semi ya Mubalagha.....	50
4.3.5	Tamathali ya Semi ya Tafsida	52
4.3.6	Tamathali ya Semi ya Tauria	53
4.3.7	Tamathali ya Semi ya Shitizai / kejeli.....	55

4.3.8	Tamathali ya Semi ya Dhihaka	57
4.3.9	Tamathali ya Semi ya Takriri	58
4.3.10	Tamathali ya Semi ya Tabaini	60
4.3.11	Tamathali ya Semi ya Msisitizo Bayani.....	62
4.4	Hitimisho	63
4.5	Dhamira Zilizojitokeza Kutoka katika Tamathali za Semi	63
4.5.1.1	Dhamira ya Uongozi Mbaya.....	65
4.5.1.2	Dhamira ya Mapenzi Nje ya Ndoa.....	68
4.5.1.3	Dhamira ya Umasikini.....	72
4.5.1.4	Dhamira ya Mapenzi kwa Wanafamilia	75
4.5.1.5	Dhamira ya Uchawi na Ushirikina.....	78
4.5.1.6	Dhamira ya Umoja na Mshikamano.....	80
4.5.1.7	Dhamira ya Ulevi wa Kupindukia.....	82
4.5.1.8	Dhamira ya Mapenzi ya Kweli	85
4.5.1.9	Dhamira ya Chuki na Uhasama	89
4.5.1.10	Dhamira ya Unyanyasaji wa Wanawake	93
4.5.1.11	Dhamira ya Kufanya Kazi Kwa Bidii	97
4.5.1.12	Dhamira ya Usaliti	99
4.5.1.13	Dhamira ya Malezi Mabaya kwa Watoto	102
4.5.1.15	Dhamira ya Wivu wa Kupindukia.....	109
4.5.1.16	Dhamira ya Upendo.....	111
4.5.1.17	Dhamira ya Imani za Kidini	115
4.5.1.18	Dhamira ya Upendo kwa Viumbe Hai	116
4.5.1.19	Dhamira ya Umuhimu wa Ndoa	118

4.5.1.20 Dhamira ya Uasharati	119
4.5.1.21 Dhamira ya Umuhimu wa Elimu	123
4.5.1.22 Dhamira ya Ukombozi.....	126
4.6 Hitimisho	131
SURA YA TANO	133
MUHTASARI NA MAPENDEKEZO	133
5.1 Utangulizi	133
5.2 Muhtasari.....	133
5.3 Mapendekezo	136
5.4 Hitimisho	137
MAREJELEO.....	138
VIAMBATANISHO	144

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 4.3: Tamathali za semi zilizotumika katika riwaya za <i>Kichwamaji na Vuta n'kuvute</i>	43
Jedwali Na. 4.3.1.1 linaonesha tamathali ya semi ya tashibiha zilizotumika katika riwaya ya <i>Kichwamaji</i>	44
Jedwali Na. 4.3.2.2 linaonesha tamathali ya semi ya tashibiha zilizotumika katika riwaya ya <i>Vuta n'kuvute</i>	45
Jedwali Na. 4.3.2.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Tashihisi Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Kichwamaji</i>	46
Jedwali Na. 4.3.2.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Tashihisi Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Vuta n'kuvute</i>	47
Jedwali Na. 4.3.3.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Sitiari Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Kichwamaji</i>	49
Jedwali Na. 4.3.3.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Sitiari Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Vuta n'kuvute</i>	49
Jedwali Na. 4.3.4.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Mubalagha Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Kichwamaji</i>	50
Jedwali Na. 4.3.4.2 Linaonesha Mubalagha Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Vuta n'kuvute</i>	51
Jedwali Na. 4.3.5.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Tafsida Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Kichwamaji</i>	52
Jedwali Na. 4.3.5.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Tafsida Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Vuta n'kuvute</i>	53

Jedwali Na. 4.3.6.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Tauria Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Kichwamaji</i>	54
Jedwali Na. 4.3.6.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Tauria Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Vuta n'kuvute</i>	54
Jedwali Na. 4.3.7.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Shitizai Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Kichwamaji</i>	55
Jedwali Na. 4.3.7.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Shitizai Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Vuta n'kuvute</i>	56
Jedwali Na. 4.3.8.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Dhihaka Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Kichwamaji</i>	57
Jedwali Na. 4.3.8.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Dhihaka Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Vuta n'kuvute</i>	57
Jedwali Na. 4.3.9.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Takriri Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Kichwamaji</i>	58
Jedwali Na. 4.3.9.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Takriri Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Vuta n'kuvute</i>	59
Jedwali Na. 4.3.10.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Tabaini Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Kichwamaji</i>	60
Jedwali Na. 4.3.10.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Tabaini Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Vuta n'kuvute</i>	61
Jedwali Na. 4.3.11.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Msisitizo Bayani Uliotumika Katika Riwaya ya <i>Kichwamaji</i>	62
Jedwali Na. 4.3.11.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Msisitizo Bayani Zilizotumika Katika Riwaya ya <i>Vuta n'kuvute</i>	62

Jedwali Na. 4.5.2.1 Linaonesha Dhamira Zilizojitokeza Kwenye Tamathali za Semi	
Katika Riwaya za Kichwamaji na <i>Vuta n'kuvute</i>	131

ORODHA YA VIAMBATANISHI

Kiambatanishi 1: Tamathali za Semi Katika Riwaya ya *Kichwamaji*144
Kiambatanishi 2: Tamathali za Semi Katika Riwaya ya *Vuta n’kuvute*149

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Tatizo

Utafiti huu umehusika kuchunguza matumizi ya lugha kwa waandishi wawili, mmoja kutoka upande wa Tanzania bara na mwingine kutoka upande wa Zanzibar. Ni utafiti linganishi uliochunguza matumizi ya lugha katika kazi ya fasihi na jinsi yanavyofanana na kutofautiana kati ya mwandishi E. Kezilahabi mwenye asili ya Tanzania bara ambapo lugha ya Kiswahili kwake ni lugha ya pili na Shafi A. Shafi mwenye asili ya Zanzibar ambapo lugha ya Kiswahili ndio lugha yake ya kwanza.

Kwa mujibu wa wataalamu wa fasihi kama vile Mulokozi (1995), yeye ameona kwamba utanzu wa kwanza kuwepo duniani ni ushairi wa nyimbo. Lakini pia tunaweza kusema kwamba riwaya nayo pia ilikuwepo kutokana na sifa zinazoelezwa na wataalamu ambazo kwa sifa hizo utanzu uliodhihirishwa tunauita riwaya. Sifa hizo zilikuwa zikionekana kwenye hizo nyimbo / mashairi ya zamani, kama alivyosema Madumulla (2009a), utanzu wa riwaya ulikuwepo tangu hapo kale lakini ulifungamanishwa katika tungo za kishairi simulizi, hususani ndani ya tendi za kale kama vile utenzi wa *Fumolyongo*, Utenzi wa *Rasil-ghuli* na kadhalika.

Mbali na maelezo ya hapo juu, pia tunaweza kusema uandishi wa riwaya tulizonazo hivi leo unaowasilishwa kwa njia ya nathari, ni kama muendelezo tu wa yale yaliyokuwepo hapo kabla, yaani ni masimulizi kwa njia ya nathari badala ile ya nudhumu kama ilivyokwisha kuelezwa na Madumulla (ameshatajwa) ambapo visa na matukio yakiwasilishwa kwa kupitia nyimbo zilizokuwa katika muundo wa

mashairi ya kimapokeo. Na mtindo huu wa uandishi wa riwaya tulionao hivi sasa umeanza kutumika mwanzoni mwa karne ya 19 mara tu baada ya kugundulika maandishi ya Kirumi (Senkoro, 1977).

Mara baada ya ugunduzi huo wa uandishi ndipo waandishi wengi waliibuka na kuandika kazi mbalimbali. Miongoni mwao ni mwandishi mashuhuri katika fani ya fasihi andishi ya Kiswahili kwa upande wa riwaya ni huyu Shafi A. Shafi.

Wamitila (2002a), amemualezea mwandishi Shafi A. Shafi kuwa ni miongoni mwa watunzi bora wa kazi za fasihi andishi za Kiswahili, ambaye kutokana na umahiri wake kwenye kazi hii ya utunzi wa riwaya ameweza kushinda tunzo mbalimbali za uandishi bora wa riwaya ya Kiswahili na hili amelipata kutokana na matumizi yake mazuri ya lugha hasa katika kipengele cha tamathali za semi. Naye Mohamed na Senkoro (1987:55) wamemuelezea mwandishi Shafi A. namna alivyo mahiri katika matumizi ya lugha, mfano ni pale aliposema Mohamed wakati akimhakiki kupitia riwaya ya *Kuli*. “licha ya kuonesha ufundi wake wa kuwapa wahusika lugha tofauti, mwandishi ametuonesha vile vile ubingwa wake wa kutumia tamathali za semi. Methali kadhaa zimetumika ili kuongezea uzito katika maudhui”. Hapa Mohamed (ameshatajwa) anatuonesha jinsi ya uhodari wa mwandishi Shafi A, na namna anavyoweza kuitumia lugha hasa katika kipengele cha tamathali za semi.

Mulokozi (2010), katika kumueleza Kezilahabi juu ya umahiri wake katika kazi za uandishi wa fasihi na namna zilivyo na umuhimu mkubwa kwa jamii ya waswahili, amesema kwamba Kezilahabi ni mchambuzi wa kijamii ambaye anahoji kutoka katika jumuiya za jamii na imani juu ya ujamaa, ukristo, elimu ya magharibi, siasa ya

kifalsafa na kimatendo. Pia Kezilahabi ni mtaalamu aliyezitoa dhamira zake kwa mtazamo wa nadharia ya ubinafsi, udhanaishi, na kufanikiwa kufichua woga na mtanziko wa watanzania wenye kipato cha kati. Na Wamitila (1999:38-40) akaengezea katika kuonesha umahiri wa usanii wa Kezilahabi katika uandishi wa kazi za fasihi na namna anavyosarifu vipengele vya fani katika kazi zake.

Kwa mfano amesema majina yanayotumiwa na Kezilahabi huwa yanaleta maana na wakati mwengine hutumia kejeli katika baadhi ya majina, kwa mfano Deogratias wa *Rosa Mistika* ni jina ambalo liko kinyume na jina la Deusdedit Kazimoto katika *Kichwamaji*. Lile la *Rosa Mistika* lina maana asante Mungu lakini lile la *Kichwamaji* lina maana Mungu mwema mazoea.

Lugha na matumizi yake katika kazi ya fasihi ndio uti wa mgongo wa kazi yoyote ya fasihi, kazi ya fasihi bila ya lugha haitohisabiwa kuwa ni fasihi. Kwani fasihi ni sanaa inayotumia lugha katika kuwasilisha yale yaliyokusudiwa na msanii wa kazi ya fasihi. Ufundi wa msanii katika matumizi ya lugha kwenye kazi yake ya fasihi ndio unaodhihirisha ubora wa kazi hio. Lugha ya fasihi ni tofauti na lugha ya kawaida kwani lugha ya fasihi ni lugha teule yenye vionjo maalumu vinavyotofautisha kati ya lugha ya fasihi na lugha ya kawaida, vionjo hivyo kwa ujumla wake tunaviita matumizi ya lugha. Kama anavyoeleza Leech (1969), kwamba kazi yoyote ya fasihi haiwezi kufahamika vizuri pasina utumiaji mzuri wa lugha ambayo ndio nyenzo ya kujieleza kwa kazi ya fasihi. Hivyo hakuna fasihi bila ya kuwepo kwa lugha. Naye Fadhili (2013) amesisitiza umuhimu wa lugha katika kazi yoyote ya fasihi, na akaonesha namna vipengele vya mtindo vinavyoana na lugha

katika kukamilisha maudhui. Maudhui ya kazi yoyote ya fasihi hufahamika vyema kutokana na umahiri wa msanii katika kipengele hicho cha matumizi ya lugha.

Katika kuijenga vyema kazi ya fasihi ni utumiaji wa lugha ya kifasihi, Muhammed (1981:17) amesema kuhusu lugha kuwa ni kitu muhimu na cha lazima kwa kazi za fasihi; na akasisitiza kuwa lugha ni kiini au uti wa mgongo wa fasihi. Hivyo basi fasihi ni sanaa ya lugha, ila lugha ya fasihi ni teule iliyoteuliwa kwa madhumuni ya kuunda sanaa itakayomvuta msomaji au msikilizaji na kumfanya kazi anayoisoma au kuisikiliza kutamani isimalizike. Haya hupatikana kwa utumiaji mzuri wa matumizi ya lugha katika kazi ya fasihi na hasa katika kipengele cha tamathali za semi.

Na kwa upande wa umuhimu wa matumizi na uteuzi mzuri wa lugha katika kazi ya fasihi, Mbunda (1992:47), ameeleza “kazi za lugha katika fasihi hazihesabiki na wala hatuwezi kuzieleza zote”. Hii ina maana kuwa vipengele vya matumizi ya lugha katika kazi za fasihi ni vingi sana lakini hata hivyo amesisitiza Mbunda (ameshatajwa) uzuri wa lugha katika kazi za fasihi unazingatia ukamilifu wake katika sarufi, mofolojia (maumbo), fonolojia (umbo sauti) na umbo maana katika uchangamano wake. Hivyo msanii hana budi kuteuwa kipengele cha lugha kitakachoweza kukamilisha kazi yake kupitia sifa zilizokwishaatajwa hapo juu.

Naye Mulokozi (1996:15) ameifananisha lugha na mali ghafi katika kazi ya fasihi. na akasisitiza kuwa lugha hukuwa na kuongezeka msamiati wake kupitia kazi za fasihi. Pia akaonesha kwa kadiri lugha inavyotumika na kufinyangwa na watunzi ndivyo inavyokuwa na kupevuka. Kwa mtazamo huo unaonesha jinsi fasihi ilivyo na mchango mkubwa katika kukuza na kuendeleza na kueneza lugha kwa watumiaji.

Misamiati mingi ya Kiswahili inayotumika hivi leo, chanzo chake kimetokana na kazi za wasanii. Hivyo lugha ya Kiswahili imeweza kuongeza msamiati wake kupitia kazi za fasihi kupitia kipengele cha lugha.

Kwa mujibu wa Senkoro (2011), “kazi ya fasihi haiwezi kueleweka vizuri bila ya kuwa na maarifa ya lugha ambayo ndio njia ya kujieleza vizuri”. Kwa upande mwingine Senkoro (2011a:11) katika kufafanua zaidi juu ya lugha na kusema “lugha ndio mzizi wa kazi ya fasihi, na bila yenyewe kuwepo haiwezekani kuwepo na fasihi. Mwandishi ama mtunzi wa kazi ya fasihi hutumia lugha kuyaibusha mawazo yake katika kazi hiyo. Lugha ndio njia aitumiayo msanii wa fasihi kuyaeleza mambo mbalimbali ya jamii yake kwa njia ya ubunaji / ubunifu na kisanii. Na akataja kuwa matumizi ya lugha yako ya aina nyingi kama vile matumizi ya tamathali za usemi, misemo, nahau, methali, lugha za wahusika hasa lahaja zao, miundo ya sentensi na kadhalika. Senkoro (2011b:12) akafafanua maana ya vipengele vya matumizi ya lugha na kuonesha katika kipengele cha tamathali za semi na kusema ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii wa fasihi ili kutia nguvu katika maana, mtindo na hata sauti katika maandishi ama kusema. Vile vile akaongeza kwa kusema wakati mwingine hutumika kwa njia ya kuipamba kazi yake ya fasihi kwa kuongeza utamu wa lugha.

Naye Khatib (1986:1) alitoa ufafanuzi juu ya tamathali za semi kuwa kusema kuwa ni dafina kubwa isiyoweza kuchimbwa na kumalizika. Katika tanzu zote za fasihi simulizi na fasihi andishi zimejaa tamathali za semi. Akaendelea kusema tamathali zimeshehenezwa tumbwitumbwi ili ziweze kuteka masikizi na maoni ya wasikilizaji au watumiaji. Khatib aliwanukuu Mulokozi na Kihigi (1979:2), wakisema tamathali

za semi ni vifananisho au viwakilisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti au zinazofanana. Wakaendelea kwa kusema ni usemi wenye kupanua, kupuuza au kubadilisha maana za dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu iliyokusudiwa na mtunzi au mzungumzaji. Pia Senkoro (1984:13) ameeleza kuwa “tamathali za semi ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii ili kutia nguvu katika maana, mitindo na hata sauti katika maandishi ama kusema. Wakati mwingine hutumiwa kama njia ya kuipamba kazi ya fasihi na kuongeza utamu wa lugha”. Naye Mwamanda (2008:42) amesema tamathali za semi ni viwakilisho au vifananisho vya dhana fulani kwa dhana nyingine tofauti zinazofanana. Huu ni usemi unaobadilisha maana dhahiri au za kawaida za maneno ili kuleta maana maalumu ya fasihi iliyokusudiwa na msanii. Kwa hiyo tamathali za semi ni miongoni mwa kipengele cha lugha katika fasihi.

Kwa mtazamo huo wa Senkoro (ameshatajwa) na Mulokozi (ameshatajwa) pamoja na wataalamu mbalimbali wa fasihi wameonesha umuhimu wa lugha katika kazi za fasihi lakini bila ya kufanya ulinganishi wa vipengele hivyo. Hivyo basi riwaya ni miongoni mwa kazi za fasihi, nayo ili ikamilike ni lazima itumie lugha ya kifasihi. Na lugha ya fasihi hujengwa na vipengele mbalimbali. Kama vile:- methali, tamathali za semi, dhihaki, tafsida, shitizai (kinaya au kejeli), innuendo (kijembe), sitiari, tashibiha au mshabaha, tashihisi au uhaishaji, lakaabu, mubalagha, ritifaa, tabaini, takriri, ishara na kadhalika.

Juu ya yote hayo, kupitia riwaya za Kiswahili za Kezilahabi na riwaya za Shafi A. ni riwaya zinazokidhi matakwa ya matumizi ya lugha kwa kuwa na uteuzi mzuri wa matumizi ya lugha ya kifasihi, zinazoendana na matakwa ya jamii na kuonesha

namna waandishi hawa walivyotumia vizuri kipengele cha matumizi ya tamathali za semi katika kazi zao. Utafiti huu umechunguza matumizi ya lugha kwa waandishi wawili, mmoja kutoka upande wa Tanzania bara na mwengine kutoka upande wa Zanzibar. Ni utafiti linganishi uliochunguza matumizi ya lugha katika kazi ya fasihi na jinsi yanavyofanana na kutofautiana kati ya mwandishi E. Kezilahabi mwenye asili ya Tanzania bara ambapo lugha ya Kiswahili kwake ni lugha ya pili na Shafi A. Shafi mwenye asili ya Zanzibar ambapo lugha ya Kiswahili ndio lugha yake ya kwanza.

Ingawa watafiti wengi pamoja na wahakiki wa kazi za fasihi kama tulivyokwisha kuona hapo juu, wamechunguza na kuhakiki vipengele vya lugha vinavyotumika katika kazi za fasihi pasina kuvifanyia ulinganishi kati ya mwandishi mmoja na mwandishi mwengine, kwa mfano Salem (2013) katika utafiti wake wa shahada ya uzamivu ya Chuo Kikuu Huria; yeye amechunguza mahusiano ya lugha na vipengele vyengine vya fani katika tamthilia. Hata hivyo tatizo bado lipo la namna ya vipengele vya lugha hususani matumizi ya tamathali za semi ni kwa vipi vinalingana na kutofautiana, utafiti huu umechukuwa nafasi hio ili kuziba pengo hilo kwa kuchunguza mfanano na mpingano uliopo wa matumizi ya tamathali za semi kwa waandishi wawili kupitia vitabu teule.

Mtafiti aliona ipo haja ya msingi ya kufanya utafiti wa kina juu ya matumizi ya lugha ya kifasihi kupitia kipengele cha tamathali za semi katika riwaya mbili teule; ni riwaya ya *Kichwamaji* ilioandikwa na Kezilahabi pamoja na riwaya *Vuta n'kuvute* ilioandikwa Shafi A. Shafi.

1.2 Usuli wa Mada

Riwaya ni utanzu mmoja wapo miongoni mwa tanzu za fasihi andishi, ambapo mara nyingi huwa unaeleza mambo mbalimbali yanayohusu maisha ya wanadamu kwa mawanda mapana zaidi kuliko tanzu nyingine za fasihi. Kwa mtazamo wa Njogu na Chimerah (1999a), katika kulifanikisha suala la kuzungumzia mambo yanayohusu maisha ya wanadamu ndipo mwandishi huumba muhusika na kumbebesha visa na matukio mbalimbali yanayomuhusu mwanadamu katika maisha yake tokea kuzaliwa kwake hadi kufa. Mara nyingi visa na matukio ya wahusika huelezwa kwa mchangamano na mwingiliano ambapo kupitia riwaya mambo hayo huonekana zaidi kuliko tanzu nyingine za fasihi.

Waandishi huyawasilisha hayo kwa njia ya kuwabebesha wahusika wao dhamira mbalimbali na kuziwasilisha kwa kutumia kipengele cha lugha. Katika utafiti huu mtafiti amechunguza hayo matumizi ya lugha katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n'kuvute*, ni kwa vipi waandishi hawa wanavyofanana na kutofautiana katika matumizi ya tamathali za semi na namna wanavyowasilisha dhamira zao kupitia kipengele hicho.

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Katika nyanja ya utafiti na uhakiki wa riwaya ya Kiswahili, watafiti na wahakiki wengi kama Khatib (1986:1), Mulokozi na Kihigi (1979:2), Adam (2014) wameshughulikia fani na wengine maudhui katika riwaya na kugusia vipengele vya fani na maudhui na kuonesha jinsi vilivyo na umuhimu katika kukamilisha kazi za fasihi. Hata hivyo ziko tahakiki na tafiti zimefanywa juu ya riwaya za Kezilahabi na riwaya za Shafi A. Miongoni mwa watafiti hao ni pamoja na Sakkos (2008)

aliyeshughulikia udhanaishi katika riwaya ya *Kichwamaji*, Mlacha (1989) aliyehakiki vipengele mbalimbali vya fani na maudhui katika riwaya ya *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute* na Wamitila (1997) aliyeshughulikia kipengele cha motifu katika riwaya za Kezilahabi. Na wengine ni pamoja na Senkoro (1982), Msokile (1992), Mulokozi (1996) ambapo wamevitaja vipengele vya lugha kiujumla jumla katika riwaya hizo teule. Watafiti hawa kiujumla wameangalia vipengele vya matumizi ya lugha. Sasa suala la msingi linakuja, je ni vitabu hivyo tu vinavyoweza kusadifu maudhui kupitia fani? Ndipo mtafiti alipoamua kuchunguza matumizi ya lugha katika riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute* kwenye kipengele cha tamathali za semi kwa kuvifanyia ulinganishi na ulinganuzi pamoja na kuangalia dhamira zilizojitokeza kupitia tamathali hizo za semi.

1.4 Malengo ya Utafiti

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza matumizi ya lugha katika riwaya ya *Kichwamaji* na ile ya *Vuta n'kuvute*.

1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti

- (i) Kubaini mifanano iliyopo ya tamathali za semi katika riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*.
- (ii) Kubaini tamathali za semi zinazotofautiana katika riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*.
- (iii) Kuainisha dhamira zinazojitokeza kwenye tamathali za semi katika riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*.

1.5 Maswali ya Utafiti

- (i) Ni tamathali za semi zipi zinazofanana katika riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*?
- (ii) Ni tamathali za semi zipi zinazotofautiana katika riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*?
- (iii) Je! Ni dhamira zipi zinazojitokeza kwenye tamathali za semi katika riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unaleta manufaa makubwa kwa watumiaji wote wa lugha ya Kiswahili na hasa wanafunzi vyo kwani wanaweza kuibua matumizi ya tamathali za semi mbalimbali. Matokeo ya utafiti huu yana mchango mkubwa katika kujenga maaarifa ya ziada juu ya fasihi ya Kiswahili kwa upande wa riwaya na mwishowe kuweza kuelewa kufanana na kutofautiana kwa waandishi wawili tofauti kwenye kipengele cha matumizi ya lugha. Pia manufaa zaidi yanatarajiwa kupitia:-

Kitaaluma. Utafiti huu unaamsha ari kwa wanafunzi wa ngazi mbalimbali wa Chuo Kikuu Huria kufanya utafiti kama huu. Kwani watafiti wengi hasa wa zama hizi wamekua wakifanya utafiti kupitia vitabu vilivyoandikwa na waandishi wa zama hizi na kusahau kabisa waandishi wa zamani kama huyo Kezilahabi na wenzake. Pia utafiti huu utakuwa kama rejeleo muhimu kwa wanafunzi wa chuo kwani utawasaidia kugundua pengo kwa upande wao na kuiandikia mada ya utafiti kwa lengo la kuziba pengo hilo ambalo wao wameliona.

Kinadharia. Utafiti huu utakuwa kama rejeleo muhimu kwa wanafunzi kwa upande wa nadharia, kwani utawasaidia kujua namna nadharia za uhakiki na utafiti jinsi

zinavyoweza kuwasaidia katika tafiti zao, hasa nadharia ya simiotiki na nadharia ya udhanaishi. Na pia utafiti huu unatoa mchango mkubwa unaotokana na nadharia ya fasihi linganishi pamoja na mbinu za ulinganishi katika kazi za fasihi na mwisho utafiti huu utakuwa ni sehemu ya rejeleo kwa chuo kwenye upande wa nadharia ya fasihi linganishi.

1.7 Mipaka ya Utafiti

Katika kulifikia lengo la utafiti huu. Utafiti umeshughulikia kwenye upande wa fani katika vipengele vya matumizi ya lugha kwa kuchunguza tamathali za semi zilizotumika katika riwaya ya *Kichwamaji* iliyoandikwa na E. Kezilahabi na katika riwaya ya *Vuta n'kuvute* iliyoandikwa na Shafi A. Shafi. Ni utafiti wa fasihi linganishi na umebaki katika mipaka ya kitaaluma kwenye upande wa fani kwa kuchunguza kufanana na kutofautiana kwa matumizi ya tamathali za semi kama yalivyotumiwa na waandishi hawa wawili kupitia vitabu teule.

1.8 Mpangilio wa Kazi ya Utafiti

Utafiti huu umegawika katika sura tano. Nazo ni kama zifuatavyo:

- (i) Sura ya kwanza, mtafiti ameonesha utangulizi kwa ujumla unaohusu utafiti huu, kisha usuli wa tatizo la utafiti kuhusiana na suala la kuchunguza matumizi ya lugha katika riwaya ya *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*. Kisha mtafiti akaonesha tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, na umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na muhtasari wa sura ya kwanza.
- (ii) Sura ya pili, mtafiti ameonesha mapitio ya machapisho mbalimbali ya waandishi tangulizi na mkabala wa nadharia zilizotumika.

- (iii) Sura ya tatu, mtafiti ameonesha mbinu mbalimbali zinazotumika za kukusanyia data na njia ya kuchambuwa data na akaonesha njia aliyoitumia katika utafiti huu.
- (iv) Sura ya nne, mtafiti ameonesha uwasilishaji na uchambuzi wa data.
- (v) Sura ya tano, mtafiti ameonesha muhtasari wa kazi ya utafiti, mapendekezo ya utafiti na kumalizia na hitimisho.

1.9 Hitimisho

Katika sura hii ya kwanza ya utafiti wa kuchunguza matumizi ya lugha katika riwaya ya *Kichwamaji* na ile ya *Vuta n'kuvute*, vipengele vilivyokusanywa ni pamoja na usuli wa mada, usuli wa tatizo, tamko la utafiti, malengo ya utafiti, lengo kuu la utafiti, malengo mahsusi, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti na mpangilio wa kazi. Kwa ujumla katika sura hii mtafiti ameonesha namna kipengele cha matumizi ya tamathali ya semi kilivyo na mchango mkubwa katika uandishi wa kazi za riwaya. Kwani mtafiti amekusudia kuonesha mchango mkubwa uliotolewa na waandishi hawa wawili kupitia vitabu vyao teule katika nyanja ya fasihi hasa katika kipengele cha matumizi ya tamathali za semi.

SURA YA PILI

MAPITO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Katika sehemu hii mtafiti ameangalia / amepitia kazi mbalimbali za waandishi mbalimbali kuhusiana na mada hii ili kugundua, nini wamesema, nini wameona, na nini wamependekeza. Na pia ameangalia ni yepi kwa upande wao hawakuyatazama na mwishowe mtafiti akayashughulikia katika yale watangulizi hawakuyatazama. Kwa kupitia maandiko hayo na machapisho ya waandishi tangulizi mtafiti aligundua kuwa matumizi ya tamathali za semi katika riwaya ya *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute* bado hayajafanyiwa utafiti na hivyo kuna pengo la kimaarifa linataka lizibwe.

2.2 Kazi Tangulizi Zinazohusu Ufanyaji wa Utafiti.

Mtafiti ameanza kwa kupitia vitabu mbalimbali vinavyohusu muongozo wa ufanyaji wa utafiti. Miongoni mwa vitabu alivyopitia ni kama; Kitabu kinachohusu maswali ya utafiti kinachoitwa: *Research Questions*. Kilichoandikwa na Andrews (2003), alizungumzia mbinu mbalimbali za kutayarisha maswali kwa ajili ya utafiti. Kitabu hiki kiliweza kumsaidia mtafiti kuandaa maswali kulingana na mada ya utafiti huu. Thung na wenzake (2010), walizungumzia ufanyaji wa utafiti wa kielimu (research in education). Pia Shumbusho (2003), alionesha mbinu za uandhishi wa ripoti ya utafiti. Ambapo mtafiti amezitumia mbinu hizo za uandishi wa ripoti ya utafiti wake na kuweza kukamilisha kazi yake kwa ufanisi zaidi.

Vile vile Kiango na Mdee (1995:14-22) wameonesha njia za ukusanyaji wa data maktabani kwa zile mada ambazo utafiti wake utafanyika na kuishia maktaba. Kwa

mfano udurusu wa kamusi ya Kiswahili, utafiti wa vipengele vya fani kwa riwaya / uandishi ambao bado haujafanyiwa uhakiki au utafiti. Waandishi hao wamejaribu kuonesha njia za ufanyaji wa utafiti wa kimaktaba na kuonesha matatizo ya utafiti kama huo na namna ya kuyatatua matatizo hayo. Kwa kupitia Kiango na Mdee (wameshatajwa) mtafiti amenufaika sana katika kukamilisha kazi yake, kwani utafiti huu ni utafiti wa kimaktaba hivyo kwa muongozo wa Kiango na Mdee (wameshatajwa) mtafiti ameweza kukusanya data zake kwa kuvipitia vitabu teule na kuorodhesha tamathali za semi zilizotumika na waandishi hawa wawili. Na kwa mbinu hii mtafiti ameweza kukamilisha vizuri kazi yake.

2.3 Kazi Tangulizi Zinazohusu Fasihi Linganishi

Mtafiti ameendelea mbele kwa kuangalia wanataaluma mbalimbali walioandika kuhusiana na utafiti linganishi. Baadhi ya wataalamu walizungumzia dhana hii ya ulinganishi, na miongoni mwa wataalamu hao ni kama, Ponera (2014:39-66), yeye amekuwa kama mzinduzi wa fasihi linganishi ya Kiswahili kwa kuandika kitabu alichokiita: *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*, ndani yake ameonesha maana, chimbuko na nyanja za fasihi linganishi. Ingawa hata hivyo ameacha baadhi ya mapengo yanayohusiana na dhana hii ambayo yanahitaji kuzibwa na wataalamu wa fasihi ya Kiswahili. Lakini hata hivyo kitabu chake kimetoa mchango mkubwa katika kukamilisha kazi hii ya utafiti linganishi.

Pia Sanz na Romero (2007), wamezungumzia juu ya fasihi linganishi na sayansi na teknolojia na kuelezea kuongezeka kwa kasi kwa mawasiliano katika karne ya 20, kumetoa mchango mkubwa katika fasihi linganishi katika kipindi hiki cha mabadiliko ya kisayansi. Ingawa Sanz na Romero wameenda ndani zaidi na

ulinganishi wa sayansi na teknolojia katika fasihi lakini kazi zao zimemsaidia mtafiti katika kujua mbinu nyingine za ulinganishi ambazo amezitumia wakati wa kuchambua data kwa njia ya ulinganishi na ulinganuzi.

Naye Zepetnek (1998) ambaye anachukuliwa kama gwiji wa taaluma hii ya fasihi linganishi. Zepetnek (ameshatajwa) ameonsha misingi kumi (10) ya fasihi linganishi na kueleza namna fasihi linganishi inavyoweza kutumika katika kazi mbalimbali za kifasihi pamoja na masomo mengine mbalimbali. Pia ameengeza kuwa nadharia ya fasihi linganishi si tu kama nadharia bali pia inatazamwa kama nyenzo ya kuchanganua na kushughulikia masuala mengine ulimwenguni. Zepetnek (ameshatajwa) ametoa mchango mkubwa katika kazi hii ingawa hakutaja moja kwa moja ulinganishi wa matumizi ya lugha katika kipengele cha tamathali za semi lakini nadharia alizotaja katika ulinganishi zimemsaidia mtafiti katika kipengele hicho.

Naye Wamitila (2003:179), ameonsha matumizi ya mbinu ya ulinganishi na akasema wakati mwengine mtafiti analazimika kutumia mbinu hii linganishi iwapo atakua anahusisha masimulio kadhaa yanavyohusiana na masimulio fulani Ingawa yeye ameonsha katika fasihi simulizi lakini pia ni miongoni mwa muongozo mzuri wa ufanyaji wa kazi za fasihi linganishi kwa ujumla.

Kwani mtafiti ameweza kupata mbinu mbadala za kulinganisha katika kazi za fasihi andishi kwa kuzichunguza mbinu za fasihi simulizi na kuona nazo zinaweza kutumika katika ulinganishi wa fasihi andishi kwa kutumia mbinu ya linganishi kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi.

2.4 Kazi Tangulizi Zinazohusu Riwaya kwa Ujumla

Baada ya hapo mtafiti ameendelea kwa kuangalia maana ya riwaya kama ilivyoielezwa na wataalamu mbalimbali. Kwani utafiti huu, mtafiti ametafiti riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n’kuvute*, mtafiti amona ipo haja ya kuanza kuangalia maana ya riwaya na chimbuko lake ingawa wahakiki na watafiti wengi wametoa maana inayolingana lakini hata hivyo wamehitilafiana kwa baadhi ya mambo. Tukianza na TUKI katika *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (2004). ”riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni iliyoandikwa kwa maandishi ya nathari, aghalabu inaeleza ukweli fulani wa maisha”. Na pia kwa mujibu wa *Kamusi la Kiswahili Fasaha* BAKIZA (2010) “riwaya ni utungo mrefu wa kubuni wenye visa changamano ulioandikwa kinathari na wenye kusawiri hali halisi ya mwenendo wa jamii”. Kwa mujibu wa fasili hizo ni wazi kuwa kila utungo mrefu wa kubuni ulioandikwa kinathari na wenye kuzungumzia visa changamani tutauita riwaya. Kwa kiasi fulani maana hizi mbili zimejitosheleza ila zina uvulivuli kidogo kwani kuna tungo nyingi zilizo refu na zimezungumzia visa changamano lakini zipo katika utanzu wa hadithi.

Kwa mujibu wa Mulokozi (1996:149), “riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni yenye mawanda mapana, lugha ya kinathari, mchangamano wa visa na dhamira, wahusika kadhaa, na matukio yaliyosukwa kimantiki, yenye kufungamana na wakati na kushabihiana na maisha halisi”. Fasili hii ya Mulokozi (ameshatajwa) mtafiti anakubaliana nayo kwani kwa kiasi fulani imeweza kukusanya sifa zinazoikamilisha riwaya. Lakini hata hivyo kwa upande wa kinathari tumeona hapo mwanzoni kuwa riwaya zilikuwepo tokea zamani ila zilikuwa zikiwasilishwa kwa njia ya tendi. Kwa mujibu wa Mulokozi (ameshatajwa).

Naye Mlacha na Madumulla (1991:1) katika kutoa maana ya riwaya amesema: “riwaya ni hadithi iliyotungwa ambayo ina urefu wa kutosha, visa vilivyooana na ambayo imezingatia suala la muda”. Kupitia maana hii bado tunaona Mlacha na Madumulla (wameshatajwa) wakisisitiza riwaya kuwa katika muundo wa kinathari kwani waliposema kama riwaya ni hadithi, wakimaanisha ni mfumo wa kinathari. Hivyo maana yao bado inalingana na wataalamu wengine na kwa kiasi fulani maana hii ina utoshelevu.

Kwa upande wa Ntarangwi (2004:59), yeye alitoa maana ya riwaya kwa kusema ni “utungo wa kinathari uliobuniwa na ulio na urefu wa kiasi kinachoweza usawiri wa wahusika na matendo yao ili kuwakilisha uhalisi wa maisha ya jamii husika katika ploti maalumu”. Katika maana hii tunaona kipengele cha urefu amekitaja ila ameshindwa kuonesha huo urefu wa kiasi, kwani kiasi kipo kwa kila mtu, na kila mtu anakuwa na kiasi chake kulingana na kipimo cha mtu huyo. Hivyo Ntarangwi (ameshatajwa) alipaswa kutaja ukubwa wa hicho kiasi ama kwa kutaja idadi ya maneno, idadi ya sura katika riwaya au hata kutaja idadi ya kurasa.

Pia Wamitila (2002b:5) ameeleza maana ya riwaya kuwa “ni kazi iliyoandikwa kwa mtindo wa kinathari ambayo ina urefu wa kiasi fulani. Ni pana, ina uchangamano wa kimtindo na kidhamira na inashughulikia masuala kadhaa katika mtazamo mpana wa wakati’. Tukiitazama kiundani fasili hii ya Wamitila tunaikuta ina mapungufu katika baadhi ya mambo, kwani haikuweka wazi urefu, urefu ni wa kiasi gani, ingawa wako baadhi ya wataalamu wameeleza riwaya lazima ifikishe idadi ya maneno elfu sitini (60,000) lakini ni riwaya chache zilizofikisha idadi hiyo ya maneno. Na ndio maana Wamitila akarudi tena (2003:187) akatoa fasili nyingine ya riwaya kwa kusema

“riwaya ni kazi ya kubuni na kuhusisha binadamu au wanyama (wahusika) ambao wanatenda mambo fulani kwa ukamilifu fulani na matukio yake huhusika kipindi au wakati fulani”. Na pia Muhando na Balisidya (1976) wamesema riwaya inaanzia na maneno 35,000 na hili kulingana na wahakiki wengine juu ya kazi ya kubuni au hadithi iliyotungwa kutokana na uwezo wa fanani. Maelezo haya ni yamsingi sana kwa mtunzi yeyote kwani yeye ndiye anayeijua hadhira yake, lakini hata hivyo Kezilahabi (1983:235) yuko kinyume na maelezo hayo kwani yeye anasema:- “Kwa bahati hivi sasa hatuwezi kusema kuwa kuna riwaya ya Kiswahili ambayo haieleweki kabisa kwa watu; ingawa dalili za kuanza kuandika riwaya na hadithi fupi zisizoeleweka kwa urahisi zimeanza kuonekana. Jambo ambalo ningependa kuonya hapa ni kuwa, mwandishi wa riwaya asisukumwe kuandika riwaya kwa ajili ya watoto wa shule. Riwaya si kitabu cha kiada na si cha ziada. Mwandishi wa riwaya si mtu wa kufungwa, lakini si mtu anayeweza kuruhusiwa kusema chochote kila anachotaka awe hana mipaka”

Na Njogu na Chimerah (1999b:35) wametoa maana ya riwaya kwa kusema ni utungo mrefu wa kubuni, na wenye ploti, uliotumia lugha ya nathari. Katika maana hii wamesisitiza utungo huo uwe na ploti, na ploti inahusisha maingiliano ya vitushi kwa namna vinavyoingiliana na kuzuana na kusababishana. Yaani ni mfuatano wa matukio yanayojenga riwaya. Na hailazimishwi riwaya kuwa na mfuatano wa visa wa moja kwa moja yaani mwanzo wa riwaya hadi mwisho, bali pia riwaya inaweza kuwa katika mtindo wa rejea rejea.

Baada ya kuangalia maana ya riwaya sasa tuangalie historia kwa ufupi au chimbuko la riwaya kama inavyoelezwa na waandishi wengi. Tukianza Mulokozi (1996:149)

“riwaya zilizuka kutokana na fani za kifasihi zilizokuweco kabla yake, hususani zile za kihadithi, na kwamba ilipata msukumo kutokana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia yaliyotokea Ulaya katika karne za 16 hadi 18”. Hata hivyo tayari tumekwishaona kuwa riwaya zilikuwepo kabla ya hata hiyo karne ya 16 ila zilikuwa zikiwasilishwa kwa mfumo wa mashairi ya nyimbo, na pia tumeona si masimulizi ya kihadithi peke yake bali pia mashairi ya nyimbo za zamani nayo yalisababisha kutokea kwa riwaya.

Kwa upande wa chimbuko la riwaya ya Kiswahili, kama ilivyozungumzwa na Mlacha na Madumulla (1991:11) “...historia ya riwaya ya Kiswahili ni muhimu kuhusisha na fasihi simulizi. Uhusiano huo sio wa kimuundo, ingawa muundo wa masimulizi ulichangia kwa kiasi katika riwaya za mwanzo, lakini zaidi ulitokana na uandishi wa hadithi za Kiswahili. Edward Steere alipozikusanya na kuhariri hadithi alizopata kutoka kwa wakaazi wa Zanzibar...” Mbali na kauli hiyo ya Mlacha na Madumulla (wameshatajwa) juu ya historia ya riwaya kuwa inahusiana sana na fasihi simulizi. Lakini Madumulla (2009) amekuja tena na kauli nyingine ya ziada juu ya chimbuko la riwaya, akieleza riwaya ilitokana na nathari bunilifu kama vile hadithi, hekaya na ngano zilizosimuliwa tangu kale. Kwa ajili hiyo riwaya ililetwa na fani ya ushairi kupitia tendi za zamani zilizoandikwa kwa hati za kiarabu kwa matamshi ya Kiswahili kwani kwa wakati huo ndio uandishi uliokuweco pwani ya Afrika ya Mashariki. Kwa ajili hiyo historia ya riwaya inafungamana sana na historia ya watu wa pwani ya Afrika ya Mashariki.

Kwa mujibu wa <http://chombez.blogspot.com>, kuwa riwaya ya Kiswahili ilianza tokea wakati wa ukoloni wa Kiingereza na riwaya ya kwanza ya Kiswahili ni Uhuru

wa Watumwa iliyotungwa na James Mbotela (1934). Baadae zikafuata riwaya za kina Shaaban Robert. Mara baada ya uhuru wakaibuka waandishi wengi chipukizi akina Kezilahabi, Mohamed Suleiman, Senkoro na kadhalika na ndio kipindi ilipoandikwa riwaya ya *Kichwamaji*. Kwa mujibu wa Mabala na Richard (2002) “miaka ya 1990-2000 waliibuka waandishi wengi na kuandika dhana mbalimbali kama vile usaliti, mapenzi, ugonjwa wa ukimwi, rushwa na kadhalika. Kwa lengo la kufichua uovu uliomo ndani ya jamii”. Na ndio kipindi ilipoandikwa riwaya ya *Vuta n’kuvute*.

2.5 Kazi Tangulizi Zinazohusu Vitabu Teule

Baada ya hayo; mtafiti aliangalia mapitio mbalimbali yanayohusiana na mada kwenye upande wa uandishi wa riwaya za Kezilahabi na uandishi wa riwaya za Shafi Adam. Na alianza na Wanakikundi cha Under Tree (2013), wameizungumzia riwaya ya *Kichwamaji* kama ni moja ya riwaya iliyojikita zaidi katika nadharia ya udhanaishi. Kwani ndani yake imezungumzia matatizo yanayomsibu mwanadamu na kukwepa imani ya kinjozi juu ya maana ya kuishi, mwandishi anakwepa kueleza kwanini mtu azaliwe, ateseke kisha afe. Lakini hata hivyo hawakuzungumzia chochote juu ya riwaya ya *Vuta n’kuvute* si kwa upande huo wa nadharia ya udhanaishi wala ulinganishi mwengine.

Naye Shayo (2011) yeye alifanya utafiti linganishi na akahusisha riwaya ya *Vuta n’kuvute* na riwaya ya *Nyota ya Rehema*. Aliangalia upande wa maudhui na kutazama kwa kulinganisha mitazamo ya waandishi hawa na wanajamii juu ya mimba za watoto wa nje ya ndoa. Lakini aliacha pengo kwenye utafiti wake la kulinganisha upande wa fani kwenye matumizi ya lugha kwani jambo hilo

hakulishughulikia. Hivyo mtafiti ameona ipo haja ya kufanya utafiti huu linganishi kupitia vitabu teule kwenye matumizi ya lugha.

Low (2011), katika utafiti wake katika ngazi ya uzamili ameandika juu ya athari ya lugha katika kuibua dhamira. Amezungumzia vipengele mbalimbali vya lugha na kutolea mfano kutoka katika nyimbo za kizazi kipyua zinazohusu UKIMWI. Miongoni mwa vipengele vya matumizi ya lugha alivyovitaja ni pamoja na tafsida, tashibiha, taswira na kadhalika. Lakini kwa upande wa kuvilinganisha vipengele hivyo na kitu kingine hakuzungumzia chochote.

Mwingine ni Prof. Joseph Mbele ambaye, kwa mujibu wa <http://hapakwetu.blogspot.com>, amezungumzia wasifu na uhodari wa Shafi Adam Shafi katika uandishi wake wa riwaya ya *Vuta n'kuvute* namna alivyoweza kutumia vyema kipengele cha matumizi ya lugha. Kwani ndani ya kazi yake mumejaa vionjo vingi vya lugha ya fasihi kama matumizi ya tamathali za semi. Wataalamu wengine walioonesha mchango mkubwa wa Shafi A. katika kazi zake za riwaya na namna unavyowasilisha matumizi ya lugha katika riwaya. Kwa mfano, Mussa (2007) katika utafiti wake wa kuchunguza mchango wa suala la ukombozi katika riwaya za Shafi A. ambapo alichunguza suala hilo kupitia riwaya za *Kuli* (1977), *Kasri ya Mwinyi Fuadi* (1978) pamoja na *Vuta n'kuvute* (1999) na kuweza kubaini aina za ukombozi zilizojitokeza katika riwaya teule na kubaini mchango wa mwandishi katika kuleta ukombozi kwa maendeleo ya Zanzibar. Adam (2014) wakati alipochunguza dhamira za kijamii na kiutamaduni katika riwaya za Kiswahili ngazi ya uzamivu aliweza kubaini dhamira za kijamii na kiutamaduni pamaoja na kutathmini uhalisia wa dhamira za kijamii na kiutamaduni kupitia riwaya za Shafi A. Yeye alitumia riwaya

ya *Kuli* na *Vuta n'kuvute*, mwishowe ameweza kugundua mbinu za kisanaa zilizotumiwa na mwandishi wa riwaya hizo katika kusawiri dhamira za kijamii na kiutamaduni. Dhamira hizo amezitoa kupitia kipengele cha lugha na hivyo inadhihirika wazi kuwa Shafi A. ni mtunzi mahiri katika utumiaji wa lugha katika kazi zake. Kupitia watafiti / wahakiki hao walitoa mchango mkubwa katika utafiti huu kwa kutoa muongozo wa matumizi ya lugha yaliyotumiwa na mwandishi kupitia riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Pia Kharifa (2013), naye alifanya utafiti linganishi kwa kuchunguza kufanana na kutofautiana kwa fani na maudhui katika methali. Mtafiti huyu alilinganisha kati ya methali za Kitanzania na methali za Kilibya namna zinavyofanana na kutofautiana katika upande wa fani na maudhui. Na kwa kupitia utafiti huu mtafiti ameweza kubaini na kumsaidia kujua baadhi ya mbinu linganishi na linganuzi katika kazi za fasihi. Lakini upande wa matumizi ya lugha katika utafiti linganishi Kharifa (ameshatajwa) hakugusia jambo hilo, na ndio maana mtafiti huyu wa utafiti linganishi alilishughulikia jambo hilo.

Asha (1981:77) yeye alizungumzia fasihi simulizi na fasihi andishi kwa ujumla, na alionesha tofauti zilizopo kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi. Mwandishi huyu alitaja fasihi hizi zinatofautiana kwa mambo kumi na saba (17). Lakini kwa upande wa mfanano hakugusia. Hiyo ndio sababu ya mtafiti kuziba pengo hili lililoachwa na waandishi wa fasihi. Licha ya Asha (ameshatajwa) kuzungumzia tofauti za fasihi simulizi na fasihi andishi, pia Senkoro (2006:22-38) ameona makutano baina ya fasihi simulizi na fasihi andishi ni namna ya utolewaji wa fasihi simulizi ambao hutegemea sana kipengele cha lugha na kusisitiza zaidi katika matumizi ya taswira

na lugha ya ishara, hasa katika tanzu za ngano, methali, vile vile na habari za kimafumbofumbo, ambapo ndani yake yamejaa matumizi ya tamathali za semi zenye kufananisha watu na vitu au vitu vya aina moja na vya aina nyingine. Kwa mtazamo huu ni dhahiri kuwa matumizi ya tamathali za semi zina mchango mkubwa katika kukamilisha kazi za riwaya za Kiswahili.

Naye Sauda (2007), alizungumzia matumizi ya lugha katika nyimbo za waganga na kugundua kuwa nyimbo hizo kwa kawaida zinatumia lugha ya kifasihi katika kipengele cha mafumbo. Na kupitia mafumbo hayo ndio ujumbe unapatikana kwa jamii husika na hudhihiri dhamira mbalimbali kupitia kipengele hicho cha mafumbo, na kwa upande wa utafiti huu matumizi ya tamathali za semi ni moja kati ya kipengele cha lugha nacho kinatoa dhamira mbalimbali zenye maufaa kwa jamii. Lakini hata hivyo mafumbo ni sehemu moja tu katika sehemu nyingi za kipengele cha matumizi ya lugha na mtafiti hakugusia upande wa sehemu nyingine za matumizi ya lugha, hivyo imeonekana kuwa ni mapungufu ya Sauda (ameshatajwa) ambapo mtafiti huyu aliyapitia kwa kina.

Kwa upande wa kazi za Kezilahabi, wapo watafiti na wahakiki wengi waliozishughulikia kwa kutumia nyanja mbalimbali. Wako waliofanya ulinganishi wa kazi za Kezilahabi na kazi za waandishi wengine, na wako waliofanya kwa kazi za Kezilahabi zenyewe kwa zenyewe. Miongoni mwa hao ni Mosha (2013) katika utafiti wake wa wahusika Padri katika riwaya za Kezilahabi katika ngazi ya Uzamili. Mosha (ameshatajwa) ametafiti kupitia riwaya za *Rosa Mistika* (1971), *Gamba la Nyoka* (1979) na *Nagona* (1990). Kupitia riwaya hizo mtafiti amezungumzia muhusika Padri na uhusika wake jinsi alivyowasilishwa katika riwaya za Kezilahabi

na kuonesha dhamira mbalimbali zilizowasilishwa na muhusika Padri. Vile vile kubaini motifu inayojitokeza kupitia muhusika Padri katika riwaya hizo. Na Mwangoka (2011) alikuja kuziba pengo la Mosha (ameshatajwa) juu ya suala la motifu za safari za makuzi ya wahusika. Yeye ametafiti riwaya za *Rosa Mistika* na *Dunia Uwanja wa Fujo* na kufanikiwa kutafiti na kuchambua motifu za msako na safari za wahusika kama zilivyojitokeza katika riwaya za Kezilahabi. Vile vile alionesha ni kwa kiasi gani matatizo wanayopambana nayo wahusika wakiwa watu wazima kama yanahusiana na kurukwa kwa hatua za makuzi ya utotoni mwao. Lakini kwa upande wa riwaya ya *Kichwamaji* hawakugusia kipengele chochote.

Naye Senkoro (1996:92) alionesha namna mwandishi Kezilahabi jinsi anavyowasilisha kazi zake, kwa upande wa uchojarishaji katika kazi za kezilahabi ulianza katika zile kazi za mwanzo za *Rosa Mistika*, *Kichomi* na *Kichwamaji*. Kazi za riwaya hizi zinajishughulisha na maana ya maisha kwa kutumia mazingira ya vijiji na miji ya Tanzania. Lakini kwa jicho la kidhanaishi (existentialism) huyaona maisha ni kitu kisicho na maana na ndio maana wahusika wa Kezilahabi huamua kujiua kutokana na nadharia hii kwa kuona maisha si kitu chochote.

Mfano muhusika Kazimoto na Rosa. Na wakati mwengine wahusika huamua kujitenga na maisha na kuwa buruda (Charles). Akahakiki kwa mara nyingine tena Senkoro (2011c:83) kwa kushughulikia riwaya ya Kezilahabi ya *Dunia Uwanja wa Fujo* kwa upande wa maudhui na alibaini kuwa mwandishi alishughulikia zaidi upande wa migogoro, matatizo, na mikinzano ya jamii, kiuchumi, na kifalsafa katika jamii. Akaendelea kufafanua na kuionesha Tanzania baada ya Azimio la Arusha na kuibua dhamira mbalimbali zilizojitokeza katika riwaya hiyo katika kipindi hicho, na

dhamira hizo ni kama vile malezi na athari za kijamii juu ya malezi, mivutano baina miji na vijiji, nafasi ya mwanamke katika jamii, mapenzi na ndoa na falsafa kuhusu maisha. Haya ni kwa upande wa Senkoro (ameshatajwa) juu ya riwaya za Kezilahabi. Hata hivyo ameacha pengo katika kulinganisha na kutofautisha kupitia vipengele vya matumizi ya lugha.

Pia Mlacha (1989) amezungumzia juu ya matumizi ya lugha ya sitiari katika kazi za Kezilahabi na kutolea mfano kupitia riwaya ya *Rosa Mistika* na kueleza kuwa kupitia riwaya hii mwandishi ameweza kuwasilisha dhamira mbalimbali kutokana na kipengele hiki cha matumizi ya sitiari na kuweza kurejelea mambo kadha wa kadha yenye kujenga dhamira. Mwandishi alipomnukuu Rosa akisema “mwezi mkubwa ukimwangalia mlangoni”. Hii ni sitiari ambayo ina maana ya kuwa mambo anayoyafanya Rosa yote yanaonekanwa hadharani. Kupitia mawazo haya ya Mlacha (ameshatajwa) yatamsaidia sana mtafiti katika kazi yake ya kuibua dhamira zinazotokana na matumizi ya tamathali za semi zilizotumika katika vitabu teule. Naye Wamitila (2007) akiunga mkono maneno ya Mlacha hapo juu, yeye aliandika juu muundo wa usimulizi wa matumizi ya sitiari katika riwaya za Kezilahabi. Kwa upande wake alitolea mfano riwaya ya *Nagona* na *Mzingile* na kuonesha miundo hiyo jinsi inavyoweza kujenga dhamira na kuibua maudhui mbalimbali kupitia riwaya hizo teule. Aliendelea kusema matumizi ya sitiari za miujiza zilizotumiwa na Kezilahabi katika riwaya hizi ni jambo la kawaida mno. Maelezo hayo ya Wamitila (ameshatajwa) juu ya usimulizi na matumizi ya sitiari ni muhimu sana katika utafiti huu kwani yaliweza kutoa mchango mkubwa katika kuibua dhamira zinazojengwa na tamathali za semi.

Wamitila (2006a:28) akiunga mkono maelezo ya hapo juu kuhusiana na mazingira katika riwaya za Kezilahabi. Anasema kwa upande wake riwaya za *Gamba la Nyoka*, *Rosa Mistika*, *Kichwamaji* na *Dunia Uwanja wa Fujo* zimeegemezwa katika mandhari ya kijijini. Haya ni mazingira anayoyafahamu vizuri sana mwandishi na yanachangia sana katika kuzipa riwaya hizo mandhari zenye mguso pamoja na kuimarisha ushabahi wake na kwa njia hii, Kezilahabi kazipa nguvu kubwa riwaya zake ya uhalisia wa kisimulizi. Maelezo hayo ya Mlacha, Senkoro na Wamitila (wameshatajwa) yalimsaidia mtafiti katika uchaguzi wa nadharia ya utafiti na kupelekea kuchagua nadharia ya udhanaishi ambayo ndio iliyomuongoza mtafiti katika utafiti wake huu.

2.6 Mkabala wa Nadharia

Mkabala wa nadharia za kihakiki na kitafiti ni nyenzo muhimu katika kazi ya uhakiki na utafiti. Lakini ifahamike kwamba nyenzo hii kazi yake kubwa ni kumsaidia mhakiki / mtafiti kufikia lengo la kazi yake. Kwa kawaida nadharia hutumika kulingana na kazi ya fasihi iliyopo kwani nadharia hizi zina ufaafu kwa baadhi ya dhamira na wakati mwingine zina mapungufu kwa baadhi ya dhamira. Pia nadharia hizi zinazuka kulingana na mazingira fulani kwa wakati huo. Na nadharia za kihakiki / kitafiti ziko nyingi na huathiriana zenyewe kwa zenyewe kwa kiasi kikubwa. Mtafiti aliongozwa katika kazi yake ya utafiti huu na nadharia kuu mbili, nazo ni nadharia ya Simiotiki na nadharia ya Udhanaishi.

2.6.1 Nadharia ya Simiotiki / Umatini

Nadharia ya Simiotiki kwa mujibu wa Wamitila (2002:132), inatokana na neno Simiotiki / Umatini lenye asili ya Kiyunani lenye maana ya ishara na ambalo hutumiwa kuelezea mielekeo ya makundi fulani ya kihakiki.

Mwanzilishi wa nadharia ya Simiotiki ni mwana isimu wa Ki-Swizi, Ferdinand de Saussure (1857-1913) wakati alipokuwa akitafiti mienendo ya lugha za wanadamu. Ferdinand de Saussure aligundua kuwa katika kuipata maana ya maneno katika lugha huwa kuna mahusiano ya vitu viwili navyo ni kitaja na kinachorejelewa. Pia nadharia hii imeungwa mkono na mwanafalsafa wa Kimarekani ajulikanae kama Charles Pierse. Yeye amehusisha katika kuipata maana ya maneno katika lugha kwa vitu vitatu navyo ni yambwa, ishara na yambiwa. Lakini wana nadharia hii wanaamini kuwa kiashirii kikawa polisemi ingawa kimekuwa kile kile bali kinachoashiriwa kikawa tofauti. Wakapiga mfano utowaji wa zawadi wa mvinyo kwenye jamii ya ulaya. Zawadi hii inaweza kuwa ni urafiki, upole, ukarimu, pongezi, mapenzi au wema. Naye Dino (2002), alionesha kwa mifano namna ya nadharia ya simiotiki inavyoweza kusaidia katika kukupatia maana ya kitu zaidi ya maana moja. Kwani aliweza kuvunja vunja matini katika sehemu ndogo ndogo alizoziita leksia na kuweza kuthibitisha kuwa kila leksia moja ina maana tatu au zaidi zinazopatikana na msomaji wa matini.

Nadharia hii inaungwa mkono na wataalamu wengi wa lugha kutokana na msingi wake wa kuhusisha vitu vitatu. Miongoni mwa wataalamu hao ni pamoja na Wanashule ya Prague, Umberto Eco, Greimas, Todorov na Roland Barthes. Pamoja na hao Wamitila (ameshatajwa) naye pia anaunga mkono dhana hii na kusema maana ya kitu hujulikana zaidi na wanajamii husika na namna wanavyotafsiri. Na kutolea mifano ya tahakiki mbalimbali za riwaya za Kiswahili. Nadharia hii imetumiwa na watafiti na wahakiki mbalimbali kama vile Salem (ameshatajwa) katika utafiti wake wa Shahada ya Uzamivu ya Chuo Kikuu Huria Tanzania.

Pia Adam (ameshatajwa) alitumia nadharia hii ya simiotiki na kuweza kumsaidia sana katika kazi yake ingawa yeye alikuwa akichunguza dhamira za kijamii na kiutamaduni lakini alifanikiwa kukamilisha kazi yake kupitia nadharia hii. Mtafiti anaamini kuwa itamsaidia kwani moja kati ya vitabu alivyofanyia utafiti Adam (keshatajwa) ni kitabu cha riwaya ya *Vuta n'kuvute*. Pia Rugebandiza (2011) aliitumia nadharia hii ya simiotiki na kuweza kumsaidia katika utafiti wake kwani aliweza kubainisha vigezo vya matini vya kifasihi kwa kutumia ishara. Na mtafiti alitumia riwaya katika kazi yake, na kwa kiasi fulani mbinu walizopita Adam na Rugebandiza katika kukamilisha kazi zao ndizo mtafiti alizipita ili kukamilisha vyema kazi yake. Kwani ukitazama katika riwaya za Shafi A. utakuta hutumika ndani yake lugha ya picha, tamathali za semi, sitiari na kadhalika. Na nadharia hii inatoa muongozo wa matumizi ya vitu zaidi ya kimoja na namna inavyohamisha maana.

Kimsingi, nadharia hii mtafiti anakubaliana nayo kutokana na kuwa lugha siku zote inakuwa na vitu viwili; kiashirii na kiashiriwa, hivyo ni wazi kuwa hakuna uhusiano wa moja kwa moja wa neno lililotajwa kwa kiashiriwa. Na kwa upande wa kazi za fasihi waandishi hutumia misimbo mbalimbali kwa ishara au matukio na kuweza kuhamisha maana halisi waliyoikusudia kutoka katika neno maalumu kwa hadhira. Kwa mfano TAKILUKI (1997) kupitia mashairi ya *Malenga Wapya* katika shairi la Hali Halisi; mshairi amesema: “mshumaa unawaka mbona giza linazidi”. Mshairi ametumia neno mshumaa akimaanisha uhuru na neno giza akimaanisha matatizo / hali ngumu katika jamii. Kwa kupitia mfano huo wa lugha ya picha unadhihirisha wazi kuwa hadhira au wasikilizaji wanaweza kuwa na maana nyingi. Hivyo hadhira

ili aweze kuipata maana kisimiotiki ni lazima atafakari sana matumizi hayo ya lugha yaliotumika na mwandishi yanaleta tafsiri gani?

Ili kuweza kujibu maswali ya utafiti huu, ndipo mtafiti akatumia nadharia hii kwa kuzingatia misimbo mbalimbali iliyomo katika vitabu teule vya utafiti huu hasa ukizingatia matumizi ya tamathali za semi na namna zinavyotoa dhamira mbalimbali na mwisho wake mtafiti akaibuka na dhamira 22 zilizotokana na tamathali za semi.

2.6.2 Nadharia ya Udhanaishi

Udhanishi ni dhana inayotumika kuelezea falsafa ya kuwako na maisha. Dhana hii inatumika kuelezea maono au mitazamo inayohusiana na hali ya maisha ya binadamu, nafasi na jukumu lake ulimwenguni na uhusiano wake na Mungu. Kwa mujibu wa Wamitila (2003) “Udhanishi ni dhana inayotumiwa kuelezea falsafa ya kuwako na maisha”. Pia dhana hii ina mtazamo wa kujumuisha masuala maisha ni nini? Maisha yana maana gani kwa binadamu? Na kwa njia gani mwanadamu anaweza kubadilisha maisha yake yaliyojaa dhiki, mashaka na huzuni. Alienda mbele zaidi Wamitila (2006b:122) aliona kuwa mawazo ya nadharia ya udhanishi yaliyojitokeza katika riwaya za Kezilahabi na kusema “...wanachunguza jinsi masharti wanayojipangia wanadamu wanavyoathiri maisha na uhuru wa mtu binafsi. Kwa mfano katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* tunaona jinsi mawazo yanahusu ujamaa yanavyoingilia uhuru wa tumaini kama muhusika ambaye anaonekana kama kielelezo cha unyonyaji unaopingwa na itikadi za kijamaa”.

Na kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (wameshatajwa), wakimnukuu mdhanishi Jean Paul Sartre akisema juu ya udhanishi ni dhana inayohusu mtu huzawa au

hujipata ametumbwika kwenye ombwe la aina fulani. Yuko huru kuishi tu katika ombwe hilo au kuishi huku akikabiliana vilivyo na ulimwengu uliomzunguka, kwa kuwa hana uwezo juu ya masuala kama maumivu na mateso, anaweza kukata tamaa. Hata hivyo, kabla ya kukumbwa na mauti, mtu huyu atafanya matendo yanayotoa maana ya maisha yake. Kwa ujumla udhanaishi hujikita zaidi na dhana ya maisha.

Mwanzilishi wa dhana hii kwa mujibu wa <https://www.facebook.com/permalink.php> yaliyowasilishwa na wanakikundi wanaojiita Undertree Group cha SAUT Malimbe Mwanza mwaka 2013, “Udhanaishi unahusishwa kwa kiasi kikubwa na mwana theolojia Ki-Den Soren Kier Kegaard, mwanafalsafa wa Kijerumani Friedrich Nietzsche. Na muasisi mkuu wa dhana hii ni Jean Paul Sartre. Na kwa upande wa fasihi ya Kiswahili, gwiji wa dhana hii ni E. Kezilahabi kutokana na uandishi wake umejikita zaidi katika dhana hii.

Kutokana na kuwa nadharia hii ya Udhanaishi inajikita zaidi katika kueleza matatizo yanayomkuta binadamu, kwani nadharia hii inakwepa imani ya kinjozi juu ya imani ya kuishi. Pia nadharia hii haiamini uwepo wa Mungu na Uumbaji wake wa Ulimwengu. Vile vile nadharia huonesha juhudi za mtu binafsi za kujipatia uhuru wake, uwezo wake wa kujiamini katika kupambana na maisha ingawa mwishowe huishia katika mauti au katika majanga makubwa. Hivyo basi mwandishi wa riwaya ya *Kichwamaji* (E. Kezilahabi) ametumia dhana hii ya udhanaishi katika riwaya zake, naye mwandishi wa riwaya ya *Vuta n’kuvute* (Shafi A. Shafi) yeye si mdhanaishi lakini hata hivyo katika riwaya yake alionesha kwa kiasi fulani juu ya suala la maisha na tabu katika maisha kwa kumbebesha dhima hizi muhusika wake Yasmin. Na jambo hili lilitoa msaada mkubwa kwa mtafiti kutumia nadharia hii kwa

kuwa imetumika kwa mwandishi Kezilahabi na vile vile baadhi ya matendo ya wahusika yaliyobeba dhamira za kidhanaishi kuonekana kwa mwandishi A. Shafi.

2.7 Umuhimu wa Nadharia Hizi katika Utafiti

Nadharia kama ni yenzo moja wapo ya kufanikisha kazi za utafiti zina umuhimu mkubwa katika kuongoza uandishi wa tasnifu hii.

Kwanza; katika kuichambua kazi ya fasihi kifani kunapelekea kuibuliwa vipengele mbalimbali vya fani. Nadharia ya simiotiki iliyotumika kwa kuangalia maneno ya kiashiria na kiashiriwa pamoja na maana inayojitokeza ndipo pakaibuliwa tamathali za semi mbalimbali.

Pili; mtegemeano uliopo wa fani na maudhui katika kazi yoyote ya fasihi hupelekea kuibuliwa kwa dhamira, nadharia ya udhanaishi imelifanikisha jambo hilo kwa kuweza kutoa dhamira mbalimbali. Kiujumla maswali ya utafiti yameweza kupata majibu kutokana na nadharia hizi.

2.8 Ombo la Kitaaluma

2.8.1 Mapungufu

Utafiti huu umeonesha mapungufu ya wataalamu juu ya yale waliyoyasema kuhusiana na mada hii kwani watafiti wengi wa hapo juu hawakujishughulisha na utafiti linganishi. Na kwa wale waliozungumzia utafiti linganishi tuliona hawakugusia katika vitabu teule, na hili limejulikana na mtafiti kwa kutembelea Maktaba mbalimbali za Tanzania, lakini mtafiti hakukuta katika Maktaba hizo rejea za kutosha zinazohusiana na vitabu teule juu ya ulinganishi wa tamathali za semi. Mohochi (2000) amesema tahakiki na tafiti nyingi zimeegemea zaidi katika taaluma

ya fasihi ya Kiswahili na kuegemea zaidi katika vipengele vya maudhui kuliko vipengele vya fani. Kwa hiyo mtafiti aliamua kuchukua fursa hiyo ili kuziba pengo hili kwa kufanya utafiti linganishi kati ya riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute* kwa upande wa fani kwenye matumizi ya lugha katika kipengele cha tamathali za semi.

2.8.2 Makusudio

Mtafiti amekusudia kuonesha katika utafiti huu, matumizi ya lugha kama kipengele muhimu katika kazi ya fasihi andishi. Pia alionyesha namna kipengele cha tamathali za semi kilivyotumika katika riwaya mbili teule na kwa kiasi gani matumizi hayo ya tamathali za semi yanafanana katika riwaya hizo na kwa kiasi gani yametofautiana kupitia vitabu viwili vya riwaya tuele.

2.9 Hitimisho

Katika sura hii ya pili mtafiti alichambua kwa kina yale yaliyoandikwa na watafiti na wahakiki wa kazi za fasihi tangulizi yanayohusiana na mada ya utafiti. Ambapo waandishi tangulizi wamegusia vitabu teule kwa upande wa tahakiki na utafiti wa vipengele vya maudhui na kwa kiasi kidogo kwenye upande wa fani kwa ujumla, bila ya kufanya ulinganishi wa vipengele hivyo hasa kipengele cha lugha kwenye matumizi ya tamathali za semi. Na mwisho wa sura hii ufafanuzi wa mkabala wa nadharia zilizotumika katika utafiti huu ulijadiliwa na kuonesha ni kwa kiasi gani ulivyoweza kufanikisha lengo la utafiti huu. Sura inayofuata itaonesha mbinu za utafiti zilizotumika.

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea mbinu alizozitumia mtafiti katika ukusanyaji wa data. Hapa mtafiti anaelezea mpango wa utafiti huu wa kukusanya data na muda aliyotumia, walengwa wa utafiti, mawanda ya utafiti, zana za utafiti, mbinu ya kimaktaba ya ukusanyaji wa data pamoja na udhibiti wa data.

3.2 Mbinu za Utafiti

Utafiti huu umetumia mbinu ya kimaktaba kama ilivyopendekezwa na Kiango na Mdee (1995:14-22) kwa utafiti wa kuchambua / kuhakiki kamusi au vitabu vya fasihi katika vipengele vya fani. Mbinu hii ya kimaktaba imetumika kwa kuonesha matumizi ya lugha yaliyotumiwa na waandishi hawa wawili pamoja na kulinganisha na kutofautisha matumizi hayo, mtafiti alivisoma vitabu teule kwa undani kabisa kisha aliorodhesha tamathali za semi zilizojitokeza kwa waandishi wote wawili na mwisho alifafanua dhamira zilizojitokeza kutoka katika hizo tamathali za semi.

3.3 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu umekusanya data kwa kutumia mbinu ya kimaktaba kwa kuvitalii vitabu teule. Na shughuli hii ya kukusanya data imetumia muda wa miezi mitatu hadi kukamilika kwake, na kazi ya kuchambua data imetumia miezi miwili, kwa ujumla shughuli ya kukusanya data na kuzichambua imechukua muda wa miezi mitano. Na njia iliyotumika katika kukusanya data ni ile ya kimaktaba ya kuvidurusu vitabu teule na kukusanya katika jedwali kila tamathali ya semi iliyojitokeza. Na uchambuzi

wa data umeoneshwa kwa njia ya mdafoa, kwa kuziweka pamoja tamathali za semi za aina moja na kuonesha idadi ya tamathali za semi zilizotumika kwa kila mwandishi na kubaini tamathali za semi zilizofanana na zilizotofautiana kwa waandishi wote wawili. Mwishowe kuonesha kwa njia ya maelezo namna matumizi ya tamathali za semi yalivyotumika na kubainisha dhamira zilizojitokeza.

3.4 Walengwa wa Utafiti

Utafiti huu umewalenga baadhi ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili wa jinsia zote wakike na kiume ambao ni wadau wa fasihi linganishi na wanafunzi wa vyuo vikuu wa nagazi mbalimbali. Na pia hata watumiaji wengine wa kawaida wa lugha ya Kiswahili nchini Tanzania na duniani kwa ujumla.

3.5 Uteuzi wa Sampuli

Usampulishaji ni mchakato wa kuteua washiriki miongoni mwa kundi kubwa la watafitiwa kwa madhumuni ya kupata kikundi kidogo kitakachoshiriki katika kutoa data. Kwa mujibu wa Thungu na wenzake (2010:279), Usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka kundi kubwa (populesheni) ambao ndio watakaotoa data kwa kuwakilisha kundi kubwa.

Katika kutayarisha sampuli katika utafiti, wako baadhi ya wataalamu wameonesha njia bora za kupata sampuli kwa kuyagawa makundi kulingana na wingi wa washiriki, na pia kuangalia usawa wa jinsia na hata umri. Miongoni mwa hao ni Uwe (2007:48), ameanesha namna ya kuwagawa watafitiwa kulingana na umri na jinsia. Lakini hata hivyo utafiti huu haukuzingatia ugawaji wa jinsia ya kike na kiume wala

kuzingatia umri. Kwani huu umekuwa ni utafiti wa kimaktaba, kama ilivyopendekezwa na Kiango na Mdee (wameshatajwa).

3.5.1 Mbinu za Uteuzi wa Sampuli

Kwa mujibu wa Rwegoshora (2006), amesema mbinu za uteuzi wa sampuli zinaweza kuwekwa katika makundi mawili (2), mbinu za sampuli nasibu na mbinu za sampuli zisizo nasibu. Mbinu za sampuli nasibu zinajumuisha mbinu kama vile usampulishaji kutegemea fursa, usampulishaji wa kujitolea, usampulishaji tabakishi, usampulishaji ongezi na usampulishaji kwa madhumuni maalumu. Utafiti huu umetumia mbinu ya usampulishaji kwa madhumini maalumu. Hii ni mbinu ya kuteua sampuli kutokana na sifa stahiki zinazoendana na mada ya utafiti, wakati mwingine usampulishaji huu tunaita usampulishaji wa kutumia sampuli lengwa.

Hivyo utafiti huu umetumia aina ya sampuli lengwa katika kukusanya data za utafiti. Sampuli lengwa ni aina ya sampuli ambayo humwezesha mtafiti kuteuwa watafitiwa wake huku akiwa na imani kwamba watafitiwa hao ndio watakaoweza kumpatia data anazozihitaji ili kujibu maswali ya utafiti wake. Yaani watafitiwa wa utafiti huu ni hivi vitabu teule na data zilikusanywa kutoka moja kwa moja katika vitabu teule vya riwaya za Kezilahabi, *Kichwamaji* (1974) na Shafi A. Shafi, *Vuta n'kuvute* (1999).

3.6 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu ni utafiti linganishi, uliojishughulisha na fasihi andishi kwa upande wa fani katika kipengele cha matumizi ya lugha, kwa kuchunguza kufanana na kutofautiana kwa waandishi teule juu ya kipengele cha tamathali za semi katika riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*.

3.7 Zana / Vifaa vya Utafiti

Kwa mujibu wa Creswell (2009), ameeleza kwamba zana / vifaa vya utafiti ni sehemu iliyo muhimu sana katika ukusanyaji wa data. Mtafiti ametumia zana tofauti katika kukamilisha utafiti wake ikiwa ni pamoja na karatasi, kalamu, ngamizi (kompyuta), na vitabu teule vya utafiti huu.

3.7.1 Ngamizi / Kompyuta

Ngamizi/ Kompyuta ni mashine ya kielektroniki inayotumika kuhifadhi na kusarifu taarifa zinazolingizwa ndani yake. (BAKIZA, 2010). Katika utafiti huu kifaa hiki kilitumika tokea wakati wa kuandaa pendekezo la utafiti hadi uandishi wa ripoti ya utafiti. Kwa hivyo chombo hiki / kifaa hiki kilimsaidia mtafiti katika kukusanyia data za utafiti, kuandika tasnifu na kuweza kukitumia kama chombo cha kuwekea kumbukumbu kwa muda mrefu bila ya kupotea.

3.7.2 Kalamu na Karatasi

Matumizi ya kalamu na karatasi katika kazi ya utafiti ni vifaa bora kabisa, kwani ni vifaa vya jadi vya utafiti, na hapana shaka vitaendelea kutumika kwa muda wa miaka mingi ijayo kwa vile ni vifaa vilivyo rahisi kupatikana na ni vyepesi kutumika na vile vile ni vyepesi kubebeka na wala havihitaji utaalamu wa kipekee kuvitumia. Hivyo mtafiti alitumia kalamu na karatasi kwa kuandikia kumbukumbu mbalimbali alizopata kutoka maktabani na vile vile wakati wa kukusanya data na kuchambua data alivitumia vifaa hivi. Kwani kalamu na karatasi ilikuwa ndio vifaa vya mwanzo kutumika katika utafiti huu.

3.8 Ukusanyaji wa Data

Katika shughuli ya utafiti, ukusanyaji data ni hatua muhimu ya kuweza kukamilisha utafiti, au tunaweza kusema ukusanyaji wa data ndio roho ya utafiti wowote ule. Hivyo mtafiti yeyote anatakiwa awe mweledi katika hatua hii kwa kuchagua mbinu muafaka inayoendana na kazi yake. Naye Kothari (2002:117), ameanesha ukusanyaji wa data uko wa namna mbili: data za msingi na data za upili.

3.8.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile data mpya zinazokusanywa na mtafiti wa mada husika ambazo hazijawahi kukusanywa na mtafiti mwingine kabla yake. Kwa kawaida watafiti wa mwanzo wa utafiti husika huacha pengo ambalo mtafiti mwingine huja kuliziba, na mara nyingi mtafiti wa kwanza hutumia data za msingi kwani yeye huwa wa kwanza kuzikusanya data ambazo hazijakusanywa na mtafiti yeyote kabla yake. Utafiti huu kwa kiasi fulani umetumia data za msingi ili kuweza kujibu maswali ya utafiti na kutokana na kuwa utafiti huu ni wa kimaktaba.

3.8.2 Data za Upili

Data za upili ni zile data ambazo zimewahi kukusanywa na watafiti tangulizi wa utafiti husika. Data hizi za upili hupatikana ama hujulikana na mtafiti kwa kutalii tasnifu mbalimbali, tahakiki, makala na hata katika tovuti na hapo mtafiti hubaini pengo lililoachwa na watafiti tangulizi. Utafiti huu pia umekusanya data kwa njia ya mlinganisho wa data ambazo tayari zimekwishawahi kukusanywa na zile alizozikusanya mtafiti. Hii ni kwa kuvipitia vitabu teule na tasnifu zake ambazo mtafiti amezikuta maktaba na kisha kujibu maswali ya utafiti huu.

Hata hivyo Kothari (ameshatajwa) akaendelea kueleza kuwa ziko mbinu nyingine nyingi za kukusanya data. Na pia Wamitila (2003:179) amezitaja kuwa ni pamoja na uchunzaji, hojaji, dadisi, pamoja na kushiriki katika utendaji na kadhalika. Lakini mtafiti katika kulikamilisha hili ametumia mbinu ifuatayo:-

3.8.3 Mbinu ya Kimaktaba

Mbinu hii ya kimaktaba inahusisha jinsi ya kutafuta data kwa njia ya kuvisoma vitabu mbalimbali kama vile vitabu teule, majarida, barua, nyaraka, taarifa mbalimbali zilizomo katika mtandao na wavuti, vitabu vya ziada na vitabu vya kiada pamoja na tahakiki na tasnifu za watafiti mbalimbali kutokana na mahitaji ya utafiti husika. Katika kipindi cha kukusanya data. Mtafiti ametumia mbinu ya kimaktaba ya kuvisoma vitabu teule, kama ilivyopendekezwa na Kiango na Mdee (1995:14-22) kulingana na aina ya utafiti huu, kwani utafiti huu umejikusisha na vipengele vya fani kwenye upande wa matumizi ya lugha katika kipengele cha tamathali za semi kama zilivyotumiwa na waandishi wa vitabu teule.

Kiango na Mdee (wameshatajwa) wamesema mhakiki au / na mtafiti katika kazi ya kuchambua vipengele vya fani, njia iliyokuwa bora ni ile ya utafiti / uhakiki wa kimaktaba. Kwa kupitia mbinu hii ambayo ilimwezesha mtafiti kupata data za upili maktabani kwani maktabani ni chanzo kizuri cha utafiti wa maelezo, mtafiti aliweza kuchunguza tamathali za semi mbalimbali zilizotumiwa na waandishi wa vitabu teule. Vile vile mbinu hii ilimwezesha kuibua dhamira mbalimbali kutokana na tamathali za semi alizozikusanya kwa kuangalia matendo ya wahusika jinsi yalivyohusiana na tamathali za semi husika. Hivyo basi mtafiti alivisoma vitabu teule moja kwa moja na kuanza kuorodhesha yale aliyoyapata katika matumizi ya

tamathali za semi yaliyotumika katika vitabu hivyo. Na njia hii ilimsaidia mtafiti wakati wa kuchambua data kwani ilikuwa kwake ni rahisi kutenganisha tamathali za semi zilizofanana na zile zilizotofautiana.

3.9 Uchambuzi wa Data

Kazi ya uchambuzi wa data ilikuwa ni nyepesi kwa mtafiti, kwani data za utafiti huu zilichambuliwa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa data ya kimaudhui. Uchambuzi huu ni ule uchambuzi wa kifasihi ambao hutoa fursa kwa mtafiti kusoma, kutazama au hata kusikiliza jambo linalohusu kazi za fasihi kisha mtafiti hutoa maelezo juu ya dhamira alizozipata pamoja na vipengele vyengine vya kisanaa. Katika utafiti huu mtafiti alitumia mbinu hii kwa kuanza kukusanya tamathali za semi na kisha kupitia matendo ya wahusika, mtafiti aliibua dhamira kwa mujibu wa malengo na maswali ya utafiti. Mtafiti alihakikisha kuwa shughuli ya kukusanya data ilikamilika kwa muda muafaka na kwa ufanisi mkubwa. Na kwa kufanya hivyo kulimfanya mtafiti afanye kazi ya uchambuzi wa data kwa urahisi, kwani alitumia njia ya mdafao kwa kuweka pamoja yale matumizi ya tamathali za semi yanayofanana na kuonesha kwa njia hio hio matumizi ya tamathali za semi yanayotofautiana kwa maandishi wote wawili. Pia alitolea maelezo na mifano kwa kuonesha dhamira za matumizi ya tamathali za semi zilizotumika na maandishi wote wawili.

3.10 Udhibiti wa Data

Mtafiti alihakikisha kuwa data alizozikusanya zilikuwa ni za ukweli na za kuaminika. Kwa kulifikia hili mtafiti amehakikisha kuwa kwanza amevisoma vitabu teule na kuvielewa, kisha ametalii / amesoma vitabu vya nadharia ya fasihi kwa

ujumla vilivyoandikwa na wataalamu mbalimbali vinavyohusu matumizi ya lugha katika kazi za fasihi. Baadae amehakikisha kila kipengele cha tamathali za semi kilichotumika na waandishi hawa amekidhibiti kwa kukiandika na kuweka katika orodha maalumu ya majedwali pamoja na kuonesha dhamira zilizojitokeza katika kila tamathali ya semi.

3.11 Hitimisho

Sura hii ya tatu ilieleza mbinu zilizotumika katika kukusanyia data tokea mwanzo kabisa wa utafutaji wa data hadi mwisho wake wa kuziandika hadi kuzidhibiti. Katika sura hii mtafiti ameeleza mbinu za maktaba alizozitumia, mpango wa utafiti, walengwa wa utafiti, usampulishaji, mawanda ya utafiti, zana / vifaa vya utafiti, ukusanyaji wa data kama vile data za msingi na data za upili, mbinu ya kimaktaba pamoja na sababu za kutumia mbinu hiyo badala ya mbinu ya uwandani, uchambuzi wa data na udhibiti wa data.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Katika sura hii mtafiti aliwasilisha data alizozipata katika utafiti wake kuhusu matumizi ya tamathali ya semi na kuweza kufanikiwa kukusanya aina kumi na moja (11) za tamathali za semi zilizotumiwa na waandishi teule kisha kuziorodhesha katika majedwali ishirini na mbili (22). Na mwishowe akazichambua data hizo kwa njia ya maelezo kwa kuonesha dhamira ishirini na mbili (22).

4.2 Usuli wa Watunzi

4.2.1 Kezilahabi ni Nani?

E. Kezilahabi ni mwandishi mashuhuri katika fani ya uandishi wa fasihi ya Kiswahili katika utanzu wa riwaya, tamthilia, ushairi na hata hadithi fupi. Mwandishi amezawa tarehe 13 Aprili 1944, katika kijiji cha Namagondo kilichopo kisiwani Ukerewe katika Ziwa Victoria. Katika mwaka 1967 alijiunga na kupata shahada yake ya kwanza katika Chuo Kikuu cha Afrika ya Mashariki cha Dar-es-Salam. Katika mwaka 1985 alijipatia shahada yake ya uzamivu (Ph.D) katika chuo Kikuu cha Wisconsin Madison kilichoko Marekani. Katika mwaka 1987 alipanda ngazi kutoka Mkufunzi msaidizi na kuwa Profesa Mshiriki. Katika mwaka 1994 alichaguliwa katika ngazi ya kimataifa kuwa mmoja wa majaji wa kuamua nani apewe zawadi ya uandishi ya Jumuiya ya Madola. Na kwa sasa ni Profesa Mshiriki katika Chuo Kikuu cha Botswana kwenye idara ya Lugha za Kiafrika. Riwaya alizoandika: *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), *Gamba la Nyoka*

(1979), *Nagona* (1990), *Mzingile* (1991). Pamoja na riwaya hizo pia ameandika Hadithi Fupi, Tamthilia na Mashairi. Na kazi zake nyingi zimetafsiriwa kwa lugha mbalimbali za kimataifa; kama vile Kijapani, Kiingereza na Kijerumani.

4.2.2 Shafi A. Shafi ni Nani?

Shafi A. Shafi ni mwandishi wa riwaya ya *Vuta n'kuvute*. Aliezawa mwaka 1940 na kupata elimu yake Zanzibar na kujiunga na Chuo cha Ualimu cha Nkrumah katika mwaka 1957 hadi 1960. Kwa wakati huo Chuo kilikuwa kikiitwa Chuo cha Ualimu cha Sayyid Khalifa. Katika mwaka 1963 alipata Diploma ya juu katika fani ya siasa ya uchumi katika chuo cha Fritz Heckert kilichopo katika nchi iliyokuwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Ujerumani. Aliendelea na kujielimisha tokea 1964 hadi mwaka 1965 katika fani ya Uandishi wa Habari mjini Prague, nchini Czechoslovakia ambapo kwa sasa inaitwa Jamhuri ya Czech. Pia alienda nchini Sweden 1982 na nchini Marekani mwaka 1983 kote huko kwa ajili ya kujiengezea taaluma. Riwaya alizoandika: *Kasri ya Mwinyi Fuadi* (1978), *Kuli* (1979), *Vuta n'kuvute* (1999), *Haini* (2003) na *Mbali na Nyumbani* (2012). Pamoja na riwaya zake hizo pia ameweza kushirikiana na Mdee na wenzake (2011) katika kuandika Kamusi.

4.3 Tamathali ya Semi

Moja kati ya malengo mahsusi ya utafiti huu lilikuwa ni kubaini mfanano wa matumizi ya tamathali za semi katika riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*. Katika kufikia lengo hili, utafiti huu ulitumia mbinu ya mapitio ya maandiko kwa kusoma, kuchunguza na kuchambua riwaya hizo teule ili kubainisha mfanano wa matumizi ya tamathali za semi kwa waandishi wote wawili. Hivyo basi, kwa kutumia mbinu hiyo, utafiti huu uliweza kubainisha mfanano huo wa tamathali za semi na

kubaini kutokuwepo kwa tofauti ya matumizi ya tamathali ya semi. Kwa mujibu wa Senkoro (1984), “Tamathali za semi ni maneno, nahau au sentensi ambazo hutumiwa na wasanii ili kutia nguvu katika maana, mitindo na hata sauti katika maandishi ama kusema. Wakati mwingine hutumiwa kama njia ya kuipamba kazi ya fasihi na kuongeza utamu wa lugha”. Katika kujibu swali namba moja na namba mbili la utafiti huu, mtafiti ameweza kukusanya data zinazohusu tamathali za semi zilizotumika katika vitabu teule na kuonesha mfanano wao katika tamathali za semi kwa kuziorodhesha katika majedwali maalumu kwa kila moja. Kwa kutumia mbinu ya mapitio ya kutalii machapishi na huku ikisaidiwa na nadharia ya simiotiki, utafiti ulibainisha tamathali za semi zilizotumika kwa waandishi wawili kama jedwali lifuatalo:

Jedwali 4.3: Tamathali za semi zilizotumika katika riwaya za *Kichwamaji na*

Vuta n’kuvute

Aina ya Tamathali ya Semi	<i>Kichwamaji</i>	<i>Vuta n’kuvute</i>
Tashibiha	20	51
Tashihisi	26	44
Sitiari	12	5
Mubalagha	9	33
Tafsida	10	6
Tauria	8	10
Shitizai	9	9
Dhahaka	3	2
Takriri	12	31
Tabaini	5	31
Msisitizo Bayani	2	1

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya za *Kichwamaji na Vuta n’kuvute* (2016)

Jedwali Na. 4.3.2.2.3 limeonesha orodha ya matumizi ya tamathali za semi zilizotumiwa na waandishi wawili na kubainisha utumizi wao juu ya tamathali za semi. Kwa hiyo swali namba moja na namba mbili limeweza kupata majibu. Sehemu ifuatayo inajadili tamathali za semi hizo kwa kuonesha kila moja jinsi ilivyotumika kwa mwandishi mmoja mmoja na kuziorodhesha baadhi na nyingine kuzionesha kwenye kiambatishi namba moja na namba mbili.

4.3.1 Tamathali ya Semi ya Tashibiha

Kwa mujibu wa Mulokozi na Kahigi (1979). Tashibiha au mshabaha ni aina ya tamathali ya semi inayotumika katika mlinganisho wa mambo au vitu kwa kutumia viunganishi kama vile “kama”, “mfano wa”, “mithili ya”, “sawa na” na kadhalika. Tamathali hii hutumia vitu vitatu navyo ni kizungumzwa, kifananishi na kiungo. Kwa kutumia nadharia ya simiotiki mtafiti ameweza kubaini tamathali za semi za tashibiha zilizotumiwa na waandishi wote wawili na kubainika kufanana katika kutumia tamathali hii ya semi na kuorodhesha katika majedwali yafuatayo:

Jedwali Na. 4.3.1.1 linaonesha tamathali ya semi ya tashibiha zilizotumika katika riwaya ya *Kichwamaji*

Na.	Uk.	Mfano wa Tashibiha
1	1.	Wazee kwa vijana, wake kwa wanaume. Wote kama wagonjwa wangojeao kumuona daktari.
2	2	Watu tulikua tumekaa nje tuliweza kusikia sauti yake ikinguruma kama simba.
3	3	Mgongo wa mzee huyo sasa ulikuwa kama ukurasa ambao haukuandikwa maneno.
4	23	Walikuja mbio kama kwamba atakayekuwa wa kwanza kufika atapata zawadi

5	24	Kila mtu alikuwa akitembea polepole kama mgonjwa.
6	29	Hofu kubwa ilinipata kama kwamba simba wa Tsavo walikua mbele yangu.
7	31	Mchanga huu ulikuwa ukimwagika kama mvua kupitia dirishani.
8	33	Mahali pale palikuwa wazi kama uwanja wa mpira
9	45	Waliponiona walishituka kama kwamba waliona mzuka
10	59	Pembeni niliona suruali yangu imewekwa juu ya kiti kama kikombe cha mashindano.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Kichwamaji* (2016)

Jedwali Na. 4.3.2.2 linaonesha tamathali ya semi ya tashibiha zilizotumika katika riwaya ya Vuta n’kuvute.

Na	Uk	Mfano wa Tashibiha
1	1	Yasmin alikuwa na kijiso kidogo cha mdawari mfano wa tungule na macho makubwa ambayo kila wakati yalionekana kama yanalengwa lengwa na machozi.
2	8	Alifungua mlango taratibu, alipoingia ukumbini alimkuta Bwana Raza amekaa juu ya kiti amevimba kama kiboko.
3	11	Mikono huinyanyua na kuishusha, akijibenua na kujinyonganyonga mithili ya mkunga aogelevyo kupitia mapangoni.
4	11	Walitazamana lakini Yasmin hakuweza kuvumilia mtazamo wa kijana yule aliyekuwa na macho makali kama kurunzi.
5	13	Jumamosi ikapeperuka kama kishada kilichokatika arijojo....
6	14	Bwana Raza akaona sasa maji yamezidi unga, hajui la kulifanya, Yasmin amechachamaa, amekuja juu kama moto wa kifuu...
7	14	Unani... hajawahi kumaliza akachapwa kofi la pili. Yasmin alianguka juu ya kochi kama mzigo anatweta kama mgonjwa wa pumu.
8	15	Wachukuzi namba walimzonga kama nzi wanapouzongea mzoga, kila mmoja katika wachukuzi wale akitaka kujua mizigo ya Yasmin...
9	16	Majirani walikwishajaa madirishani wanamwangalia Yasmin akitoka na kikapu chake mkononi, amenywea kama aliyemwagiwa maji ya baridi.
10	20	Alisema Yasmin akitabasamu na kuonesha meno yake yaliyokuwa yaking’aa kama marmar.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Vuta n’kuvute* (2016)

Jedwali Na. 4.3.1.1 na 4.3.1.2 yameonesha baadhi ya orodha ya matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha zilizotumiwa na waandishi wawili na kubainisha kufanana kwao kwa utumizi wa tashibiha na vile vile kukosekana tofauti ya utumizi wa tamathali za semi hiyo. Kwa hiyo swali namba moja na namba mbili limeweza kupata majibu.

4.3.2 Tamathali ya Semi ya Tashihisi

Kwa mujibu wa Msokile (1992). Tamathali ya semi ya tashihisi ni aina ya tamathali ya semi yenye kutumika katika kunafsisha vitu, yaani kufanya vitu viwe na maumbile na kusema au kutenda kama mtu. Wakati mwingine tamathali hii huitwa uhaishaji. Tamathali ya semi hii hutumika kwa kuipa kitu sifa au tabia ya kibinadamu kitu kisicho na sifa wala uweza huo. Kwa kutumia nadharia ya simiotiki mtafiti ameweza kubaini tamathali za semi za tashihisi zilizotumiwa na waandishi wote wawili na kubainika kufanana katika kutumia tamathali hii ya semi na kuorodhesha katika majedwali yafuatayo:

Jedwali Na. 4.3.2.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Tashihisi Zilizotumika

Katika Riwaya ya *Kichwamaji*

Na	Uk.	Mfano wa Tashihisi
1	1	Niligundua kwamba kwa muda wa nusu saa tulikuwa hatuendi: mstari ulikuwa umesimama.
2	4	Nilikasirika kidogo, lakini hasira yangu niliimeza kwa kuuma meno.
3	7	Sababu yenyewe ilikuwa kwamba mwalimu alimwekea zero kubwa yenye macho mawili na meno yakimcheka.
4	10	Alifanya kosa ambalo nilikuwa siwezi kumsamehe. Kisasi kilianza kunikera moyo wangu.

5	13	Nilikata shauri kwenda kuutazama ili kutuliza kichwa changu kidogo chenye kiburi.
6	18	Mwaka wa kwanza nafikiri ulipita salama. Mambo yalianza mwaka wa pili alipokuwa darasa la kumi..
7	29	Giza lilikuwa limeshaingia. Aliniacha mimi na mawazo mengi.
8	30	Niliona kwamba watu wote wa nyumbani kwetu walikuwa wanekwisha nyang'anywa utu wao, hapakuwa na mtu tena pale nyumbani.
9	37	Huu ni ugonjwa unaoletwa na vijana na utatumaliza sisi kina mama wenye mabinti.
10	39	...halafu wakitoka nje usiku huvaa nguo ambazo huwa zimetunzwa nje majanini ili kupoteza harufu kwa umande

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Kichwamaji* (2016)

Jedwali Na. 4.3.2.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Tashihisi Zilizotumika

Katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute*

Na	Uk	Mfano wa Tashihisi
1	5	Yasmin aliyapuuza yote yale akageuza ubavu wa pili, mara usingizi ukamchukua.
2	5	Yasmin alipigwa na mshangao hakujua yameanzaje hata yakaja ya kuhama Unguja.
3	10	Nyumba za mtaa ule zilikuwa za kizamani zilizoshikana moja baada ya nyingine.
4	11	Baada ya kunywa chai alijihisi nyumba imemuelemea amezungukwa tena na upweke, akaanza kuufukuza upweke ule kwa kusikiliza muziki.
5	18	Kwa Yasmin kimya kile kilikuwa cha sauti tu, kwani kichwani mwake mlikuwa mmejaa mawazo yaliyokuwa yakisokotana na kumfanyia kelele ambazo mtu yoyote hakuweza kuzisikia ila yeye mwenyewe.
6	25	Baada ya kiasi cha mikupuo mitatu, Salum alitulia na sigara yake mkononi akisikiliza pombe inamwambia nini kichwani mwake.
7	35	Macho yote yameingia ndani, amefuga sharafa la ndevu nazo zimechanganyika nyeusi na nyeupe hujui zipi zinataka kumtawala mwenzake.
8	36	Hakupata kusafiri na husikia tu kwa wale wanaotweka mitepe yao, wakupambana na dharuba za kusi na kaskazi, bahari inapotafirika.
9	44	Nuru ya jua iliingia kwa hamaki chumbani mle na ikakashifu uchafu wote wa chumba kile.
10	55	Lakini mara tu baada ya sauti za ala za tarabu kuwasili ndani ya masikio yao.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute* (2016)

Jedwali Na. 4.3.2.1 na 4.3.2.2 yameonesha baadhi ya orodha ya matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi zilizotumiwa na waandishi wawili na kubainisha kufanana kwao kwa utumizi wa tashihisi na vile vile kukosekana tofauti ya utumizi wa tamathali za semi hiyo. Kwa hiyo swali namba moja na namba mbili limeweza kupata majibu.

4.3.3 Tamathali ya Semi ya Sitiari

Tamathali ya semi ya sitiari ni aina ya tamathali inayotumika katika kuhusisha matendo, kitu au tabia ya vitu vyenye maumbile tofauti (huleta uhamisho wa kimaana). Vilevile Mulokozi na Kahigi (1979) wamefasiri maana ya sitiari kuwa ni uhamishaji wa maana na hisi kutoka katika kitu au dhana nyingine, vitu hivyo vinavyohusishwa kwa kawaida huwa havina uhusiano wa moja kwa moja.

Wakati mwingine sitiari haitumii kiunganishi katika kuhusisha matendo tofauti. Hivyo tunaweza kusema sitiari ni tamathali ya semi inayotumika kulinganisha vitu viwili vyenye sifa tofauti bila ya kutumia kiunganishi. Kwa kutumia nadharia ya simiotiki mtafiti ameweza kubaini tamathali za semi za sitiari zilizotumiwa na waandishi wote wawili na kubainika kufanana katika kutumia tamathali hii ya semi na kuorodhesha katika majedwali yafuatayo:

Jedwali Na. 4.3.3.1 na 4.3.3.2 yameonesha baadhi ya orodha ya matumizi ya tamathali ya semi ya sitiari zilizotumiwa na waandishi wawili na kubainisha kufanana kwao kwa utumizi wa sitiari na vile vile kukosekana tofauti ya utumizi wa tamathali za semi hiyo. Kwa hiyo swali namba moja na namba mbili limeweza kupata majibu.

Jedwali Na. 4.3.3.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Sitiari Zilizotumika**Katika Riwaya ya *Kichwamaji***

Na	Uk	Mfano wa Sitiari
1	10	Mwafrika akawa Mwafrika; Mzungu akawa Mzungu; Mhindi akawa Mhindi; na Mwarabu akawa Mwarabu.
2	17	Rukia ni Malaya.
3	25	Sisi jembe letu ni kalamu.
4	37	Huu ni ugonjwa unaoletwa na vijana.
5	43	Niliona kwamba elimu ilikuwa sumu ya furaha kwangu.
6	44	Nilikuwa maiti, na ninafikiri kwamba sasa ungekuwa unalia...
7	45	Nilijiona maiti tena.
8	54	Huyu sasa amekuwa mpira, wa kudunda na kuacha hapo, wengine pia wadunde.
9	93	Siku ya visa ni visa.
10	127	Hata! Mke wa mwizi ni mwizi, mke wa mlevi ni mlevi. Manase alisema.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Kichwamaji* (2016)

Jedwali Na. 4.3.3.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Sitiari Zilizotumika**Katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute***

Na	Uk	Mfano wa Sitiari
1	39	Amekuwa mfa maji kamili.
2	96	Basi kila siku aje kwetu tu, kwani nyumba yetu msikiti?
3	175	Sasa amenasa ni mahabusu wake, si huru tena wa kwenda apendako.
4	217	Yule askari aliyekuja kumfungulia alimwona ni mkombozi aliyemkomboa kutoka jahanamu.
5	243	Denge amekonda ni mifupa mitupu.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute* (2016)

4.3.4 Tamathali ya Semi ya Mubalagha

Tamathali ya semi ya mubalagha ni aina ya tamathali ya semi inayotumika katika kutia chumvi katika maelezo yanayofanywa katika kazi za sanaa. Tamathali hii hutia chumvi kuhusu uwezo wa viumbe, tabia zao na kuhusu sifa zao kwa madhumuni ya kuchekesha au kusisitiza jambo (Senkoro 2011:12). Vilevile Mulokozi na Kahigi (1979) wameonesha dhima ya mubalagha katika kazi za fasihi kuwa ni kuongeza utamu na kuleta athari fulani. Kwa kutumia nadharia ya simiotiki mtafiti ameweza kubaini tamathali za semi za mubalagha zilizotumiwa na waandishi wote wawili na kubainika kufanana katika kutumia tamathali hii ya semi na kuorodhesha katika majedwali yafuatayo:

Jedwali Na. 4.3.4.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Mubalagha Zilizotumika Katika Riwaya ya *Kichwamaji*

Na	Uk	Mfano wa Mubalagha
1	18	Uzuri wake kama nilivyosikia watu wakisema, ulikuwa ni uzuri wa aina ya pekee. Uzuri ambao hata kipofu aliweza kuuona.
2	30	Sikutaka kugeuzwa na hofu kama wao; wao walikwisha kuwa watu ambao hawawezi hata kuguna.
3	46	Bado hajajifungua? Aliuliza Matlida kwa sauti. Bado. Labda atazaa mapacha. Nilimwona majuma mawili yaliyopita. Tumbo lilikuwa kubwa.
4	47	Uzuri wake ulienea Ukerewe nzima.
5	56	Leo sitakunywa pombe. Unafahamu usiku nilipofika kitandani nilikufa.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Kichwamaji* (2016)

**Jedwali Na. 4.3.4.2 Linaonesha Mubalagha Zilizotumika Katika Riwaya ya
*Vuta n'kuvute***

Na	Uk	Mfano wa Mubalagha
1	2	Bwana Raza huvuta biri moja baada ya moja na moshi wa biri hizo huhanikiza harufu yake mbaya nyumba nzima.
2	7	Ah! Babu we, unayajuwa maneno ya mume wangu tena akianza kusema hamalizi.
3	14	Bwana Raza akili hana kichaa hana, midomo inamtetemeka, maneno yamemkwama hayatoki kinywani.
4	21	Salum alimtumbulia macho Yasmin akaanza kumchunguza tokea utosini hadi dole gumba halafu akamuuliza; hujambo dada?
5	23	Alikwenda nazo uani akiwaacha Roger na Yasmin peke yao ndani ya chumba. Walibakia chumbani mle kimya kama mabubu.
6	31	Ama kweli shoga yangu ulikuwa hupo ulimwenguni. Leo mji mweupe, kuna dansa la kukata na shoka Raha leo.
7	33	Mara takrima ya bia ilimfikia Yasmin lakini yeye hakuwa mnywaji wa bia na badala yake alikirimiwa soda na alizinywa mpaka zikamkifu.
8	44	Ilipofika saa tatu, ndani ya uwanja huo ilikua hapana pa kutia mguu. Wachezaji wakuwa wamebanana wakisuguliana majasho.
9	48	Faraji alimdhihaki. Ala! Kula lazima, unajua kuna nchi duniani kama hukula unashitakiwa?
10	59	Mtu wewe! Uko wapi? Hakuna pembe ya mji niliyoibakisha kukutafuta wewe. Mwajuma alilalamika.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute* (2016)

Jedwali Na. 4.3.4.1 na 4.3.4.2 yameonesha baadhi ya orodha ya matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha zilizotumiwa na waandishi wawili na kubainisha kufanana kwao kwa utumizi wa mubalagha na vile vile kukosekana tofauti ya utumizi wa tamathali za semi hiyo. Kwa hiyo swali namba moja na namba mbili limeweza kupata majibu.

4.3.5 Tamathali ya Semi ya Tafsida

Tamathali ya semi ya tafsida ni aina ya tamathali ya semi inayotumika kwa kukisema kitu au inayoamba ili kupunguza ukali wake na kuweka adabu au ficho. Senkero (2011: 18) anasema tafsida ni aina ya tamathali ambayo hujitokeza kwa matumizi ya maneno, misemo au nahau ambayo hupunguza ukali au matusi badala ya kutumia lugha ya uwazi. Kwa kutumia nadharia ya simiotiki mtafiti ameweza kubaini tamathali za semi za tafsida zilizotumiwa na waandishi wote wawili na kubainika kufanana katika kutumia tamathali hii ya semi na kuorodhesha katika majedwali yafuatayo:

Jedwali Na. 4.3.5.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Tafsida Zilizotumika Katika Riwaya ya Kichwamaji

Na	Uk	Mfano wa Tafsida
1	19	Niliona wazi kwamba Manase alikuwa akijaribu kufanya mambo yasiyofaa.
2	20	Alifika hata hatua ya kutumia nguvu! Na kweli alitumia nguvu bila ya utashi wangu.
3	21	Manase anamwita ndugu yangu malaya!
4	57	Huu uovu wa watoto kuanza mchezo mbaya wangali watoto wadogo.
5	80	Nilipomkaribia nilimpa vibao viwili vitatu akaanguka chini.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Kichwamaji* (2016)

Jedwali Na. 4.3.5.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Tafsida Zilizotumika**Katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute***

Na	Uk	Mfano wa Tafsida
1	45	Na siku zote hizi ulikuwa wapi? Tulipotelea Ulaya huko tukipigwa na baridi.
2	49	Ah, juzi juzi nilimkuta mtoto yule kwa Mwajuma, leo yupo na Faraji na Faraji mkocho kwa makoo.
3	118	Ndo maana na sisi tumeazimia kwenda huko kustarehe pamoja nao.
4	124	Wewe nini? Denge aliuliza. Mimi ni mjamzito.
5	145	Waliobahatika walirudi nyumbani na kulala wawili wawili na wasiokuwa na bahati walikwenda kukumbatia mito.
6	199	Hakuelewa safari yake ya kuja Dar es salaam inahusiana nini na kupelekwa ndani ya nyumba kama ile iliyokaa kama gofu lililokumbiwa na wakazi wake kwa kuogopa wafu wanaoranda usiku kucha.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute* (2016)

4.3.6 Tamathali ya Semi ya Tauria

Kwa mujibu wa Msokile (1992). Ameeleza maana ya tamathali ya semi ya tauria kuwa ni aina ya tamathali ya semi inayotumika kwa kutumia maneno ya tahajia moja. Tahajia hizo huwa katika herufi, vina na kadhalika lakini maana ya maneno hayo huwa ni tofauti. Tamathali hii ya semi pia huitwa mchezo wa maneno. Kwa kutumia nadharia ya simiotiki mtafiti ameweza kubaini tamathali za semi za tauria zilizotumiwa na waandishi wote wawili na kubainika kufanana katika kutumia tamathali hii ya semi na kuorodhesha katika majedwali yafuatayo:

Jedwali Na. 4.3.6.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Tauria Zilizotumika**Katika Riwaya ya *Kichwamaji***

Na	Uk	Mfano wa Tauria
1	23	Niliona kwamba sasa wakati wa kusahau vitabu ulikuwa umeingia na kwamba nilikuwa nimeyafika maisha yanayoitwa maisha.
2	56	Kazimoto, jina la bure lakini moto hauwaki. Nitamleta tena leo. Usiniaibishe tena.
3	66	Ukitembea huko nje watu watakuuliza, nyumbani hawajambo? Utajibuje kama hukuwasabahi asubuhi.
4	91	Vua nguo! Baba alisema. Nihurumie sitarudia tena! Kalia alilia.
5	105	Ebu sema tena nikusikie, alisema Tabia, nilimwambia. Tabia, tabia yangu unaiona nzuri; mbona mimi nina kiburi sana.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Kichwamaji* (2016)

Jedwali Na. 4.3.6.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Tauria Zilizotumika**Katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute***

Na	Uk	Mfano wa Tauria
1	6	Alimwomba mumewe amrejeshe nyumbani lakini alikataa kata kata.
2	19	Hivi sasa Yasmin alikabiliwa na maisha mapya kabisa, maisha ambayo hakupata kuishi kwani ijapokuwa alikuwa akiishi Ng'ambu, lakini alikuwa haishi king'ambu.
3	38	Ah, haidhuru nitaishi hivyo yache maji yafuate mkondo na upepo uvume utakapo kwani wangapi wenye dhiki. Mwisho wa dhiki si dhiki ni faraja tu.
4	40	Alipomtazama usoni macho yao yalikutana, ya Yasmin yalikuwa manene yaliyorembuka remburembu naye akatahayari akakabiliana na Denge...
5	44	Alifikiri vipi ataweza kumwingia mtoto yule amwambie maneno aambilike.
6	75	Hakuacha kumweleza jinsi Yasmin alivyopotoka na kumnasihi atafute mwengine miongoni mwa mabanati waliotelewa wakaleleka, waliofunzwa wakafunzika, waliotunzwa wakajitunza.
7	207	Msiwe na wasiwasi Mambo ndiye anayejua mambo hayo, atatueleza.
8	211	Hapo ndipo Bukheti alipomjua Mambo akayajua na mambo yake.
9	215	Bukheti alimwalia Mambo, akamwambia, wewe Mambo hujui mambo wala hujui vyombo. Kwa majahazi yale hakuna lisilowezezana.
10	246	Mambo akaanza mambo yake. Bwan Badi ndo ushakwama Unguja.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute* (2016)

Jedwali Na. 4.3.6.1 na 4.3.6.2 yameonesha baadhi ya orodha ya matumizi ya tamathali ya semi ya tauria zilizotumiwa na waandishi wawili na kubainisha kufanana kwao kwa utumizi wa tauria na vile vile kukosekana tofauti ya utumizi wa tamathali za semi hiyo. Kwa hiyo swali namba moja na namba mbili limeweza kupata majibu.

4.3.7 Tamathali ya Semi ya Shitizai / kejeli

Kwa mujibu wa Msokile (1992). Tamathali ya semi ya shitizai ni aina ya tamathali ya semi inayotumika kwa kukusudia kuleta maana iliyo kinyume na ile iliyokusudiwa ama kinyume na ukweli ulivyo. Kwa kutumia nadharia ya simiotiki mtafiti ameweza kubaini tamathali za semi za shitizai / kejeli zilizotumiwa na waandishi wote wawili na kubainika kufanana katika kutumia tamathali hii ya semi na kuorodhesha katika majedwali yafuatayo:

Jedwali Na. 4.3.7.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Shitizai Zilizotumika Katika Riwaya ya *Kichwamaji*

Na	Uk	Mfano wa Shitizai
1	2	Hata mkoba wenyewe hujui kuushika! Unaupakata kama mtoto!
2	25	Nimekuja kuuliza kama una habari yoyote kuhusu mtoto wetu. Mtoto gani? Huyo mwenda wazimu, alijibu
3	54	Kwa nini hawawezi kumwoza? Hajapata mchumba. Nani ataoa makapi.
4	57	Mimi nimesikia saba na ametiwa mimba hiyo na kijana fulani mchafu mchafu. Sijui wasichana hawana macho?
5	91	Kazimoto, nisaidie kushika kidudu hiki, baba aliniomba.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Kichwamaji* (2016)

Jedwali Na. 4.3.7.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Shitizai Zilizotumika**Katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute***

Na	Uk	Mfano wa Shitizai
1	60	Sikiliza Sista, hawa wakoloni na vijibwa vyao ni mtu ni watu wapumbavu kabisa, kwao kila mtu mkoministi.
2	65	Enhe! Koplo Matata aliwaza na kuguta, yule mtoto wa kihindi, yeye ataweza kunipatia habari za mbwa yule.
3	66	Lakini itayumkinika. Hivyo wanawake wale wasiojua chochote wataweza kunishinda mimi kwa akili?
4	69	Unaonaje basi tukaja wote mimi na wewe tukaja usiku? Lo! Hata ingelikuwa nimekosa mtu wa kufuatana naye.
5	112	Afadhali Yasmin, wao walifikiri labda ni bibiye kama wao, lakini walipomwangalia Mwajuma walimwona kama kisonoko tu kilichotumwa kumsindikiza bibiye mwenzao madukani.
6	149	Lakini kwa takrima ya Shihabu, Mwajuma nae leo kaingia Alakefak. Waliagiza Milk Shake wakala ikawatosha.
7	157	Umekaa kama mtoto wa miaka kumi na mbili.
8	181	Inspekta Wright amesimama mbele ya mlango wa ile nyumba, akamkaribisha kwa kumkejeli. Karibu bwana kubwa.
9	227	Mke ni mwenzako katika safari ya maisha. Raha na furaha, shida na msiba, dhiki na taabu, mke sio unakwenda kulichukua kurumbembe limeota mbawa unaliweka ndani ya nyumba halafu unasema ati una mke.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute* (2016)

Jedwali Na. 4.3.7.1 na 4.3.7.2 yameonesha baadhi ya orodha ya matumizi ya tamathali ya semi ya shitizai zilizotumiwa na waandishi wawili na kubainisha kufanana kwao kwa utumizi wa shitizai na vile vile kukosekana tofauti ya utumizi wa tamathali za semi hiyo. Kwa hiyo swali namba moja na namba mbili limeweza kupata majibu.

4.3.8 Tamathali ya Semi ya Dhihaka

Kwa mujibu wa Msokile (1992). Tamathali ya semi ya dhihaka ni aina ya tamathali ya semi inayotumika kwa kuonesha dharau ya jambo au ina lengo la kumueka mtu katika hali ya duni kupita kiasi, lakini mbinu za kifumbo. Kwa kutumia nadharia ya simiotiki mtafiti ameweza kubaini tamathali za semi za dhihaka zilizotumiwa na waandishi wote wawili na kubainika kufanana katika kutumia tamathali hii ya semi na kuorodhesha katika majedwali yafuatayo:

Jedwali Na. 4.3.8.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Dhihaka Zilizotumika Katika Riwaya ya *Kichwamaji*

Na	Uk	Mfano wa Dhihaka
1	2	Wazee wengine hawana akili hata kidogo! Anaingia humu na fimbo! Anafikiri humu kuna vita.
2	72	Wanaume wawili bado mnatembea na fimbo; woga gani huo!
3	104	Njiani tukirudi Sabina alisema, sikuamini kwamba na wewe utaweza siku moja kuwa mtu mzima.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Kichwamaji* (2016)

Jedwali Na. 4.3.8.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Dhihaka Zilizotumika Katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute*

Na	Uk	Mfano wa Dhihaka
1	103	Alikwenda chumbani kwake akaleta kiti na baada ya kukaa aliwasalimu wageni, hamjambo watoto wazuri?
2	117	Huseni alicheka sana na kusema, tokea lini Karimjee Club wakaingia watu kama nyinyi? Kwani hamjui kwamba nyumba ile ni ya watukufu tu?

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute* (2016)

Jedwali Na. 4.3.8.1 na 4.3.8.2 yameonesha baadhi ya orodha ya matumizi ya tamathali ya semi ya dhihaka zilizotumiwa na waandishi wawili na kubainisha kufanana kwao kwa utumizi wa dhihaka na vile vile kukosekana tofauti ya utumizi wa tamathali za semi hiyo. Kwa hiyo swali namba moja na namba mbili limeweza kupata majibu.

4.3.9 Tamathali ya Semi ya Takriri

Kwa mujibu wa Msokile (1992). Tamathali ya semi ya takriri ni aina ya tamathali ya semi inayotumika kwa kurudia maneno, silabi au sauti zinazolingana katika kazi ya sanaa. Waandishi hutumia tamathali ya semi ya takriri kwa lengo la kusisitiza jambo. Kwa kutumia nadharia ya simiotiki mtafiti ameweza kubaini tamathali za semi za takriri zilizotumiwa na waandishi wote wawili na kubainika kufanana katika kutumia tamathali hii ya semi na kuorodhesha katika majedwali yafuatayo:

Jedwali Na. 4.3.9.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Takriri Zilizotumika Katika Riwaya ya *Kichwamaji*

Na	Uk	Mfano wa Takriri
1	4	Mambo waliyosema yalikuwa mengi. Mara kucheka, mara mimi sitaki, na mara huniamini.
2	12	Madeni, ndugu yangu, madeni. Utakuta wengi wana mikopo ajabu! Magari yote mikopo; maredio makubwa, yote mikopo; majiko ya kupikia, yote mikopo; karibu kila kitu cha maana kiko chini ya mkopo!
3	26	Ni mwendawazimu. Ninakwambia ukweli ni mwenda wazimu. Tena ningependa utusamehe kwa mambo aliyotenda. Ni mwendawazimu!
4	36	Basi, basi baba, nisamehe, nilisema upesi.
5	37	Rukia, nilimwita polepole. Rukia, niliita tena. Hakuniitikia. Nilijaribu tena. Rukia, jaribu kula chakula kidogo.
6	41	Matlida alitupa shoka chini aliponiona. Karibu! Karibu! Alipiga kelele.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Kichwamaji* (2016)

Jedwali Na. 4.3.9.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Takriri Zilizotumika**Katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute***

Na	Uk	Mfano wa Takriri
1	17	Sina shauri lolote, nimekuja kwako kukusikiliza utaniambia nini. Tafadhali nisitiri, nisitiri aibu yangu.
2	38	Nasema veve siku hizi nafatana na golo. Toka! Toka kwenda zako! Mimi sitaki ona hata uso yako.
3	40	Leo nimetamani kuja kukutembelea, siku nyingi sikukuona. Karibu basi, karibu ndani.
4	53	Na kama hakuja n'tayachoma moto, Wallahi n'tayachoma moto.
5	58	Halafu alisimama na kujishika kiuno. Wacha nikamtafute Denge, leo, leo n'do leo, lazima nitamwona, nitamsaka popote pale alipo.
6	60	Sikiliza Sista, hawa wakoloni na vijibwa vyao ni watu wapumbavu kabisa, kwao kila mtu ni mkoministi. Ukidai haki yako wewe koministi. Ukisema ukweli wewe koministi. Ukipinga utawala wewe koministi...
7	74	Alimfikiri Raza na kumuona kama mwendawazimu au labda mtu aliyepumbaa kwani watoto wazuri wote waliojaa katika jiji la Mombasa, yeye hakuona isipokuwa Yasmin. Yasmin, Yasmin, Yasmin gani naye?
8	77	Denge unataka nikuimbie kweli? Ala! Sasa unafikiri nakufanyia mzaha? Ngoja usiwe na haraka, iko siku nitakuambia. Iko siku nitakuambia...
9	95	Mimi sirudi, pendo jambo la hiari, hawawezi kunilazimisha kumpenda nisiyemtaka, Yasmin alisema, macho yake yashaanza kumbadilika machozi yanamlengalenga. Mimi sirudi! Sirudi! Sirudi ng'o.
10	109	Alimwombea dua, Mungu ampeleke salama, amrudishe salama, amnusuru na kila la shari

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute* (2016)

Jedwali Na. 4.3.9.1 na 4.3.9.2 yameonesha baadhi ya orodha ya matumizi ya tamathali ya semi ya takriri zilizotumiwa na waandishi wawili na kubainisha kufanana kwao kwa utumizi wa takriri na vile vile kukosekana tofauti ya utumizi wa tamathali za semi hiyo. Kwa hiyo swali namba moja na namba mbili limeweza kupata majibu.

4.3.10 Tamathali ya Semi ya Tabaini

Kwa mujibu wa Msokile (1992). Tamathali ya semi ya tabaini ni aina ya tamathali ya semi inayotumika kwa kusisitiza jambo kwa kutumia maneno ya ukinzani. Kwa kutumia nadharia ya simiotiki mtafiti ameweza kubaini tamathali za semi za tabaini zilizotumiwa na waandishi wote wawili na kubainika kufanana katika kutumia tamathali hii ya semi na kuorodhesha katika majedwali yafuatayo:

Jedwali Na. 4.3.10.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Tabaini Zilizotumika Katika Riwaya ya *Kichwamaji*

Na	Uk	Mfano wa Tabaini
1	10	Nilipotoka hospitalini nilikuwa na nia ya kusoma kufa kupona.
2	68	Na ndugu yangu akiwa amekwisha anza kula kidogo ingawa si sana.
3	104	Nikimpata mchumba sasa sijui nitampendaje! Nitamng'ang'ania kufa na kupona.
4	110	Njooi mnisaidie! Binti yangu mgonjwa sana. Sijui kama anapumua ama anakufa!
5	187	– kwamba unamfanya mtazamaji pia ashughulike. Aisogee mbele na kurudi nyuma, kuinama na kuinuka.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Kichwamaji* (2016)

Jedwali Na. 4.3.10.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Tabaini Zilizotumika**Katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute***

Na	Uk	Mfano wa Tabaini
1	12	Bado yungali mgeni mjini Mombasa, si jirani wala muhisani, si mjomba wala shangazi, hana wa kumzulia angalau akapata kisingizio cha ruhusa.
2	14	Wewe! Nimekuchukua kwenu hohehahe! Huna mbele wala nyuma unanuka umasikini leo umekuwa na jeuri enh?
3	29	Tokea kuhamia kwa Mwajuma, Yasmin hakuwa mtokaji. Alikuwa hendi harudi. Yeye na ndani na ndani na yeye, kama mwari.
4	37 akijiuliza. Niingiye au nisiingiye? Lakini mara alifikia uamuzi na bila ya kupoteza wakati aligonga mlango.
5	38	...Mwisho wa dhiki si dhiki ni faraja tu, Yasmin alijipa moyo.
6	42	Alisimama vile vile hendi harudi.
7	44	Baina yao hapakuwa na ugomvi wa kutofautiana na wote wawili wakawa na maisha ya bahati nasibu, leo wapate kesho wakose.
8	52	Wewe Yasmin huwajui vijana wa siku hizi, unayemdhania siye n'do ndiye.
9	58	Ah! Mambo makubwa haya. Naona ananiuliza mambo nisiyoyajua mbele wala nyuma.
10	70	Somoye. Mwari mzima anayetawishwa kwa mila na desturi za asili. Hatoki, hendi harudi yeye ni wa ndani tu.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute* (2016)

Jedwali Na. 4.3.10.1 na 4.3.10.2 yameonesha baadhi ya orodha ya matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini zilizotumiwa na waandishi wawili na kubainisha kufanana kwao kwa utumizi wa tabaini na vile vile kukosekana tofauti ya utumizi wa tamathali za semi hiyo. Kwa hiyo swali namba moja na namba mbili limeweza kupata majibu.

4.3.11 Tamathali ya Semi ya Msisitizo Bayani

Kwa mujibu wa Msokile (1992). Tamathali ya semi ya msisitizo bayani ni aina ya tamathali ya semi inayotumika kwa kuonesha ushindani wa mawazo. Kwa kutumia nadharia ya simiotiki mtafiti ameweza kubaini tamathali za semi za msisitizo bayani zilizotumiwa na waandishi wote wawili na kubainika kufanana katika kutumia tamathali hii ya semi na kuorodhesha katika majedwali yafuatayo:

Jedwali Na. 4.3.11.1 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Msisitizo Bayani

Uliotumika Katika Riwaya ya *Kichwamaji*

Na	Uk	Mfano wa Msisitizo bayani
1	73	Leo nimeota ndoto ya ajabu, alisema tena. Ulikuwa na mwanamke? Hata! Nimeota nikiwa mbinguni. Sema kweli! Kabisa!
2	122	Mimi siku hizi mambo ya dini haya nimeacha kuyafikiri sana. Ninachojua, ninajua; nisichojua, sijui; na ninachoamini, ninaamini. Haifai kujaribu kufahamu mambo usiyoweza kuelewa, Manase alisema.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Kichwamaji* (2016)

Jedwali Na. 4.3.11.2 Linaonesha Tamathali ya Semi ya Msisitizo Bayani

Zilizotumika Katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute*

Na	Uk	Mfano wa Msisitizo Bayani
1	59	Hakujua aanzie wapi lakini kwa ghafla aliuliza. Ati wewe msaliti! Msaliti! Denge alistuka na kushangaa. Msaliti nimemsaliti nani? Aliuliza.

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute* (2016)

Jedwali Na. 4.3.11.1 na 4.3.11.2 yameonesha baadhi ya orodha ya matumizi ya tamathali ya semi ya msisitizo bayani zilizotumiwa na waandishi wawili na kubainisha kufanana kwao kwa utumizi wa msisitizo bayani na vile vile kukosekana tofauti ya utumizi wa tamathali za semi hiyo. Kwa hiyo swali namba moja na namba mbili limeweza kupata majibu.

4.4 Hitimisho

Sehemu hii imejadili kuhusu usuli wa watunzi na matumizi ya tamathali za semi kama zilivyotumika na waandishi wawili teule kupitia riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*. Utafiti umebaini mfanano wao wa tamathali za semi kwani wote wametumia tamathali za semi kumi na moja na hivyo swali namba moja limeweza kujibiwa. Aidha utafiti haukukuta tofauti ya matumizi ya tamathali za semi kwa waandishi wote wawili na kwa ajili hiyo swali la pili limepata jawabu. Imebainika watunzi wote wametumia tamathali za semi za tashibiha, tashihisi, sitiari, mubalagha, tafsida, tauria, shitizai, dhihaka, takriri, tabaini na msisitizo bayani. Licha ya kufanana huko lakini pia utafiti umebaini kuwa mwandishi wa *Kichwamaji* ametumia tamathali za semi kidogo kuliko mwandishi wa *Vuta n'kuvute* na limesababishwa na ukubwa wa riwaya zenyewe, kwani riwaya ya *Vuta n'kuvute* ni refu kuliko riwaya ya *Kichwamaji* na pia uasili wa waandishi nao umechangia tofauti hiyo kwani Kezilahabi Kiswahili kwake ni lugha ya pili, tofauti na Shafi Kiswahili ni lugha yake ya kwanza.

4.5 Dhamira Zilizojitokeza Kutoka katika Tamathali za Semi

Kwa mujibu wa Mhilu na wenzake (2010:78). Dhamira ni wazo au mawazo makuu ambayo yamejitokeza katika kazi ya fasihi. Dhamira hugusa maeneo yote ya

kimaisha, uchumi, siasa, utamaduni na shughuli nyingine za kijamii kama vile elimu, afya na miundo mbinu mbalimbali. Vile vile tunaweza kusema. Dhamira ni mawazo yanayowasilishwa na msanii kupitia kazi yake ya fasihi. Katika kujibu swali la tatu la utafiti huu lenye kusema; Ni dhamira zipi zilizojitokeza katika tamathali za semi zilizotumika. Ndipo mtafiti akapata jibu la swali hili kwa kuziwasilisha data kwa njia ya maelezo zinazoonisha dhamira zilizojitokeza kupitia tamathali za semi zote alizozikusanya kwenye majedwali na kupata dhamira 22 zilizojitokeza kutoka katika tamathali za semi. Dhamira hizo ni kama zifuatazo:-

- (a) Uongozi mbaya.
- (b) Mapenzi nje ya ndoa.
- (c) Athari za umasikini.
- (d) Mapenzi kwa wanafamilia.
- (e) Athari ya uchawi na ushirikina.
- (f) Umuhimu wa umoja na mshikamano.
- (g) Ulevi wa kupindukia.
- (h) Mapenzi ya kweli.
- (i) Chuki na uhasama.
- (j) Unyanyasaji wa wanawake.
- (k) Kufanyakazi kwa bidii.
- (l) Usaliti.
- (m) Malezi mabaya kwa watoto.
- (n) Ujasiri na ushujaa.
- (o) Wivu wa kupindukia.
- (p) Upendo.

- (q) Imani za kidini.
- (r) Upendo kwa viumbe hai.
- (s) Umuhimu wa ndoa.
- (t) Uasharati.
- (u) Umuhimu wa elimu.
- (v) Ukombozi.

4.5.1.1 Dhamira ya Uongozi Mbaya

Dhamira hii ya uongozi mbaya ni miongoni mwa dhamira zilizoibuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n'kuvute* na kisha kuziorodhesha kwa njia ya majedwali tisa. Uongozi mbaya ni ile hali ya kiongozi au mkubwa wa sehemu yoyote katika taasisi za umma au taasisi binafsi kutumia vibaya madaraka yake juu ya wale anaowaongoza. Data zinazoonesha dhamira ya uongozi mbaya kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.1.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili vyenye sifa tofauti kwa kutumia kiunganishi ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 1: **Wazee kwa vijana, wake kwa wanaume. Wote kama wagonjwa wangojeao kumuona daktari.** Data hii inaonesha dhamira ya namna baadhi ya viongozi wasiowajali raia wanapokuja ofisini na kuwaacha wakisubiri kwenye bao kwa muda mrefu.

Pia katika ukurasa wa 7 kutoka jedwali hili namba 4.3.2.1 linaonesha data ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kuipa sifa ya kibinadamu kitu kisicho na sifa hio

kwa lengo la kuipamba kazi ya fasihi ambapo ametumia neno zero na kupewa tabia ya kibinadamu ya kucheka: **Sababu yenyewe ilikuwa kwamba mwalimu alimwekea zero kubwa yenye macho mawili na meno yakimcheka.** Data hii inaonesha dhamira ya baadhi walimu wakiwa kama ni viongozi wa madarsa wakitumia vibaya taaluma yao kwa wanafunzi ambapo hupelekea kurudisha nyuma maendeleo ya elimu kwa wanafunzi.

Jedwali Na. 4.3.5.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tafsida kwa kupunguza ukali wa maneno kwa kutumia neno nilimpa vibao badala ya neno kumpiga vibao na kuibua dhamira ya uongozi mbaya. Ukurasa wa 80: **Nilipomkaribia nilimpa vibao viwili vitatu akaanguka chini.** Data hii inaonesha dhamira ya baadhi ya kina kaka wanavyowalea vibaya wadogo zao wakiwa kama viongozi ndani ya familia kwa kutumia nguvu badala ya kuwaelimisha pindi wanapokosea.

Jedwali Na. 4.3.8.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya dhihaka kwa lengo la kumuweka mtu katika hali ya duni kupita kiasi. Ukurasa wa 2: **Wazee wengine hawana akili hata kidogo! Anaingia humu na fimbo! Anafikiri humu kuna vita.** Data hii inaonesha dhamira ya baadhi ya viongozi wasiojali utu wa mtu na hata kuwakemea na kuwakaripia watu wazima wanaotembea kwa mkongojo pindi wanapokuja ofisini mwao.

Data zinazoonesha dhamira ya uongozi mbaya kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.1.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa lengo la kufananisha vitu viwili vyenye sifa tofauti kwa kutumia kiunganishi. Katika tamathali hii ya tashibiha mwandishi amelinganisha mvumo wa sauti ya mtu kama mlio wa sauti ya tarumbeta. Ukurasa wa 66: **Aligonga mlango na suti nene iliyovuma kama mlio wa tarumbeta ilijibu come in.** Hii ni data inayoibua dhamira ya uongozi mbaya kwa kuonesha baadhi ya viongozi wa taasisi za umma wanavyotumia vibaya uongozi wao kwa kuwatisha watumishi wadogo wadogo.

Jedwali Na. 4.3.2.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi ilivyotumika na kuibua dhamira ya uongozi mbaya kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na uwezo huo. Ukurasa wa 135: **Juu ya dari yalining'inia mapankaboi mawili na yanapowashwa hulifukuza joto lote...** Data hii imetumia neno pankaboi ambalo limepewa uwezo wa kibinadamu wa kufukuza kitu na ilhali halina uwezo huo. Pia data imeibua dhamira ya uongozi mbaya unaofanywa na baadhi ya wakuu wa idara kwa kujipendelea wao peke yao mabo mazuri katika ofisi zao bila ya kuwajali watumishi wengine.

Jedwali Na. 4.3.4.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo yani kwa kutia chumvi. Ukurasa wa 135: **Ilikuwepo meza kubwa ya mzunguko wa yai na meza hio imezungukwa na viti vizuri vyenye mto laini ambayo mtu angeliweza kuikalia hata kutwa bila ya kuchoka.** Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imeibua dhamira ya uongozi mbaya kwa kuonesha baadhi ya viongozi wa taasisi za

umma wanavyojipendelea wao kwa kujiwekea vifaa bora vya kazi bila ya hata kuwajali watumishi wengine.

Jedwali Na. 4.3.7.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya shitizai / kejeli kwa kutumia maneno yenye kuleta maana kinyume iliyokusudiwa ama maana kinyume na ukweli ulivyo. Ukurasa wa 181: **Inspekta Wright amesimama mbele ya mlango wa ile nyumba, akamkaribisha kwa kumkejeli. Karibu bwana kubwa.** Data hii ya tamathali ya semi ya shitizai / kejeli imeibua dhamira ya uongozi mbaya kwa kuonesha namna baadhi ya viongozi wa serikali au taasisi za umma wanavyotumia vibaya madaraka yao kwa kuwadharau na kuwakejeli watu wengine.

Jedwali Na. 4.3.10.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini kwa kutumia maneno yanayosisitiza jambo kwa njia ya ukinzani. Ukurasa wa 85: **Koplo Matata alitoka kwa haraka na kiasi cha kufumba na kufumbua alirudi na jalada mkononi na kumkabidhi Inspekta Wright.** Data hii ya tamathali ya semi ya tabaini imeibua dhamira ya uongozi mbaya kwa kusisitiza jambo kwa kutumia maneno ya ukinzani pale aliposema kiasi cha kufumba na kufumbua alirudi na jalada... data hii inaonesha namna baadhi ya viongozi wanavyotumia vibaya madaraka yao kwa kuwatuma kwa njia isio sahihi watumishi wa umma.

4.5.1.2 Dhamira ya Mapenzi Nje ya Ndoa

Dhamira ya mapenzi nje ya ndoa imeibuliwa na mtafiti kupitia data alizozikusanya za matumizi ya tamathali za semi mbalimbali. Mapenzi nje ya ndoa ni ile hali ya mtu

aliyeoa au kuolewa akawa anafanya mapenzi kwa mtu mwingine, ilhali yeye ni mke au mume wa mtu. Waandishi wote wawili wametoa dhamira zinazohusu mapenzi nje ya ndoa. Miongoni mwa tamathali za semi zilizoibua dhamira hizo ni kama zifuatazo:

Data zinazoonesha dhamira ya mapenzi ya nje ya ndoa kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.1.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili kwa kutumia kiunganishi. Ukurasa wa 2: **Watu tulikua tumekaa nje tuliweza kusikia sauti yake ikinguruma kama samba.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imeibua dhamira ya mapenzi ya nje ya ndoa kwa kutumia ulinganishi wa ungurumaji wa sauti ya mwanamme kwa mwanamke wa nje kama mngurumo wa samba. Data hii inaonesha namna baadhi ya wanaume wanaotoka nje ya ndoa zao kwa kuwafuata wanawake na kuwatia maneno ili wakubaliwe jambo lao.

Jedwali Na. 4.3.4.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kuengeza chumvi. Ukurasa wa 70: **Tulikwenda kwa vidole mpaka mlango wa nyuma, tukajibanza ukutani.** Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imeibua dhamira ya mapenzi ya nje ya ndoa kwa kuonesha namna watu wanavyoenda kwa hawara wao kwa njia ya kificho sana. Data hii imeonesha baadhi ya wanaume wanaowaendea wanawake wa nje ya ndoa zao kwa kificho sana.

Jedwali Na. 4.3.5.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tafsida kwa kuficha matusi na kupunguza ukali wa maneno. Ukurasa wa 19:

Niliona wazi kwamba Manase alikuwa akijaribu kufanya mambo yasiyofaa.

Data hii ya tamathali ya semi ya tafsida imeibua dhamira ya mapenzi ya nje ya ndoa kuficha matusi na kutumia maneno laini kwa kusema kufanya mambo yasiyofaa. Data hii inaonesha namna baadhi ya wanaume wanaofanya mapenzi ya nje ya ndoa kwa kuwaacha wake zao na kuwaendea wanawake wa nje. Data zinazoonesha dhamira ya mapenzi ya nje ya ndoa kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.1.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili kwa kutumia kiunganishi ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 150: **Tumbo lilikwisha kuwa kubwa limeumuka kama aliyemeza hamira.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imeibua dhamira ya mapenzi ya nje ya ndoa kwa kulinganisha ukubwa wa tumbo na umezaji wa hamira. Data hii inaonesha namna madhara yanayopatikana iwapo mwanamke atafanya mapenzi nje ya ndoa yake kwani hukosa msaidizi wa kumsaidia katika kulea mimba.

Jedwali Na. 4.3.2.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kitu au kiumbe kisichokuwa na sifa hiyo. Ukurasa wa 105: **Aliwaza labda amweleze au aiweke siri ile moyoni mwake huku ikimla na kumtafuna pamoja na kumuondolea raha ya maisha.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imeibua dhamira ya mapenzi ya nje ya ndoa kwa kuipa neno siri uwezo wa kibinadamu wa kula na kutafuna na kumuondolea raha ya maisha kwa mpenzi wake wa nje. Data hii imeonesha namna

baadhi ya madhara wanayoyapata wapendanao wanaofanya mapenzi nje ya ndoa kwa kutokuwa na raha ya maisha.

Jedwali Na. 4.3.4.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kutia chumvi.

Ukurasa wa 21: **Salum alimtumbulia macho Yasmin akaanza kumchunguza tokea utosini hadi dole gumba halafu akamuuliza; hujambo dada?** Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imetoa dhamira ya mapenzi ya nje ya ndoa kwa kuonesha baadhi ya wanaume wanaowafuata wake za watu bila ya kujali kuwa wanawake hao wanawaume zao.

Jedwali Na. 4.3.9.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali za semi ya takriri kwa kuyarudia rudia maneno zaidi ya mara moja kwa ajili ya kuisitiza jambo. Ukurasa wa 77: **Denge unataka nikuimbie kweli? Ala! Sasa unafikiri nakufanyia mzaha? Ngoja usiwe na haraka, iko siku nitakuimbia. Iko siku nitakuimbia...** Data hii ya tamathali ya semi ya takriri imeibua dhamira ya mapenzi ya nje ya ndoa kwa kuyarudia rudia baadhi ya maneno; "...iko siku nitakuimbia. Iko siku nitakuimbia..." kwa kuisitiza namna baadhi ya wanandoa huwakimbia waume zao na kwenda kwa wanaume wa nje na kuwafanyia mambo makubwa ikiwemo ya kuwaimbia.

Jedwali Na. 4.3.10.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini kwa kuisitiza jambo kwa kutumia maneno kinzani ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 74: **Mwisho Bwana Raza alimwomba mjomba wa Yasmin aseme na mpwawe, amlani shetani, awaze nyuma na mbele na arudi.** Data hii ya tamathali ya semi ya tabaini inaonesha dhamira ya mapenzi ya nje

ya ndoa jinsi yanavyoathiri wapendanao na kufanya baadhi ya wanandoa hao kuathirika kisaikolojia.

4.5.1.3 Dhamira ya Umasikini

Dhamira hii ya umasikini, mtafiti ameibua kupitia data alizokusanya za matumizi ya tamathali za semi mbalimbali. Umasikini ni ile hali ya mtu kuishi katika hali ya shida katika kupatikana mlo wake wa kila siku na aghalabu hupata mlo chini ya mahitaji yake na wakati mwingine hukosa kabisa. Dhamira hii imeoneshwa kupitia katika data zilizokusanywa kutoka kwa waandishi wote wawili katika majedwali yafuatayo:

Data zinazoonesha dhamira ya umasikini kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.1.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili kwa kutumia kiunganishi. Ukurasa wa 3: **Mgongo wa mzee huyo sasa ulikuwa kama ukurasa ambao haukuandikwa maneno.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imeonesha dhamira ya umasikini kwa kulinganisha mgono wa mzee aliyekuwa nguo yake imechanika ni kama ukurasa na kubainisha umasikini uliomo katika jamii.

Jadeli namba 4.3.9.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia baadhi ya maneno zaidi ya mara moja kwa lengo la kuisisitiza ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 12: **Madeni, ndugu yangu, madeni. Utakuta wengi wana mikopo ajabu! Magari yote mikopo; maredio makubwa, yote mikopo; majiko ya kupikia, yote mikopo; karibu kila kitu cha maana kiko**

chini ya mkopo! Data hii ya tamathali ya semi ya takriri imeonesha dhamira ya umasikini kwa kuonesha hali halisi ya watu wakipato cha chini na namna wanavyoishi kwa mikopo na kubaki na umasikini huku wakiwa na madeni.

Data zinazoonesha dhamira ya umasikini kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.1.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili kwa kutumia kiunganishi. Ukurasa wa 52: **Denge kuja kunijazia makorokocho chumbani, chumba chenye kama kifuu, kucha mtu halali kwa ghasia za panya.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imeibua dhamira ya umasikini kwa kulinganisha chumba cha mtu masikini hujaa makorokocho nan i kidogo kama kifuu.

Jedwali Na. 4.3.2.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na sifa hiyo. Ukurasa wa 10: **Nyumba za mtaa ule zilikuwa za kizamani zilizoshikana moja baada ya nyingine.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imetoa dhamira ya umasikini kwa kuonesha namna nyumba za wakaazi masikini zinavyoshikana ambapo ni sifa ya kibinadamu na kuibua umasikini uliomo katika jamii.

Jedwali Na. 4.3.4.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kutia chumvi ili kuisitiza ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 246: **Walimkuta nje akicheza na watoto wenzake, amejaa vumbi, shati na suruali aliyoivaa ni dongo tupu, nguo zote nyekundu kwa udongo wala huwezi kujua zilikuwa na rangi gani hapo**

mwanzo. Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imeibua dhamira ya umasikini kwa kuonesha namna maisha ya watu masikini yalivyo baadhi yao hata sabuni ya kufulia nguo huwashinda na nguo kubakia na taka hadi kubadilika rangi.

Jedwali Na. 4.3.7.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya shitizai kwa kutumia maneno yenye kuleta maana iliyokinyume na ile iliyokusudiwa au hata kinyume na ukweli ulivyo. Ukurasa wa 112: **Afadhali Yasmin, wao walifikiri labda ni bibiye kama wao, lakini walipomwangalia Mwajuma walimwona kama kisonoko tu kilichotumwa kumsindikiza bibiye mwenzao madukani.** Data hii ya tamathali ya semi ya shitizai imeibua dhamira ya umasikini kwa kuonesha namna baadhi ya watu wanavyowadhania watu weusi kuwa ni watu wasio na uwezo wa hata kuingia katika maduka makubwa makubwa kwa kuwaona wao ni masikini.

Jedwali Na. 4.3.9.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia baadhi ya maneno kwa lengo la kusisitiza jambo fulani. Ukurasa wa 53: **Sikuwahi kufika, nimekutana na rafiki yake njiani na kaniahidi kwamba atamwambia aje kuyachukua. Na kama hakuja n'tayachoma moto, Wallahi n'tayachoma moto.** Data hii ya tamathali ya semi ya takriri imeibua dhamira ya umasikini kwa kuonesha namna zilivyo nyumba za watu masikini zinashindwa kuwa na hata chumba cha kuhifadhia vitu na kupelekea kero kwa wakaazi wa nyumba hio.

Jedwali Na. 4.3.10.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini kwa kusisitiza jambo kwa kutumia maneno kinzani kwa lengo la

kufikisha ujumbe. Ukurasa wa 204: **Yasmin anaelewa vyema kwamba maisha ya kimaskini ni ya bahati nasibu. Mara uko chini umezama mara uko juu unaelea, unasukumwa huku na huku na mawimbi ya maisha.** Data hii ya tamathali ya semi ya tabaini imeibua dhamira ya umasikini kwa kutumia maneno yenye kusisitiza jambo kwa ukinzani, kwa ukinzani wa maneno “Mara uko chini umezama mara uko juu unaelea” na kuweza kuonesha hali halisi ya watu masikini kuwa maisha yao ni ya kubahatisha mara leo upate kesho ukose.

4.5.1.4 Dhamira ya Mapenzi kwa Wanafamilia

Dhamira hii ya mapenzi kwa wanafamilia imeibuliwa na mtafiti kupitia data alizozikusanya za matumizi ya tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n’kuvute*. Mapenzi kwa wanafamilia ni ile hali ya mtu au watu kuwa na furaha kwa familia yake na kuijali kwa hali na mali na siku zote huitakia mema familia hiyo na huumia katika nafsi yake iwapo itafikwa ma mabaya. Mtafiti ameionyesha dhamira hii kupitia data mbalimbali alizozikusanya za tamathali ya semi kupitia waandishi wateule kwa njia ya majedwali kama ifuatavyo:

Data zinazoonyesha dhamira ya mapenzi kwa wanafamilia kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.1.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili tofauti kwa kutumia kiunganishi.ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 23: **Walikuja mbio kama kwamba atakayekuwa wa kwanza kufika atapata zawadi.** Data hii ya tamathali ya zemi ya tashibiha imeibua dhamira ya mapenzi kwa wanafamilia kwa kutumia maneno

yanayoonesha ulinganishi wa vitu viwili kwa kutumia kiunganishi na kudhihirisha mapenzi waliyokuwa nayo baadhi ya ndugu kwa jamaa zao kwa kuwa na hamu na shauku ya kuwapokea wakati wakitoka safari ya mbali.

Jedwali Na. 4.3.2.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kiumbe kisicho na uwezo huo.

Ukurasa wa 82: **Alikuwa amefunikwa mwili mzima isipokuwa uso ndio uliokuwa umewachwa wazi ukidai machozi mengi zaidi.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imeibua dhamira ya mapenzi kwa wanafamilia kwa kutumia neno uso na kuupa uwezo wa kibinadamu wa kudai / kutaka kuliliwa kwa machozi mengi wakati wa msiba wa ndugu wa familia na kudhihirisha mapenzi ya wanafamilia hao.

Jedwali Na. 4.3.6.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tauria kwa kutumia maneno yenye tahajia moja lakini maana ya maneno hayo huwa tofauti ili kusisitiza ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 66: **Ukitembea**

huko nje watu watakuuliza, nyumbani hawajambo? Utajibuje kama hukuwasabahi asubuhi. Data hii ya tamathali ya semi ya tauria imefanikisha kazi ya mtafiti kwa kuibua dhamira ya mapenzi kwa wanafamilia kwa kutumia maneno “hukuwasabahi asubuhi” na kudhihirisha mapenzi ya wanafamilia hao ya kuulizana hali kila siku aubuhi kabla ya kutoka kwenda katika kazi zao.

Jedwali Na. 4.3.9.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya takriri kwa kulirudia rudia neno zaidi ya mara moja ili kusisitiza ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 82: **Kazimoto, ndugu yako ha, ...ako kati... katika**

hali mbaya sana, umkute, umkute! Data hii ya tamathali ya semi ya takriri imeibua

dhamira ya mapenzi ya wanafamilia kwa kusisitiza jambo la upendo kwa ndugu wa familia na kuonesha umuhimu wa kuwahudumia ndugu wakati wanapoumwa kabla ya kuwakuta mauti.

Jedwali Na.4.3.10.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini kwa kutumia maneno ya kusisitiza jambo kwa njia ya ukinzani.

Ukurasa wa 68: **Na ndugu yangu akiwa amekwisha anza kula kidogo ingawa si sana.** Data hii ya tamathali ya semi ya tabaini imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya mapenzi ya wanafamilia kwa kutumia maneno yenye kusisitiza upendo kwa wana ndugu ingawa kwa njia ya ukinzani wa maneno, pale aliposema “amekwisha anza kula kidogo ingawa si sana”.

Data zinazoonesha dhamira ya mapenzi kwa wanafamilia kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n’kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.1.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili tafauti kwa kutumia kiunganishi kwa lengo la kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 246: **Sasa ni mtoto mkubwa wa miaka mitatu. Kitoto kizuri, kishamba kwisha kazi, mchangamfu, maneno kama chiriku.** Data hii ya tamathali ya semi imeibua dhamira ya mapenzi ya wanafamilia kwa kufananisha uchangamfu wa mtoto na kufananishwa na chiriku, hivyo dhamira hii inatoa ujumbe kwa wazazi juu ya kuwajali watoto wao na kuwalea kwa mapenzi ya baba na mama.

Jedwali Na. 4.3.4.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko yalivyo kwa kutia chumvi ili

kusisitiza ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 59: **Mtu wewe! Uko wapi? Hakuna pembe ya mji niliyoibakisha kukutafuta wewe. Mwajuma alilalamika.** Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya mapenzi ya wanafamilia kwa kutumia maneno yenye kuonesha ukuzaji wa mambo uliko vile yalivyo kwa maneno “hakuna pembe ya mji niliyoibakisha kukutafuta wewe” hivyo dhamira hii inaonesha namna wana ndugu wanavyopendana na kutafutana sana ikiwa hawaonani.

Jedwali Na. 4.3.9.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia maneno zaidi ya mara moja kwa lengo la kusisitiza ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 40: **Leo nimetamani kuja kukutembelea, siku nyingi sikukuona. Karibu basi, karibu ndani.** Data hii ya tamathali ya semi ya takriri imeibua dhamira ya mapenzi ya wanafamilia kwa kutumia neno “karibu sana” na kulirudia zaidi ya mara moja kwa lengo la kusisitiza ujumbe uliokusudiwa, na kuonesha namna baadhi ya wanandugu wanavyopendana na huwa na furaha kubwa siku wanapokutana.

4.5.1.5 Dhamira ya Uchawi na Ushirikina

Dhamira hii ya uchawi na ushirikina imeibuliwa na mtafiti kupitia data alizozikusanya za matumizi ya tamathali ya semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* tu. Kwani katika riwaya ya *Vuta n’kuvute* dhamira hii haikupatikana kupitia tamathali za semi zilizotumika. Uchawi na ushirikina ni hali ya mtu au watu kuwa na imani ya mambo au vitu vya kimazingara ambapo huviamini kwa kumleta manufaa au madhara na humpasa kufuata taratibu hizo. Na mambo ya vitu / imani hiyo huwa havionekani kwa macho bali ni mambo ya kufikirika tu.

Data zinazoonesha dhamira ya uchawi na ushirikina kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.1.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili tofauti kwa kutumia kiunganishi ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 24: **Kila mtu alikuwa akitembea polepole kama mgonjwa.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imeibua dhamira ya uchawi na ushirikina kwa kutumia maneno ya ulinganishi kwa kutumia kiunganishi kwa kuonesha hofu iliyowajaa kutokana na uchawi na ushirikina na kuwafanya kutembea kama wagonjwa, dhamira hii inaonesha namna uchawi na ushirikina jinsi unavyoleta madhara katika jamii.

Jedwali Na. 4.3.2.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya sirmi ya tashihisi kwa kukipa uwezo wa kibinadamukitu kisicho na uwezo huo kwa lengo la kufikisha ujumbe. Ukurasa wa 30: **Niliona kwamba watu wote wa nyumbani kwetu walikuwa wanekwisha nyang'anywa utu wao, hapakuwa na mtu tena pale nyumbani.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imeibua dhamira ya uchawi na ushirikina kwa kuupa uchawi uwezo wa kibinadamu wa kuwanyang'anya watu utu wao na kuonesha namna uchawi unavyoleta madhara katika jamii.

Jedwali Na. 4.3.4.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kutia chumvi. Ukurasa wa 30: **Sikutaka kugeuzwa na hofu kama wao; wao walikwisha kuwa watu ambao hawawezi hata kuguna.** Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imeibua dhamira ya uchawi na ushirikina kwa kutumia maneno yanayoonesha

ukuzaji wa mambo kuliko vile yalivyo na kuonesha jinsi uchawi na ushirikina unavyotia hofu kwa watu mpaka ikawa hawawezi hata kuguna.

4.5.1.6 Dhamira ya Umoja na Mshikamano

Dhamira hii ya umoja na mshikamano imeibuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za matumizi ya tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*. Umoja na mshikamano ni hali ya watu wa jamii moja au tofauti kushirikiana kwa pamoja katika shughuli zao za kijamii, kiuchumi, kisiasa na kadhalika. Mtafiti ameibua dhamira hii kutoka kwa waandishi wote wawili.

Data zinazoonesha dhamira ya umoja na mshikamano kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.1.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili tofauti kwa kutumia kiunganishi.

Ukurasa wa 180: **Baada ya mazishi tulirudi nyumbani mikono mitupu. Matumaini yetu yalifutika kwa urahisi kama mwalimu afutavyo mandishi yake ubaoni ambayo bado hayajanakiliwa na wanafunzi.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imeibua dhamira ya umoja na mshikamano uliooneshwa wakati wa mazishi ya mtoto wa Kazimoto kwa kuwashirikisha wanajamii wote waliowazunguka kwa kulinganisha matumaini yao yaliyopotea na kufutwa kwa maandishi ya kwenye ubao.

Jedwali Na. 4.3.2.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na uwezo huo ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 98: **Siku ya tatu Kalia pia alitusaidia;**

lakini hata hivyo shamba lilikuwa bado linatutazama. Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imeibua dhamira ya umoja na mshikamano kwa kuonesha mashirikiano yaliyofanywa na ndugu na majirani katika kazi ya shambani, hivyo data inaonesha namna ya ukubwa wa shamba ulivyopewa sifa ya kibinadamu ya kuwaangalia.

Data zinazoonesha dhamira ya umoja na mshikaano kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.1.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulin ganisha vitu viwili vilivyo tofauti kwa kutumia kiunganishi. Ukurasa wa 203: **Mambo alimweleza. Siye tena yule Mambo anayechekacheka ovyo kama bahuli.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imefanikisha kazi ya mtafiti kwa kuibua dhamira ya umoja na mshikamano kwa wanamampambno wakati mwenzao Denge amefungwa na kupanga njama za kumtorosha jela, kwa kulinganisha uchekekaji ovyo wa Mambo na bahuli.

Jedwali Na. 4.3.3.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya sitiari kwa kuhusisha matendo ya vitu, au tabia ya vitu vyenye maumbile tofauti na kuleta uhamisho wa kimaana. Ukurasa 96: **Basi kila siku aje kwetu tu, kwani nyumba yetu msikiti?** Data hii ya tamathali ya semi ya sitiari imeibua dhamira ya umoja na mshikamano kwa wanajamii kwa kutumia mneno yenye ulinganishi wa nyumba na msikiti na hivyo kuhimiza suala la kutembeleana.

Jedwali Na. 4.3.4.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kutia chumvi kwa lengo la kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 31: **Ama kweli shoga yangu**

ulikuwa hupo ulimwenguni. Leo mji mweupe, kuna dansa la kukata na shoka Raha leo. Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imeibua dhamira ya umoja na mshikamano uliooneshwa na Mwajuma na shoga yake Yasmin kwa kutumia maneno “shoga yangu ulikuwa hupo ulimwenguni”.

Jedwali Na. 4.3.10.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini kwa kutumia maneno yenye kuonesha ukinzani kwa kusisitiza jambo. Ukurasa wa 29: **Tokea kuhamia kwa Mwajuma, Yasmin hakuwa mtokaji. Alikuwa hendi harudi. Yeye na ndani na ndani na yeye, kama mwari.** Data hii ya tamathali ya semi ya tabaini imefanikisha kazi ya utafiti kwa kuibua dhamira ya umoja na mshikamano kwa kusisitiza jambo kwa kutumia maneno ya ukinzani ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. pale aliposema “tokea kuhamia kwa Mwajuma, Yasmin hakuwa mtokaji. Alikuwa hendi harudi”.

4.5.1.7 Dhamira ya Ulevi wa Kupindukia

Dhamira hii ya ulevi wa kupindukia imeibuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n’kuvute*. Ulevi wa kupindukia ni hali ya mtu kutumia vitu vinavyoleweshwa na kumfanya akili yake itawaliwe na vitu hivyo na hufanya jambo kinyume na matakwa ya akili yake.

Data zinazoonesha dhamira ya ulevi wa kupindukia kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.1.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili tafauti kwa kutumia kiunganishi ili

kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 81: **Nilipokuwa njiani nikirudi nyumbani nilisikia sauti za walevi wakiimba kama kwamba wakilia.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya ulevi wa kupindukia kwa kuonesha ulinganishi wa sauti za walevi wakati wakiimba ikawa kama wanalia, hivyo dhamira imeonesha athari ya ulevi wa kupindukia ambapo humfanya mnywaji kutojielewa anafanya nini.

Jedwali Na. 4.3.2.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na uwezo huo ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 44: **Hofu kubwa ilinishika na pombe yote iliruka. Niliona mwisho wa maisha yangu hapa duniani.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya ulevi wa kupindukia kwa kutumia maneno yenyenukuipa uwezo wa kibinadamu pombe wa kuruka na kuonesha ya madhara ya pombe yanavyopelekea mafia kwa watumiaji.

Jedwali Na. 4.3.4.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kutia chumvi kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kutia chumvi. Uk wa 56: **Leo sitakunywa pombe. Unafahamu usiku nilipofika kitandani nilikufa.** Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imeweza kuibua dhamira ya ulevi wa kupindukia kwa kuukuza usingizi wa mlevi ukawa sawa na kufa hivyo kuonesha namna mtu anapokunywa pombe huwa akili inamruka na hawezi kufanya jambo lolote linaliongozwa na akili yake.

Jedwali Na. 4.3.7.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya shitizai kwa kutumia maneno yenye kuleta maana iliyokinyume na ile iliyokusudiwa ama kinyume na ukweli ulivyo. Uk wa 171: **Galoni mbili tu! Pombe ya huku si kama ya kwenu Ukerewe. Mke wangu ananiambia kila siku kwamba pombe ya kwenu inaleweshana sana. Ya hapa ni maji, yatawezaje kuleweshana?** Data hii ya tamathali ya semi ya shitizai imeibua dhamira ya ulevi wa kupindukia kwa kutumia maneno yaliyo kinyume na maana iliyokusudiwa ama kinyume na ukweli ulivyo kwa kuonesha galoni mbili haziwezi kumleweshana mtu wakati sio kweli.

Data zinazoonesha dhamira ya ulevi wa kupindukia kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.1.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili vinavyotofautiana kwa kutumia kiunganishi ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 24: **Waliingia vichochoroni, Salum mbele Roger nyuma anafuata tu kama mkia.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imeibua dhamira ya ulevi wa kupindukia kwa kuonesha namna baadhi ya watu katika jamii huwa hawajihisi raha katika maisha yao mpaka wapate pombe. Dhamira inaonesha namna ugeni alionao Roger na kufuata kwake nyuma nyuma kufuata pombe kukafanishwa na mkia.

Jedwali Na. 4.3.2.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kiumbe kisicho na uwezo huo ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 245: **Baada ya kiasi cha mikupuo mitatu, Salum alitulia na sigara yake mkononi akisikiliza pombe inamwambia**

nini kichwani mwake. Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imeweza kuibua dhamira ya ulevi wa kupindukia kwa kuipa pombe uwezo wa kibinadamu wa kuweza kumwambia mtu kitu au jambo. Hivyo dhamira inaonesha namna ulevi unavyompelekea mtu kufanya jambo kinyume na matakwa ya akili yake.

4.5.1.8 Dhamira ya Mapenzi ya Kweli

Dhamira hii ya mapenzi ya kweli imeibuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n'kuvute*. Mapenzi ya kweli ni ile hali ya mtu kuwa na furaha ya dhati ya ndani ya moyo wake juu ya jambo anapolipata au kwa mtu anapokutana nae na wakati wote hutamani jambo lake au mtu ampate kwa hali ya furaha. Hivyo dhamira hii ni muhimu sana kwa maisha ya wanadamu kama ilivyoelezwa na waandishi wawili wa vitabu teule.

Data zinazoonesha dhamira ya mapenzi ya kweli kama zilizoordheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jadwel namba 4.3.1.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili tafauti kwa kutumia kiunganishi ili kuipamba kazi ya msanii na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 106: **“Ashama” alinambia. Niliashama kama kinda la ndege kiotani.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imeweza kuibua dhamira ya mapenzi ya kweli kwa kuonesha namna mtu anavyokuwa tayari kuitikia yale anayoambiwa na mpenzi wake hata kama ni jambo la kitoto. Pale alipolinganisha suala la kumlisha kitu mdomoni na kinda la ndege.

Jedwali Na. 4.3.4.1 linaonesha data zilizokusanywa za tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kutia chumvi. Ukurasa wa 18: **Uzuri wake kama nilivyosikia watu wakisema, ulikuwa ni uzuri wa aina ya pekee. Uzuri ambao hata kipofu aliweza kuuona.** Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imefanikisha kazi ya mtafiti kwa kuibua dhamira ya mapenzi ya kweli kwa kuonesha namna Kazimoto alivyokuwa akimpenda Sabina hadi kufikia kuzidisha uzuri wake na kusema hata kipofu anauona.

Jedwali Na. 4.3.6.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tauria kwa kutumia maneno yenye tahajia moja. Tahajia hizo huwa katika herufi lakini maana ya maneno hayo ni tofauti. Ukurasa wa 157: **Kila siku Sabina, alifoka, wengine wanaita wake zao Maggy, Betty; wewe kila siku Sabina! Sabina! Unataka kusabina nini. Mapenzi gani hayo!** Data hii ya tamathali ya semi ya tauria imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya mapenzi ya kweli kwa wapendanao pale aliposema “Sabina! Sabina! Unataka kusabina nini.” na kuonesha wapenzi siku zote hupeana majina mazuri mazuri kulinga na mapenzi yao.

Jedwali Na. 4.3.10.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini kwa kusisitiza jambo kwa kutumia maneno yenye ukinzani ili kusisitiza ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 104: **Nikimpata mchumba sasa sijui nitampendaje! Nitamng’ang’ania kufa na kupona.** Data hii ya tamathali ya semi ya tabaini imefanikisha kazi ya mtafiti kwa kuibua dhamira ya mapenzi ya kweli kwa wapendanao kwa kuonesha namna baadhi ya watu wanavyojua kupenda hadi kusema wataamng’ang’ania mpenzi wake kufa na kupona.

Data zinazoonesha dhamira ya mapenzi ya kweli kama zilizoordheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.1.2 linaonesha data zilizorodheshwa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili vinavyotofautiana kwa kutumia kiunganishi ili kuipamba kazi ya msanii na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 11: **Mikono huinyanyua na kuishusha, akijibenua na kujinyonganyonga mithili ya mkunga aogelevyo kupitia mapangoni.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imafanikisha kazi ya mtafiti kwa kuibua dhamira ya mapenzi ya kweli kwa wapendanao kwa kulinganisha namna ya kujibenua na kujinyonganyonga mbele ya mpenzi wake na ujinyongoaji wa mkunga. Hivyo dhamira imeonesha namna mpenzi hufanya lolote la kumridhisha mpenzi wake.

Jedwali Na. 4.3.2.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na sifa wala uwezo huo ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 36: **Hakupata kusafiri na husikia tu kwa wale wanaotweka mitepe yao, wakapambana na dharuba za kusi na kaskazi, bahari inapotafirika.** Data hii ya tamathali za semi ya tashihisi imeweza kufanikisha kazi ya mtafiti kwa kuibua dhamira ya mapenzi ya kweli kwa kuipa bahari uwezo wa kibinadamu wa kutafaranika, dhamira imeonesha mapenzi ya kweli aliyonayo Bukheti ambaye alihama Mombasa na kwenda Unguja kwa ajili ya mwanamke.

Jedwali Na. 4.3.4.2 linaonesha data zilizokusanywa za tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kutia chumvi. Ukurasa wa 161: **Ama leo. Tulikuwa hatuna nafasi hata ya kumeza mate. Denge wee, Denge**

wee, Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imeweza uibua dhamira ya mapenzi ya kweli kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo pale alipoonesha namna Yasimn alipokuwa akimtaja mpenzi wake hata ikawa ikwa watu hawana nafasi hata ya kumeza mate.

Jedwali Na. 4.3.6.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tauria kwa kutumia maneno yenye tahajia moja lakini maana zake ni tofauti ili kuipamba kazi yake na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 246: **Mambo akaanza mambo yake. Bwan Badi ndo ushakwama Unguja.** Data hii ya tamathali ya semi ya tahajia imeweza kuibua dhamira ya mapenzi ya kweli kwa kutumia neno “mambo” kwa maana mbili tofauti na kuonesha dhamira hio namna mapenzi yalivyomfanya Bwan Badi kuhama Mombasa na kuhamia Unguja.

Jedwali Na. 4.3.9.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia maneno zaidi ya mara moja ili kusisitiza ujumbe uliokusudiwa na kufikisha ujumbe wake kwa hadhira. Ukurasa wa 109: **Alimwombea dua, Mungu ampeleke salama, amrudishe salama, amnusuru na kila la shari.** Data hii ya tamathali ya semi ya takriri imefanikisha kazi ya utafiti kwa kuibua dhamira ya mapenzi ya kweli kwa kuyarudia rudia maneno zaidi ya mara moja na kuonesha namna Yasmin alivyokuwa na mapenzi ya kweli kwa Denge wakati akimuaga kwa ajili ya safari.

Jedwali Na. 4.3.10.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini kwa kusisitiza jambo kwa kutumia maneno yenye ukinzani ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Uk wa 44: **Baina yao hapakuwa na ugomvi wa**

kutofautiana na wote wawili wakawa na maisha ya bahati nasibu, leo wapate kesho wakose. Data hii ya tamathali ya semi ya tabaini imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya mapenzi ya kweli kwa wapendanao kwa kuonesha namna Mwajuma alivyokuwa akimpenda kikweli shoga yake Yasmin hata wakaweza kuishi katika maisha ya leo kupata kesho wakose.

4.5.1.9 Dhamira ya Chuki na Uhasama

Dhamira hii ya chuki na uhasama imebuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n'kuvute* na kuziorodhesha kwa njia ya majedwali tisa. Chuki na uhasama ni ile hali ya mtu kuwa na donge ndani ya nafsi yake na kutojali wala kutofurahi kwa yale mazuri anayoyapata mwenzake na wakati mwengine hupelekea kugombana na hata kutaka lile jambo zuri kwa mwenziwe limuondokee. Hivyo dhamira hii ina athari kubwa tena mbaya kwa maisha ya wanadamu kama ilivyoielezwa na waandishi wawili wa vitabu teule.

Data zinazoonesha dhamira ya chuki na uhasama kama zilizoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.2.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na sifa na uwezo huo. Ukurasa wa 13: **Nilikata shauri kwenda kuutazama ili kutuliza kichwa changu kidogo chenye kiburi.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imeweza kuibua dhamira chuki na uhasama kwa kukipa kichwa sifa ya kibinadamu ya kuwa nakiburi na kuweza kudhihirisha chuki aliyokuwa nayo Kazimoto kwa Manase.

Jedwali Na. 4.3.3.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya sitiari kwa kulinganisha vitu viwili vyenye maumbile tofauti kwa lengo la kuleta msisitizo wa jambo fulani. Ukurasa wa 44: **Nilikuwa maiti, na ninafikiri kwamba sasa ungekuwa unalia...** Data hii ya tamathali ya semi ya sitiari imefanikisha kazi ya utafiti kwa kuibua dhamira ya chuki na uhasama kwa kulinganisha uhai wa Kamata na umauti wake iliyofanywa na vijana wawili waliomlewesha Kamata na kumpiga kwa sababu ya kukataliwa na mkewe.

Jedwali Na. 4.3.5.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tafsida kwa kupunguza ukali wa maneno au kuficha matusi. Ukurasa wa 21: **Manase anamwita ndugu yangu malaya!** Data hii ya tamathali ya semi ya tafsida imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya chuki na uhasama iliyofanywa na Manase baada ya kumbaka Rukia na kumpa ujauzito kisha akamwita Malaya.

Jedwali Na. 4.3.7.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya shitizai inayotumika kwa kukusudia kuleta maana iliyo kinyume na ile iliyokusudiwa ama kinyume na ukweli ulivyo.. Ukurasa wa 25: **Nimekuja kuuliza kama una habari yoyote kuhusu mtoto wetu. Mtoto gani? Huyo mwenda wazimu, alijibu.**

Data hii ya tamathali ya semi ya shitizai imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya chuki na uhasama kwa kuonesha chuki aliyokuwa nayo Kazimoto kwa Manase kutokana na kumharibia masomo yaake Rukia kwa kumbaka na kumtia mimba na ndipo wakamwita mwenda wazimu.

Data zinazoonesha dhamira ya chuki na uhasama kama zilizoordheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.1.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tasibiha kwa kulinganisha vitu viwili vilivyo tofauti kwa kutumia kiunganishi ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 152: **Mwajuma chini Yasmin juu. Nguo zimewapanda mpaka mapajani kila mmoja anapiga mikambi kama chatu waliokatwa vichwa.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya chuki na uhasama kwa kulinganisha mvurugano na makambi ya chatu yaliyooneshwa kupitia kwa Mwajuma na Yasmin na hadi kupelekea kupigana baina yao.

Jedwali Na. 4.3.2.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kuipa sifa na uwezo kibinadamu kitu kisicho na uwezo huo ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 171: **Alikunjua kirago kimoja akalie lakini alipokikunjua kunguni walikuwa wakiendeshana mbio kama wenye kucheza foliti.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya chuki na uhasama kwa kuwapa kunguni uwezo wa kibinadamu wa kucheza foliti, hivyo dhamira imedhihirisha chukina uhasama waliyofanyiwa wapigania uhuru hadi kupelekea kufungwa bila ya kosa lolote.

Jedwali Na. 4.3.4.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kutia chumvi. Ukurasa wa 179: **Hatari! Denge alisema. Sio hatari tu, ni mauti hasa. Alisema**

yule mfungwa akimaliza kuziweka sawa nywele za Denge. Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imeweza kuibua dhamira ya chuki na uhasama kwa kuyakuza mateso wanayoyapata wafungwa wa kisiasa kuwa si mateso bali ni kifo, hivyo dhamira imeweza kuonesha chuki walizonazo wakoloni dhidi ya wapiganaji wa uhuru.

Jedwali Na. 4.3.7.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya shitizai / kejeli kwa kutumia maneno yanayokusudia kuleta maana iliyo kinyume na ile iliyokusudiwa ama kinyume na ukweli ulivyo ili kuipamba kazi ya fasihi. Ukurasa wa 69: **Unaonaje basi tukaja wote mimi na wewe tukaja usiku? Lo! Hata ingelikuwa nimekosa mtu wa kufuatana naye.** Data hii ya tamathali ya semi ya shitizai imeweza kuibua dhamira ya chuki na hasama kwa kutumia maneno yenye kuleta maana kinyume na kuweza kuonesha chuki na uhasama uliopo kati ya wazalendo wenye kudai uhuru wa nchi yao na wakoloni na vaibaraka wao.

Jedwali Na. 4.3.10.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini kwa kutumia maneno yenye kusisitiza jambo kwa njia ya ukinzani ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 37: **Wakati yumo katika mawazo hayo, alijishtukia amekwishafika Kiponda amesimama mbele ya mlango wa nyumba ya mama yake, akijiuliza. Niingiye au nisiingiye? Lakini mara alifikia uamuzi na bila ya kupoteza wakati aligonga mlango.** Data hii ya tamathali ya semi ya tabaini imeweza kufanikisha kazi ya utafiti huu kwa kuibua dhamira ya chuki na uhasama kwa kutumia maneno kinzani katika kusisitiza jambo, pale aliposema “niingiye au nisiingiye” data hii imeweza kuonesha chuki

walizonazo baadhi ya wazazi kwa watoto wao inayosababishwa na wao wazazi kuwalazimisha katika ndoa.

4.5.1.10 Dhamira ya Unyanyasaji wa Wanawake

Dhamira hii ya unyanyasaji wa wanawake imeibuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n'kuvute* na kisha kuziorodhesha kwa njia ya majedwali tisa. Unyanyasaji wa wanawake ni ile hali ya kutowajali wanawake katika haki zao ama kwa kuwadhalilisha au hata kuwanyima haki zao za msingi na wakati mwingine kuwapiga na kuwanyima fursa ya kujiletea maendeleo. Hivyo dhamira hii ina athari kubwa tena mbaya kwa maisha ya wanawake kwani inapelekea kuwarudisha nyuma kimaendeleo na kuonekana ni watu tegemezi na wasioweza kutoa mchango wowote katika harakati mbalimbali za kimaendeleo, kama ilivyoelezwa na waandishi wawili wa vitabu teule.

Data zinazoonesha dhamira ya unyanyasaji wa wanawake kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.1.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili vyenye sifa tofauti kwa kutumia kiunganishi ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 134: **Tegemea alijaribu kujikinga kwa mikono. Na hilo ndilo lilikuwa kosa lake kubwa. Alishikwa mara moja na kutupwa chini kama gunia, miguu juu.**

Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imeweza kuibua dhamira ya unyanyasaji wa wanawake kwa kulinganisha vitu viwili tofauti kwa kutumia kiunganishi kwa

kulinganisha unyanyasaji aliokuwa akifanyiwa Tegemea na mumewe wa kupigwa na kutupwa chini umefananishwa na gunia.

Jedwali Na. 4.3.2.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kuipa sifa ya kibinadamu kitu kisicho na uwezo huo ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 18: **Mwaka wa kwanza nafikiri ulipita salama. Mambo yalianza mwaka wa pili alipokuwa darasa la kumi..** Data hii inaonesha matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kuupa mwaka uwezo wa kibinadamu wa kupita, hivyo data imedhihirisha unyanyasaji aliokuwa akifanyiwa Rukia kutoka kwa Manase hadi kupelekea kumbaki na kumtia mimba.

Jedwali Na. 4.3.9.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia maneno zaidi ya mara moja kwa lengo la kuisitiza jambo. Ukurasa wa 134: **Mimi siwezi kulima! Kama ni chakula mtaninyima! Tegemea alijibu. Utalima! Mimi nimesema siwezi! Nimesema utalima na utalima!** Data hii ya tamathali ya semi ya takriri imefanikisha kazi hii kwa kuibua dhamira ya unyanyasaji wa wanawake kwa kuyakariri maneno “utalima” na kuonesha namna baadhi ya waume wanavyowanyanyasa wake zao kwa kuwalazimisha jambo ambalo liko nje ya uwezo wake badala ya kutumia hekima na busara.

Data zinazoonesha dhamira ya unyanyasaji wa wanawake kama zilinyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n’kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.1.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili vyenye sifa tofauti kwa kutumia

kiunganishi ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 8: **Alifungua mlango taratibu, alipoingia ukumbini alimkuta Bwana Raza amekaa juu ya kiti amevimba kama kiboko.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imefanikisha kazi ya utafiti huu kwa kuonesha dhamira ya unyanyasaji wa wanawake kwa kulinganisha vitu viwili vilivyo tofauti kwa kulinganisha hasira za Bwana Raza dhidi ya mkewe Yasmin pale alipomlazimisha kuhama unguja na kuhamia Mombasa bila ya kumshauri.

Jedwali Na. 4.3.2.2 linaonesha data zilizokusanywa za tamathalia ya semi ya tashihisi kwa kuipa uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na uwezo huo ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 5: **Yasmin aliyapuza yote yale akageuza ubavu wa pili, mara usingizi ukamchukua.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imeweza kuibua dhamira ya unyanyasaji wa wanawake kwa kuipa usingizi uwezo wa kibinadamu wa kumchukuwa mtu na hivyo data inaonesha namna baadhi ya wanaume wanavyowalazimisha wake zao bila ya kuwataka ushauri wa jambo.

Jedwali Na. 4.3.4.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kutia chumvi. Ukurasa wa 7: **Ah! Babu we, unayajuwa maneno ya mume wangu tena akianza kusema hamalizi.** Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya unyanyasaji wa wanawake kwa kuyakuza maneno ya Bwana Raza kuwa akisema hanyamazi na hivyo data inaonesha namna baadhi ya wanaume hawawapi wake zao fursa ya kuwasikiliza wala kuzungumza.

Jedwali Na. 4.3.6.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tauria kwa kutumia maneno yenye tahajia moja ila maana zake ni tofauti. Ukurasa wa 6: **Alimwomba mumewe amrejeshe nyumbani lakini alikataa kata kata.** Data hii ya tamathali ya semi ya tauria imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya unyanyasaji wa wanawake kwa kutumia maneno ya tahajia moja ila yametumika kwa maana tofauti na kudhihirisha namna baadhi ya wanaume wanavyowalazimisha wake zao kubaki katika ndoa ilhali wao hawawataki.

Jedwali Na. 4.3.9.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia maneno zaidi ya mara moja kwa lengo la kusisitiza jambo fulani. Ukurasa wa 95: **Mimi sirudi, pendo jambo la hiari, hawawezi kunilazimisha kumpenda nisiyemtaka, Yasmin alisema, macho yake yashaanza kumbadilika machozi yanamlengalenga. Mimi sirudi! Sirudi! Sirudi ng'o.** data hii ya tamathali ya semi ya takriri imetoa dhamira ya unyanyasaji wa wanawake kwa kuyarudia rudia baadhi ya maneno ili kuonesha msisitizo. Hii ni dhamira inayoonesha namna baadhi ya wanaume wanavyowalazimisha wanawake kuolewa na mtu wasiemtaka.

Jedwali Na. 4.3.10.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini kwa kusisitiza jambo kwa maneno yenye ukinzani ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 12: **Bado yungali mgeni mjini Mombasa, si jirani wala muhisani, si mjomba wala shangazi, hana wa kumzulia angalau akapata kisingizio cha ruhusa.** Data hii ya tamatahali ya semi ya tabaini imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na

kuibua dhamira ya unyanyasaji wa wanawake kwa kutumia maneno yenye kukinzana na kutoa Atari wanazozipata wanawake wakati wakifungiwa ndani tu.

4.5.1.11 Dhamira ya Kufanya Kazi Kwa Bidii

Dhamira hii ya kufanya kazi kwa bidii imebuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n'kuvute* na kisha kuziorodhesha kwa njia ya majedwali matano. Kufanya kazi kwa bidii ni ile hali ya mtu au kikundi cha watu kujituma kikamilifu katika shughuli zao za kutafuta riziki za kila siku. Hivyo dhamira hii ina umuhimu mkubwa kwa maisha ya wanadamu na pia inasaidia kuleta maendeleo ya mtu binafsi, jamii na taifa kwa ujumla. Dhamira hii ya kufanya kazi kwa bidii kupitia tamathali za semi, mtafiti ameibaini kupitia riwaya ya *Vuta n'kuvute* tu kama data zinavyoonesha.

Data zinazoonesha dhamira ya kufanya kazi kwa bidii kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.1.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili vinavyotofautiana kwa kutumia kiunganishi ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 15: **Wachukuzi namba walimzonga kama nzi wanapouzongea mzoga, kila mmoja katika wachukuzi wale akitaka kujua mizigo ya Yasmin...** Data hii ya tamaathali ya semi ya tashibiha imeweza kuibua dhamira ya kufanya kazi kwa bidii kwa kulinganisha uzongaji wa wachukuzi wa kuwania kazi ni kama nzi wanapouzongea mzoga, hivyo data imeonesha dhamira ya kufanya kazi kwa bidii kwa maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.

Jedwali Na. 4.3.2.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na uwezo huo kwa lengo la kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 82: **Ukenda hapo utamkuta Bashiri yuko katikati ya mlima wa machungwa, yamemzunguka huku na huku.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imefanikisha kazi hii kwa kuibua dhamira ya kufanya kazi kwa bidii kwa kuyapa machungwa sifa ya kibinadamu ya kumzunguka muuzaji wakati hayana sifa hio na kuweza kuibua dhamira ya kufanya kazi kwa bidii kwa maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.

Jedwali Na. 4.3.4.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kutia chumvi. Ukurasa wa 82: **Ukenda huko utamkuta Bashiri katikati ya mlima wa machungwa yamemzunguka huku na huku.** Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya kufanya kazi kwa badii kwa kuikuza kazi ya kuuza machungwa kufikia mlima na hivyo data imehimiza watu kufanyakazi kwa bidii kwa maendeleo ya jamii.

Jedwali Na. 4.3.9.2 linaonesha data zilizokusanywa za tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia maneno zaidi ya mara moja kwa lengo la kusisitiza ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 228: **Mbele ya duka hilo amesimama muuza vibakuli vya bati, akipiga kelele kuvutia wanunuzi. Vyote shilingi vyote! Vyote shilingi vyote! Kimoja naongeza, ameshika vibakuli vinne mkononi.** Data hii ya tamathali ya semi ya takriri imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti

huu na kuibua dhamira ya kufanya kazi kwa bidii kwa kuyarudia rudia maneno zaidi ya mara moja na kudhihirisha umuhimu wa kufanya kazi kwa bidii kwa maendeleo ya jamii.

Jedwali Na. 4.3.10.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini kwa kusisitiza jambo kwa kutumia maneno yenye ukinzani kwa lengo la kusisitiza jambo. Ukurasa wa 156: **Humo mlikuwa mmejaa watu, kelele, hakuna anayesikilizana na mwenzake. Wahudumiaji wanakwenda na kurudi sahani wamezibeba mikononi.** Data hii ya tamathali ya semi ya tabaini imeweza kuibua dhamira ya kufanya kazi kwa bidii kwa kusisitiza jambo la kufanya kazi kwa bidii kwa kutumia maneno yanayokinzana kwa kusema wahudumiaji wanakwenda na kurudi.

4.5.1.12 Dhamira ya Usaliti

Dhamira hii ya usaliti imeibuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute* na kisha kuziorodhesha kwa njia ya majedwali saba. Usaliti ni ile hali ya mtu au kikundi cha watu walio katika jamii moja, akawa mtu huyo au kikundi cha watu kwenda kinyume na wenziwao kwa jambo ambalo wamekubaliana. Hivyo dhamira hii ina athari kubwa tena mbaya kwa maisha ya wanajamii kwani inapelekea kuwarudisha nyuma kimaendeleo na kusababisha kuwepo mivutano na migongano ndani ya jamii. Dhamira hii ya usaliti imeweza kuonekana kutoka katika riwaya moja tu ya *Vuta n'kuvute* kupitia data za tamathali ya semi zilizokusanywa.

Data zinazoonesha dhamira ya usaliti kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.1.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili vilivyo tofauti kwa kutumia kiunganishi ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 62: **Jasho linamtoka, anapuma kama ng'ombe anayeburura gari...** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imeweza kuibua dhamira ya usaliti kwa kulinganisha upumaji wa Koplo Matata na ng'ombe anayeburura gari na hivyo data imeweza kuonesha namna baadhi ya wananchi walivyokuwa wakiwasaliti wananchi wenzao kwa maslahi ya wakoloni.

Jedwali Na. 4.3.2.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na uwezo huo kwa lengo la kufikisha ujumbe. Ukurasa wa 35: **Macho yote yameingia ndani, amefuga sharafa la ndevu nazo zimechanganyika nyeusi na nyeupe hujui zipi zinataka kumtawala mwenzake.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya usaliti kwa kuipa sharafa la ndevu uwezo wa kibinadamu wa kumtawala mtu na kuonesha namna usaliti unavyomfanya mtu ashindwe hata kujishughulikia kwenye mambo ya usafi baada ya Bwana Raza kusalitiwa na mkewe Yasmin.

Jedwali Na. 4.3.4.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kutia chumvi. Ukurasa wa 65: **Alivuma nchi nzima kwa ukali wake uliochanganyika na utovu wa huruma.** Data hii inaonesha matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha jinsi ilivyoweza kutoa dhamira ya usaliti kwa kuukuza ukali wa Koplo Matata kuwa

ulienea nchi nzima na hili limetokana namna Koplo Matata alivyokuwa akishirikiana na wakoloni dhidi ya wananchi wenzake.

Jedwali Na. 4.3.7.2 linaonesha matumizi ya tamathali ya semi ya shitizai kwa kutumia maneno ynye kuleta iliyokinyume na ile iliyokusudiwa au kinyume na ukweli ulivyo. Ukurasa wa 66: **Lakini itayumkinika. Hivyo wanawake wale wasiojua chochote wataweza kunishinda mimi kwa akili?** Data hii ya tamathali ya semi ya shitizai imeweza kuibua dhamira ya usaliti kwa kuonesha wanawake hawawezi kumshinda Koplo Matata msaliti ambapo ni kinyume na uhalisia.

Jedwali Na. 4.3.9.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia baadhi ya maneno zaidi ya mara moja ili kuisisitiza ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 143: **Koplo Matata akaanza kulalamika. Mwanamke wewe! Mwanamke wewe! Sitokusahau maisha yangu! Umenifukuzisha kazi!** Data hii ya taamthali ya semi ya takriri imeweza kuibua dhamira ya usaliti kwa kuyarudia maneno ya Koplo Matata “Mwanamke wewe!” na hivyo kuonesha namna athari ya usaliti hupelekea maangamizi kwa mfanyaji au anayefanyiwa.

Jedwali Na. 4.3.10.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini kwa kuisisitiza jambo kwa kutumia maneno ya ukinzani kwa lengo la kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 58: **Ah! Mambo makubwa haya. Naona ananiuliza mambo nisyoyajua mbele wala nyuma.** Data hii ya tamathali ya semi ya tabaini imeweza kuibua dhamira ya usaliti kwa kutumia maneno yenye kuisisitiza mambo yanayofanyiwa na wasaliti kwa kuwatumikia wakoloni na

kuwauliza maswali wananchi yasitoeleweka, pale aliposema Mwajuma “ananiuliza mambo nisyoyajua mbele wala nyuma”.

4.5.1.13 Dhamira ya Malezi Mabaya kwa Watoto

Dhamira hii ya malezi mabaya kwa watoto imeibuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n’kuvute* na kisha kuziorodhesha kwa njia ya majedwali tisa. Malezi mabaya kwa watoto ni hali ya kuwalea watoto kwa misingi isiyokubalika na jamii husika au na hata kutojali haki zao katika malezi wakiwa kama watoto. Hivyo dhamira hii ina athari kubwa tena mbaya kwa maisha ya watoto ya kipindi cha utoto wao hadi kuwa wakubwa kwani huwafanya wakose mambo ya msingi katika vipindi hivyo, kama ilivyoelezwa na waandishi wawili wa vitabu teule.

Data zinazoonesha dhamira ya malezi mabaya kwa watoto kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.2.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihishi kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na uwezo ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. ukurasa wa 124: **Kwa hiyo mtu anaamini kwamba Mungu yupo ni yule aamuaye kwa kufuata milango ya fahamu zake. Kwake fahamu zinatawala bongo.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashihishi imeweza kuibua dhamira ya malezi mabaya kwa watoto kwa kuzipa fahamu uwezo wa kutawala na kuweza kuonesha namna ya athari za baadhi ya wazazi ya kuwapa watoto wao elimu ya upande mmoja tu (sekula) na mwishoe kuwafanya wasiamini kama Mungu yupo.

Jedwali Na. 4.3.6.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tauria kwa kutumia maneno ya tahajia moja lakini maana zake ni tofauti kwa lengo la kuipamba kazi ya fasihi. Ukurasa wa 91: **Vua nguo! Baba alisema. Nihurumie sitarudia tena! Kalia alilia.** Data hii ya tamathali ya semi ya tauria imeweza kuibua dhamira ya malezi mabaya kwa watoto kwa kutumia maneno yenye tahajia moja lakini maana zake ni tofauti “Kalia alilia” na hivyo kuweza kuonesha namna malezi ya nguvu na vitisho kwa watoto hayasaidii bali njia bora ya malezi kwa watoto ni kuwaelimisha ubaya na uzuri wa jambo.

Jedwali Na. 4.3.7.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya shitizai kwa kukusudia kuleta maneno yenye maana iliyo kinyume na ile iliyokusudiwa ama kinyume na ukweli ulivyo. Ukurasa wa 57: **Mimi nimesikia saba na ametiwa mimba hiyo na kijana fulani mchafu mchafu. Sijui wasichana hawana macho?** Data hii ya tamathali ya semi ya shitizai imeweza kuibua dhamira ya malezi mabaya kwa watoto kwa kutumia maneno yenye kuonesha maana iliyo kinyume “sijui wasichana hawana macho” na hivyo kudhihirisha namna malezi mabaya yanavyopelekea wasichana kupata mimba hata kwa watu wasio na hadhi katika jamii.

Jedwali Na. 4.3.9.1 linaonesha data zilizokusanywa za tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia baadhi ya maneno zaidi ya mara moja kwa lengo la kusisitiza jambo. Ukurasa wa 51: **Mnazungumza na mwehu! Alisema kwa kelele. A! anasema hakuna Mungu. Hakuna Mungu! Mtoto wa nani? Mababu na mababu wamekwenda; wamechukuliwa na nani?** Data hii ya tamathali ya semi ya takriri imeweza kuibua dhamira ya malezi mabaya kwa watoto kwa kuyarudia rudia

“anasema hakuna Mungu. Hakuna Mungu!” ambapo dhamira hii imeweza kuonesha namna athari ya baadhi ya wazazi ya kuwalea watoto wao katika malezi yasiojali mambo ya dini na mwishowe kupelekea hata kudai hakuna Mungu kabisa.

Data za dhamira ya malezi mabaya kwa watoto kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n’kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.1.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwakulinganisha vitu viwili tofauti kwa kutumia kiunganishi kwa lengo la kuipambakazi ya fasihi na kufikisha ujumbe kwa jamii. Ukurasa wa 16: **Majirani walikwishajaa madirishani wanamwangalia Yasmin akitoka na kikapu chake mkononi, amenywea kama aliyemwagiwa maji ya baridi.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imeweza kuibua dhamira ya malezi mabaya kwa watoto ambapo dhamira inaonesha athari ya baadhi ya wazazi kuwalazimisha watoto wao kuolewa na mtu asiyempenda.

Jedwali Na. 4.3.3.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya sitiari kwa kuhusisha vitu viwili vyenye tabia na maumbile tofauti ili kuleta uhamisho wa kimaana bila ya kutumia kiunganishi. Ukurasa wa 39: **Amekuwa mfa maji kamili.** Data hii ya tamatathali ya semi ya sitiari imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya malezi mabaya kwa watoto iliosababishwa na wazazi wa Yasmin kumlazimisha kuolewa na mtu asiemtaka kwa kulinganisha maisha ya Yasmin na mtu aliekufa maji na kuweza kuleta uhamisho wa kimaana wa kuhangaika na maisha.

Jedwali Na. 4.3.6.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tauria kwa kutumia maneno yenye tahajia moja lakini yametofautiana kimaana. Ukurasa wa 19: **Hivi sasa Yasmin alikabiliwa na maisha mapya kabisa, maisha ambayo hakupata kuishi kwani ijapokuwa alikuwa akiishi Ng'ambu, lakini alikuwa haishi king'ambu.** Data hii ya tamathali ya semi ya tauria imeweza kuibua dhamira ya malezi mabaya kwa watoto kwa kutumia maneno ya tahajia moja lakini yametofautiana kimaana na kuweza kuonesha athari inayopatikana kwa mtu atakaewalazimisha suala la ndoa watoto wake kwa wasiompanda.

Jedwali Na. 4.3.9.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia baadhi ya maneno zaidi ya mara moja ili kusisitiza ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 38: **Nasema veve siku hizi nafatana na golo. Toka! Toka kwenda zako! Mimi sitaki ona hata uso yako.** Data hii ya tamathali ya semi ya takriri imeweza kuibua dhamira ya malezi mabaya kwa watoto kwa kuyarudia rudia baadhi ya maneno zaidi ya mara moja “toka! Toka!” kwa lengo la kusisitiza jambo ambapo atahri ya kuwalazimisha watoto kuolewa na mtu wasiemtaka kunapelekea chuki baina ya wazazi na watoto wao.

Jedwali Na. 4.3.10.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini kwa kutumia maneno yenye kusisitiza jambo kwa kutumia maneno yenye ukinzani ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 206: Mara tu baada ya mume wangu kufa. **Denge niliyempanda, nikategemea kuishi naye akachukuliwa. Si wangu. Hapa nilipo nipo hohe, hahe sina mbele, sina nyuma, siko kwake siko kwangu. Nadhani nataabishwa na radhi za wazazi wangu.** Data hii ya tamathali ya semi ya tabaini imeweza kufanikisha kazi ya utafiti huu kwa

kuibua dhamira ya malezi mabaya kwa watoto kwa kutumia maneno ya ukinzani pale aliposema “sina mbele, sina nyuma, siko kwake siko kwangu” na hivyo kudhihirisha namna ya malezi mabaya yanavyowaathiri watoto na hata kudhani kuwa hawana radhi za wazazi wao.

4.5.1.14 Dhamira ya Ujasiri na Ushujaa

Dhamira hii ya ujasiri na ushujaa imeibuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n’kuvute* na kisha kuziorodhesha kwa njia ya majedwali sita. Ujasiri na ushujaa ni ile hali ya mtu au kikundi cha watu kujitolea katika kutetea haki zao au za wengine pasina kumuogopa wala kumjali mtu yeyote. Hivyo dhamira hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya mtu binafsi na taifa kwa ujumla kwani inapelekea kupatikana kwa haki ndani ya jamii na kukomesha dhulma, kama ilivyoelezwa na waandishi wawili wa vitabu teule.

Data zinazoonesha dhamira ya ujasiri na ushujaa kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.6.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tauria kwa kutumia maneno yenye tahajia moja lakini maana ya maneno hayo huwa ni tofauti. Ukurasa wa 111: **Aliomba toba lakini mwanamke hakumwacha mpaka majirani walipokuja. Wakamkuta Kalia! Macho mekundu, analia kama beberu.** Data hii ya tamathali ya semi ya tauria imeweza kuibua dhamira ya ujasiri na ushujaa kwa kutumia maneno ya tahajia moja lakini maana zake ni tofauti pale aliposema “Kalia! Macho mekundu, analia” na

kudhihirisha ujasiri na ushujaa uliofanywa na mwanamke ambaye alijiokoa kwa kumshika sehemu za chini za Kalia wakati alipotaka kumbaka.

Data zinazoonesha dhamira ya ujasiri na ushujaa kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.1.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili vyenye sifa tofauti kwa kutumia kiunganishi ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 170: **Aliwekwa katikati ya askari wawili wote wamekasirika nyuso wamezikunja kama waliomeza shubiri.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imeweza kuibua dhamira ya ujasiri na ushujaa kwa kulinganisha kukunjwa kwa nyuso za askari na umezaji shubiri kwa kutumia kiunganishi kama na hivyo kuweza kutoa umuhimu wa ushujaa na ujasiri katika harakati za kupambana na wakoloni kwa lengo la kupata uhuru.

Jedwali Na. 4.3.2.2 linaonesha matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na uwezo huo ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 241: **Alinyanyuka alipachika bunduki yake begani na kuelekea pale kichakani, lakini alipofika alikuta mti mkavu umevaa kofia, hauna wasiwasi umetulia vilevile, Denge ametoweka.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imeweza kuibua dhamira ya ujasiri na ushujaa kwa kuupa mti uwezo wa kibinadamu wa kuvaa kofia na kudhihirisha ujasiri na ushujaa uliooneshwa na wapigania mapinduzi kwa kumtorosha mwenzao gerezani.

Jedwali Na. 4.3.5.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tafsida kwa kupunguza ukali wa maneno. Ukurasa wa 118: **Ndo maana na**

sisi tumeazimia kwenda huko kustarehe pamoja nao. Data hii ya tamathali ya semi ya tafsida imefanikisha kazi ya mtafiti kwa kuibua dhamira ya ujasiri na ushujaa kwa kupunguza ukali wa maneno pale aliposema “kwenda huko kustarehe pamoja nao” na kuonesha ujasiri na ushujaa uliofanywa na kikundi cha ripua ripua kwenye ukumbi wa Karimjee wakati wakoloni wakistarehe.

Jedwali Na. 4.3.6.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali za semi ya tauria kwa kutumia maneno yenye tahajia moja lakini maana zake ni tofauti. Ukurasa wa 38: **Ah, haidhuru nitaishi hivyo hivyo yache maji yafuate mkondo na upepo uvume utakapo kwani wangapi wenye dhiki. Mwisho wa dhiki si dhiki ni faraja tu.** Data hii ya tamathali ya semi ya tauria imeweza kuibua dhamira ya ujasiri na ushujaa kwa kutumia neno lenye tahajia moja (dhiki) likiwa na maana tofauti ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa kuonesha ujasiri uliofanywa na Yasmin wa kukataa kuolewa na mtu asiempenda.

Jedwali Na. 4.3.10.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini kwa kusisitiza jambo kwa kutumia maneno yenye ukinzani. Ukurasa wa 133: **Kwa ule wasiwasi wake iliomfanya mara akae, mara asimame, mara aende mara arudi, ile suruali yake ndefu ya kijivujivu haikuweza kutulia vyema kiunoni na mara kwa mara ilimbidi aivutevute kuiweka sawa.** Data hii ya tamathali ya semi ya tabaini imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya ujasiri na ushujaa kwa kutumia maneno yanayokinzana pale aliposema “wasiwasi wake iliomfanya mara akae, mara asimame, mara aende mara arudi, na kuweza kuonesha ujasiri pamoja na ushujaa uliooneshwa na wanaharakati wa kudai uhuru ulivyowatia wasiwasi wakoloni.

4.5.1.15 Dhamira ya Wivu wa Kupindukia

Dhamira hii ya wivu wa kupindukia imeibuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute* na kisha kuziorodhesha kwa njia ya majedwali manne. Wivu wa kupindukia ni ile hali ya mtu kumpenda sana mpenzi wake katika hali ya kuwa na wasi wasi juu ya kila jambo analolifanya asijekuwa analifanya kwa ajili ya mtu mwengine na hasa kwa wanaume dhidi ya wanawake. Hivyo dhamira hii ina athari kubwa tena mbaya kwa maisha ya wapendanao hasa wanawake kwani inapelekea kuwarudisha nyuma kimaendeleo na kuonekana ni watu tegemezi tu na wasioweza kutoa mchango wowote wala kushiriki katika harakati zozote za kimaendeleo, kama ilivyoelezwa na mwandishi mmoja wa *Vuta n'kuvute*.

Data zinazoonesha dhamira ya wivu wa kupindukia kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.1.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashibiha kwa kulinganisha vitu viwili vyenye sifa tofauti kwa kutumia kiunganishi ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 175: **Alikuwa hendi harudi, yumo ndani tu kama kizuka, kwa sababu ya wivu aliokuwa nao Shihabu.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashibiha imeweza kuibua dhamira ya wivu wa kupindukia kwa kulinganisha kuwekwa ndani na kizuka na kuweza kuonosha namna baadhi ya wanaume walivyokuwa na wivu kisi cha kuwanyima wanawake baadhi ya haki zao.

Jedwali Na. 4.3.3.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya sitiari kwa kulinganisha vitu viwili bila ya kiunganishi na kuleta uhamisho

wa kimaana. Ukurasa wa 175: **Sasa amenasa ni mahabusu wake, si huru tena wa kwenda apendako.** Data hii ya tamathali ya semi ya sitiari imeweza kuibua dhamira ya wivu wa kupindukia kwa kulinganisha uwekwaji ndani na umahabusu na hivyo kudhihirisha namna athari za baadhi ya wanaume wenye wivu kwa wake zao.

Jedwali Na. 4.3.9.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumiza ya tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia baadhi ya maneno zaidi ya mara moja ili kuisitiza alilokusudia. Ukurasa wa 191: **Shihabu alitoka mbio pale alipokuwa amesimama akataka kujitosa kule moto unakoripuka, zima moto wakamzuia, hataki kushikwa anapigana nao kama mtu aliyechagawa, anapiga kelele, mke wangu weee! Mke wangu weee! Hapana aliyesalimika katika ajali ile.**

Data hii ya tamathali ya semi ya takriri imeweza kuibua dhamira ya wivu wa kupindukia kwa kuyarudia maneno zaidi ya mara moja na hivyo kuweza kutoa ujumbe unaowataka wanaume waache tabia ya wivu wa kupindukia kwani huleta madhara kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Jedwali Na. 4.3.10.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali za semi ya tabaini kwa kutumia maneno yenye ukinzani wakati wa kuisitiza jambo. Ukurasa wa 164: **Denge alikuwa na hisia za kutatanisha baada ya kusoma barua ile. Alihuzunika kwa kumkosa Yasmin na alifurahi kuwa Yasmin amepata mtu wa kumstiri.** Data hii ya tamathali ya semi ya tabaini imeweza kuibua dhamira ya wivu uliopindukia kwa kuonesha namna Denge alipoingia wivu kwa kumkosa Yasmin na wakati huo huo akifurahi kwa kuwa Yasmin ameolewa.

4.5.1.16 Dhamira ya Upendo

Dhamira hii ya upendo imeibuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n'kuvute* na kisha kuziorodhesha kwa njia ya majedwali kumi na mbili. Upendo ni ile hali yakuwanayo mtu kwa kumjali mpenzi wake au hata mtu wake wa karibu kama mzazi kwa mwanawe na kuonesha jinsi gani yuko tayari kufanya lolote kwa ajili yake. Hivyo dhamira hii ina umuhimu mkubwa kwa wapendanao kwani inapelekea watu hao kuishi kwa amani na furaha na daima hawako tayari kuona madhara yakitokea baina yao, kama ilivyoenezwa na waandishi wawili wa vitabu teule.

Data zinazoonisha dhamira ya upendo kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.2.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa kitu uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na uwezo huo ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 131: **Nilipofika Chuo Kikuu barua ya Sabina niliikuta kweli imeningoja.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imeweza kuibua dhamira ya upendo kwa kuzipa barua uwezo wa kibinadamu wa kumngojea mtu na hivyo data imedhihirisha namna upendo unavyowafanya watu wakumbukane hata kwa barua.

Jedwali Na. 4.3.3.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya sitiari kwa kulinganisha vitu viwili tofauti bila ya kutumia kiunganishi. Ukurasa wa 127: **Hata! Mke wa mwizi ni mwizi, mke wa mlevi ni mlevi. Manase alisema.** Data hii ya tamathali ya semi ya sitiari imeweza kuibua dhamira ya upendo

kwa kuonesha namna mtu anavyofanana na Yule anayempenda hata kama atakuwa na tabia mbaya.

Jedwali Na. 4.3.4.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kutia chumvi.

Ukurasa wa 46: **Bado hajajifungua? Aliuliza Matlida kwa sauti. Bado. Labda atazaa mapacha. Nilimwona majuma mawili yaliyopita. Tumbo lilikuwa kubwa.**

Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imeweza kufanikisha kazi ya utafiti kwa kuibua dhamira ya upendo kwa wapendanao kwa kuyakuza maneno kuliko vile yalivyo na kuonesha mapenzi walionayo majiran hao hadi kuoneana huruma kwa kuchelewa kujifungua.

Jedwali Na. 4.3.6.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tauria kwa kutumia maneno yenye tahajia moja lakini maana ya maneno hayo ni tofauti. Ukurasa wa 105: **Ebu sema tena nikusikie, alisema Tabia,**

nilimwambia. Tabia, tabia yangu unaiona nzuri; mbona mimi nina kiburi sana.

Data hii ya tamathali ya semi ya tauria imefanikisha kazi ya utafiti kwa kuibua dhamira ya upendo kwa kutumia neno la “tabia” likiwa kama ni jina la mtu na wakati huo huo likitumika kama mwenendo na hivyo kuweza kudhihirisha namna wapendanao wanavyojaliana katika mambo yao.

Jedwali Na. 4.3.8.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya dhahaka kwa kutumia maneno yenye kumuweka mtu katika hali ya uduni kupita kiasi. Ukurasa wa 104: **Njiani tukirudi Sabina alisema, sikuamini kwamba**

na wewe utaweza siku moja kuwa mtu mzima. Data hii ya tamathali ya semi ya

dhihaka imeweza kuibua dhamira ya upendo kwa wapendanao kwa kuonesha upendo wa Sabina kwa Kazimoto hadi kumfanyia utani ndani ya mapenzi yao.

Jedwali Na. 4.3.9.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia maneno zaidi ya mara moja kwa lengo la kuisitiza ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 41: **Matlida alitupa shoka chini aliponiona. Karibu! Karibu! Alipiga kelele.** Data hii inaonesha matumizi ya tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia zaidi ya mara moja mamneno ya kumkaribisha mtu huku yakionesha namna upendo kwa majirani.

Data zinazoonesha dhamira ya upendo kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.2.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na uwezo huo ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 55: **Lakini mara tu baada ya sauti za ala za tarabu kuwasili ndani ya masikio yao.** Data hii ya matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi imeweza kuibua dhamira ya upendo kwa kuzipa sauti za ala za tarabu kuwasili ambapo ni sifa ya kibinadamu na hivyo kuweza kudhihirisha upendo walionao baadhi ya watu wa kupenda zaidi muziki wa tarabu.

Jedwali Na. 4.3.3.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya sitiari kwa kulinganisha vitu viwili vyenye sifa tofauti na kuleta uhamisho wa kimaana. Ukurasa wa 217: **Yule askari aliyekuja kumfungulia alimwona ni mkombozi aliyemkomboa kutoka jahanamu.** Data hii ya tamathali ya semi ya sitiari imeweza kuibua dhamira ya upendo kwa wapendanao kwa kulinganisha

mateso ya gerezani na moto wa jahannamu na hivyo data imeonesha upendo walionao baadhi ya askari kwa wafungwa.

Jedwali Na. 4.3.4.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kutia chumvi. Ukurasa wa 218: **Nafikiri ingelikuwa kila ninayemnyoa namtoza pesa, basi ningelikuwa milionea sasa.** Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imeweza kuibua dhamira ya upendo kwa wapendanao kwa kutia chumvi na kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kuonesha namna wafungwa walivyokuwa na mapenzi ya wenyewe kwa wenyewe hadi kudiriki kusaidiana mambo yao bila ya pesa.

Jedwali Na. 4.3.6.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tauria kwa kutumia maneno yenye tahajia moja lakini maana zake nitofauti. Ukurasa wa 75: **Hakuacha kumweleza jinsi Yasmin alivyopotoka na kumnasihi atafute mwengine miongoni mwa mabanati waliotelewa wakaleleka, waliofunzwa wakafunzika, waliotunzwa wakajitunza.** Data hii ya tamathali ya semi ya tauria imeweza kuibua dhamira ya mapenzi kwa kutumia maneno ya tahajia moja lakini yakaleta maana tofauti na neno la kwanza na hivyo kudhihirisha namna baadhi ya watu walikuwa na mapenzi makubwa ya wapenzi wao hata kama wao hawatakiwi.

Jedwali Na. 4.3.9.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia maneno zaidi ya mara moja ili kusisitiza jambo alilolikusudia. Ukurasa wa 17: **Sina shauri lolote, nimekuja kwako kukusikiliza utaniambia nini. Tafadhali nisitiri, nisitiri aibu yangu.** Data hii ya tamathali ya

semi ya takriri imefanikisha kazi hii kwa kuweza kuibua dhamira ya upendo kwa wapendanao kwa kulirudia zaidi ya mara moja “tafadhali nisitiri” na hivyo kuweza kuonesha namna upendo uliopo kwa baadhi ya majirani.

Jedwali Na. 4.3.10.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini kwa kusisitiza jambo kwa kutumia maneno ya ukinzani ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 165: **Denge alimtazama Mambo akatikisa kichwa, akitoa ishara ya kutokubaliana naye. Mwanamke, alisema, mwanamke si kitu cha kunyang’anya au kunyang’anywa. Si kitu cha kunyang’anyiana.** Data hii ya tamathali ya semi ya tabaini imeweza kufanikisha kazi ya utafiti huu kwa kuibua dhamira ya upendo kwa wanawake kwa kutumia maneno yanayokinzana na hivyo kudhihirisha namna baadhi ya watu wasiojua thamani ya kupenda au kupendwa na wanawake.

4.5.1.17 Dhamira ya Imani za Kidini

Dhamira hii ya imani za kidini imeibuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na kuziorodhesha kwa njia ya jedwali moja. Imani ya kidini ni ile hali ya mtu kuwa na itikadi katika moyo wake kwa kuamini na kufuata mwenendo unaoongozwa na itikadi za kiroho, na vile vile kwa imani hiyo mtu huyo huwa yuko tayari kufanya jambo lolote kwa muongozo wa imani hiyo. Hivyo dhamira hii ina athari kubwa na mchango mkubwa katika kumlea mtu kiroho.

Data zinazoonesha dhamira ya chuki na uhasama kama zilizo rodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.11.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi yz tamathali za semi ya msisitizo bayani kwa kuingiza maneno yanayotumika kwa kuonesha ushindani wa mawazo. Ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe ulikusudiwa. Ukurasa wa 73: **Leo nimeota ndoto ya ajabu, alisema tena. Ulikuwa na mwanamke? Hata! Nimeota nikiwa mbinguni. Sema kweli! Kabisa!** Data hii ya tamathali ya semi ya msisitizo bayani imeweza kufanikisha kazi ya utafiti huu kwa kuibua dhamira ya imani ya kidini kwa kutumia maneno yanayoonesha ushindani wa mawazo pale aliposema “nimeota nikiwa mbinguni. Sema kweli!” hivyo dhamira inaonesha watu watafika mbinguni ikiwa na matendo mema.

4.5.1.18 Dhamira ya Upendo kwa Viumbe Hai

Dhamira hii ya upendo kwa viumbe hai imeibuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n’kuvute* na kisha kuziorodhesha kwa njia ya majedwali matatu. Upendo kwa viumbe hai ni ile hali ya mtu kupatwa na hisia na huruma kwa viumbe hai kwa kuwajali katika maisha yao na hata kuzisimamia katika haki zao. Hivyo dhamira hii ni muhimu sana kwa maisha ya wanadamu pamoja na kushirikiana na viumbe wengine.

Data zinazoonesha dhamira ya upendo kwa viumbe hai kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.2.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa kitu sifa au uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na uwezo huo ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 78: **Nilipotazama chini**

juu ya jiwe niliona mijusi wakiota jua nao walinisalimu kwa kutingisha vichwa.

Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imeweza kufanikisha kazi ya utafiti huu kwa kuibua dhamira ya upendo kwa viumbe hai kwa kuwapa mijusi uweza wa kibinadamu wa kusalimia kwa kutingisha vichwa, hivyo data imeweza kuonesha namna ya umuhimu wa kuwaonea huruma baadhi ya viumbe hai wengine.

Jedwali Na. 4.3.4.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kutia chumvi.

Ukurasa wa 79: **Nilijiona kwamba nilikuwa na uwezo wa kuokoa maisha yake kwa tendo moja dogo tu ambalo lilikuwa halihitaji hata tone moja la jasho.**

Nilijiona mungu mdogo. Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imeweza kutoa dhamira ya upendo kwa viumbe hai kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kuonesha namna Kazimoto alivyoweza kumuokoa nyuki na kujiona kafanya jambo kubwa kama mungu.

Data za dhamira ya upendo kwa viumbe hai kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.2.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa kitu sifa ya kibinzdamu kitu kisicho na sifa hio kwa lengo la kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 237: **Wale wafungwa walikuwa wanavishukuru vile vichaka vilivyowafadhili kivuli kizuri**

kilichowanusuru na jua kali... Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imeweza kuibua dhamira ya upendo kwa viumbe hai kwa kuvipa vichaka uwezo wa

kibinadamu wa kuwafadhili watu vivuli na kuonesha namna ilivyokuwa ni muhimu sana kupanda miti kwa ajili ya matunda na vivuli.

4.5.1.19 Dhamira ya Umuhimu wa Ndoa

Dhamira hii ya umuhimu wa ndoa imeibuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n'kuvute* na kisha kuziorodhesha kwa njia ya majedwali matatu. Kwa mujibu wa BAKWATA (1996). Ndoa ni mkataba wa kuishi pamoja kati ya mwanamme na mwanamke (mume na mke) kwa kufuata utaratibu uliowekwa na jamii. Hivyo dhamira hii ni muhimu sana kwa maisha ya wanadamu kwani hupelekea kupata heshima kwa jamii nzima.

Data zinazoonesha dhamira ya umuhimu wa ndoa kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.7.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya shitizai kwa kutumia maneno yenye kuleta maana iliyo kinyume na ile iliyokusudiwa ama kinyume na ukweli ulivyo. Ukurasa wa 140: **Usemayo ni kweli, lakini ninavyoamini mimi mwanamume asipooa akili zake pia zinakwenda tenge kidogo.** Data hii ya tamathali ya semi ya shitizai imeweza kuibua dhamira ya umuhimu wa ndoa kwa kuleta maneno yaliyo kinyume na maana iliyokusudiwa kwa kuwashusha hadhi wanaume wasiooa na kuwaona akili zao ni tenge na hivyo data imeonesha umuhimu wa jambo hili la ndoa.

Data zinazoonesha dhamira ya umuhimu wa ndoa kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.7.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya shitizai kwa kutumia maneno yenye kuleta maana iliyo kinyume na ile iliyokusudiwa ama kinyume na ukweli ulivyo. Ukurasa wa 227: **Mke ni mwenzako katika safari ya maisha. Raha na furaha, shida na msiba, dhiki na taabu, mke sio unakwenda kulichukua kurumbembe limeota mbawa unaliweka ndani ya nyumba halafu unasema ati una mke.** Data hii ya tamathali ya semi ya shitizai imeweza kuibua dhamira ya umuhimu wa ndoa kwa kuleta maneno yaliyo kinyume na maana iliyokusudiwa kwa kuonesha umuhimu wa kuoia wanawake wenye tabia nzuri na kuachana na wanawake wa mitaani wasio na malezi bora.

Jedwali Na. 4.3.9.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia maneno zaidi ya mara moja kwa lengo la kuisitiza ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 74: **Alimfikiri Raza na kumuona kama mwendawazimu au labda mtu aliyepumbaa kwani watoto wazuri wote waliojaa katika jiji la Mombasa, yeye hakuona isipokuwa Yasmin. Yasmin, Yasmin, Yasmin gani naye?** Data hii ya tamathali ya semi ya takriri imeweza kuibua dhamira ya umuhimu wa ndoa kwa kuyarudia rudia baadhi ya maneno zaidi ya mara moja kwa kuonesha msisitizo wa mtu kuona mwanamke mwenye mapenzi na atakaeweza kuishi naye kwa raha na shida.

4.5.1.20 Dhamira ya Uasharati

Dhamira hii ya uasharati imeibuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n'kuvute* na kisha kuziorodhesha kwa njia ya majedwali kumi na moja. Uasharati ni hali ya mtu mwanamme au mwanamke kushiriki / kufanya masuala ya ngono bila ya

misingi inayokubalika na wazazi au iliyowekwa na jamii kwa ujumla. Hivyo dhamira hii ina athari kubwa ilio mbaya kwa jamii, kwani huodoa heshima na kupunguza hadhi ya utu kwa wanajamii.

Data zinazoonesha dhamira ya uasharati kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.2.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na uwezo huo ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 102: **Shetani naye ana bahati nzuri, kwani ninafikiri kwamba wanawake wazuri wengi huenda motoni na shetani huwafaidi. Siku ilijileta wenyewe.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kuipa siku uweza wa kibinadamu wa kujileta wenyewe na kufanikiwa kuonesha namna vijana wanavyoshiriki mambo ya uasharati na kisha kusingizia kwamba hio kwao ni bahati njema.

Jedwali Na. 4.3.3.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ta semi ya sitiari kwa kulinganisha vitu viwili vyenye sifa tofauti na kuleta uhamisho wa kimaana. Ukurasa wa 37: **Huu ni ugonjwa unaoletwa na vijana.** Data hii ya tamathali ya semi ya sitiari imefanikiwa kuibua dhamira ya uasharati kwa kulinganisha mambo ya uasharati unaofanya na vijana ni sawa na ugonjwa na kuonesha namna ulivyoenea na kuwaambukiza vijana wengi.

Jedwali Na. 4.3.5.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tafsida kwa kutumia maneno yenye kupunguza ukali wake au hata kuficha matusi. Ukurasa wa 20: **Alifika hata hatua ya kutumia nguvu! Na kweli alitumia**

nguvu bila ya utashi wangu. Data hii ya tamathali ya semi ya tafsida imeweza kuibua dhamira ya uasharati kwa kuficha matusi kwa pale aliposema “alitungia nguvu bila ya utashi wangu” na hivyo dhamira imeonesha namna baadhi ya wanaume wanavyoendekeza uasharati na kukurubia hata kuwabaka wasichana wadogo.

Jedwali Na. 4.3.7.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya shitizai kwa kutumia maneno yenye maana iliyo kinyume na ile iliyokusudiwa au kinyume na ukweli ulivyo. Ukurasa wa 54: **Kwa nini hawawezi kumwoza? Hajapata mchumba. Nani taoa makapi.** Data hii ya tamathali ya semi ya shitizai imeweza kutoa dhamira ya uasharati kwa kuyatumia maneno yaliyokinyume na maana iliyokusudiwa kwa kumkejeli mwanamke mwenye tabia ya uasharati na kumwita makapi.

Jedwali Na. 4.3.8.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya dhihaki kwa kutumia maneno yenye kuonesha dharau kwa lengo la kumuweka mtu katika hali duni kupita kiasi kwa njia ya mafumbo. Ukurasa wa 72: **Wanaume wawili bado mnamtembea na fimbo; woga gani huo!** Data hii ya tamathali ya semi ya dhihaki imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya uasharati kwa kutumia maneno ya dharau juu ya wanaume wawili waliokuwa wakimwendea mwanamke kwa ajili ya uasharati.

Jedwali Na. 4.3.9.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia baadhi ya maneno zaidi ya mara moja ili kutoa msisitizo wa jambo. Ukurasa wa 4: **Mambo waliyosema yalikuwa mengi. Mara**

kucheka, mara mimi sitaki, na mara huniamini. Data hii ya tamathali ya semi ya takriri imeweza kutoa dhamira ya uasharati kwa kulirudia neno “mara” na kuonesha namna baadhi ya watumishi wa umma wanavyoendekeza uasharati hata wakiwa kazini.

Data zinazoonesha dhamira ya uasharati kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n’kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.5.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tafsida kwa kuficha matusi au kupunguza ukali wa maneno ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 49: **Ah, juzi juzi nilimkuta mtoto yule kwa Mwajuma, leo yupo na Faraji na Faraji mkocho kwa makoo.** Data hii ya tamathali ya semi ya tafsida imeweza kuibua dhamira ya uasharati kwa kuficha matusi kwa kutumia maneno “Faraji mkocho kwa makoo” na kudhihirisha namna baadhi ya watu wanavyopenda mambo ya uasharati.

Jedwali Na. 4.3.6.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tauria kwa kutumia maneno yenye tahajia moja lakini yakileta maana tofauti ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 40: **Alipomtazama usoni macho yao yalikutana, ya Yasmin yalikuwa manene yaliyorembuka remburembu naye akatahayari akakabiliana na Denge...** Data hii ya tamathali ya semi ya tauria imeweza kuibua dhamira ya uasharati kwa kutumia maneno ya tahajia moja ila maana ya maneno hayo ni tofauti kwa kusema “yaliyorembuka remburembu” na hivyo kubaini namna baadhi ya wanaume wanavyopenda uasharati kiasi cha kutotulia macho yao kwa kila mwanamke wanaemuona.

Jedwali Na. 4.3.8.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya dhihaki kwa kutumia maneno yenye kuonesha dharau na kumuweka mtu katika duni kupita kiasi. Ukurasa wa 103: **Alikwenda chumbani kwake akaleta kiti na baada ya kukaa aliwasalimu wageni, hamjambo watoto wazuri?** Data hii ya tamathali ya semi ya dhihaki imeweza kuibua dhamira ya uasharati kwa kuonesha baadhi ya wanaume huwafanyia dharau wanawake mara baada ya kufanya haja yao ya mambo ya uasharati.

Jedwali Na. 4.3.9.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia baadhi ya maneno zaidi ya mara moja ili kuisitiza ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 151: **Na weye nawe na Denge wako, kila uambiwalo, Denge, Denge unafikiri Denge atakupa nini?** Data hii ya tamathali ya semi ya takriri imeweza kuibua dhamira ya uasharati kwa kulirudia zaidi ya mara moja neno “Denge” na hivyo kuonesha namna baadhi ya wanawake wanavyoendekeza uasharati kiasi cha kutoona wala kusikia jambo lolote.

4.5.1.21 Dhamira ya Umuhimu wa Elimu

Dhamira hii ya umuhimu wa elimu ni miongoni mwa dhamira zilizoibuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n’kuvute* na kisha kuziorodhesha kwa njia ya majedwali sita. Elimu ni hali ya mtu kuwa na ujuzi, uelewa au utambuzi wa jambo fulani kwa kina. Hivyo dhamira hii ni muhimu sana kwa maisha ya wanadamu na maendeleo kwa ujumla.

Data zinazoonesha dhamira ya umuhimu wa elimu kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.2.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na uwezo huo ili kufikika ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 132: **Wakati wa jioni hewa yenye baridi huvuma kutoka ziwani kuja kuvipoza na kuvipa mawazo vichwa vya wanafunzi.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imefanikiwa kuibua dhamira ya umuhimu wa elimu kwa kuipa hewa yenye baridi uwezo wa kibinadamu wa kuvipa mawazo vichwa vya wanafunzi na kuweza kuonesha namna elimu ilvyo na umuhimu kwa jamii na kuwataka wanafunzi wawe wanatenga muda wa kupumzika katika masomo yao ili kuzipoza akili zao.

Jedwali Na. 4.3.3.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya sitiari kwa kulinganisha vitu viwili tofauti bila ya kiunganishi na kuleta uhamisho wa kimaana. Ukurasa wa 25: **Sisi jembe letu ni kalamu.** Data hili ya tamathali ya semi ya sitiari imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya umuhimu wa elimu kwa kulinganisha kalamu na jembe na kuonesha namna kalamu inavyompatia mtu riziki zake kwa wasomi kama jembe kwa mkulima.

Jedwali Na. 4.3.4.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya mubalagha kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo kwa kutia chumvi ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 187: **Huu ndio uzuri wa uchoraji na upakaji rangi wa siku hizi. Picha moja inaweza kuwa na maelezo elfu au zaidi.** Data hii ya tamathali ya semi ya mubalagha imeweza kuibua dhamira ya umuhimu wa elimu kwa kuyakuza mambo kuliko vile yalivyo na

kuweza kuonesha namna sanaa ya uchoraji ilivyo na umuhimu mkubwa kwa msanii huweza kueleza ujumbe wake kupitia njia hio ya uchoraji.

Jedwali Na. 4.3.6.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tauria kwa kutumia maneno yenye tahajia moja lakini yakiwa na maana tofati ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 23: **Niliona kwamba sasa wakati wa kusahau vitabu ulikuwa umeingia na kwamba nilikuwa nimeyafika maisha yanayoitwa maisha.** Data hii ya tamathali ya semi ya tauria imeweza kuibua dhamira ya umuhimu wa elimu kwa kutumia neno maisha mara mbili likiwa na maana tofauti na hivyo kudhihirisha namna elimu inavyomsaidia mtu katika maisha mara baada ya kumaliza kusoma.

Jedwali Na. 4.3.10.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini kwa kusisitiza jambo kwa kutumia maneno ya ukinzani. Ukurasa wa 10: **Nilipotoka hospitalini nilikuwa na nia ya kusoma kufa kupona.** Data hii ya tamathali ya semi ya tabaini imeweza kufanikisha kazi ya utafiti huu kwa kuibua dhamira ya umuhimu wa elimu kwa kutumia maneno yenye ukinzani katika kusisitiza jambo la kusoma na hivyo kuweza kuonesha umuhimu wa elimu kwa maendeleo ya baadae.

Data zinazoonesha dhamira ya umuhimu wa elimu kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.6.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tauria kwa kusisitiza jambo kwa kutumia maneno ya tahajia moja lakini maana zake ni tofauti ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa.

Ukurasa wa 215: **Bukheti alimwalia Mambo, akamwambia, wewe Mambo hujui mambo wala hujui vyombo. Kwa majahazi yale hakuna lisilowezezana.**

Data hii ya tamathali ya semi ya tauria kwa kuisitiza jambo la elimu kwa kutumia maneno ya tahajia moja lakini yana maana tofauti kwa kuhimiza umuhimu wa elimu ya baharini kwa manufaa ya jamii kwa ujumla.

4.5.1.22 Dhamira ya Ukombozi

Dhamira hii ya ukombozi ni miongoni mwa dhamira zilizoibuliwa na mtafiti kwa kupitia data alizozikusanya za tamathali za semi mbalimbali kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n'kuvute* na kisha kuziorodhesha kwa njia ya majedwali kumi na moja. Ukombozi ni zile harakati za kujiondoa katika hali duni na kuziendea hali za hali ya juu na iliobora zaidi, hali hizo zinaweza kuwa ni za kisiasa, kijamii na hata kiuchumi. Hivyo dhamira hii ni muhimu sana kwa maisha ya mtu mmoja mmoja na kwa jamii kwa ujumla kama zilivyooneshwa na waandishi wawili teule.

Data zinazoonesha dhamira ya ukombozi kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Kichwamaji*.

Jedwali Na. 4.3.3.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya sitiari kwa kulingaisha / kufananisha vitu viwili vilivyo tofauti bila ya kiunganishi na kuleta uhamisho wa kimaana. Ukurasa wa 10: **Mwafrika akawa Mwafrika; Mzungu akawa Mzungu; Mhindi akawa Mhindi; na Mwarabu akawa Mwarabu.** Data hii ya tamathali ya semi ya sitiari imeweza kuibua dhamira ya ukombozi kwa kufananisha mtu mmoja na mwengine na kuonesha namna uhuru na ukombozi ulivyo muhimu kwa nchi za kiafrika.

Jedwali Na. 4.3.5.1 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tafsida kwa kupunguza ukali wa maneno. Ukurasa wa 130: **Sasa tumwone anatembelea fimbo kwenda kuchungulia kaburi.** Data hii ya tamathali ya semi ya tafsida imeweza kuibua dhamira ya ukombozi kwa kupunguza ukali wa maneno kwa kuonesha namna mwanadamu anavyohitaji kujikomboa kutoka katika hali moja kwenda hali nyingine mpaka mwisho wa uhai wake.

Data zinazoonesha dhamira ya ukombozi kama zilivyoorodheshwa kutoka katika riwaya ya *Vuta n'kuvute*.

Jedwali Na. 4.3.2.2 linaomesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tashihisi kwa kukipa uwezo wa kibinadamu kitu kisicho na uwezo huo ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 100: **Mimi mwenyewe siku moja wakati narudi baharini nilikuta gari ya polisi imezikwa kichakani imejaa askari ndani na nna hakika walikuwa wakiisubiri mashua yangu.** Data hii ya tamathali ya semi ya tashihisi imeweza kuibua dhamira ya ukombozi kwa kuipa gari ya polisi sifa ya kibinadamu ya kuzikwa na kuonesha namna wanaharati wa uhuru hawatakiwi kukata tamaa katika harakati za ukombozi.

Jedwali Na. 4.3.3.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya sitiari kwa kulinganisha vitu viwili vyenye sifa tofauti bila ya kutumia kiunganishi na kuleta uhamisho wa kimaana. Ukurasa wa 243: **Denge amekonda ni mifupa mitupu.** Data hii ya tamathali ya semi ya sitiari imefanikisha kazi ya utafiti kwa kujibu swali namba tatu la utafiti huu na kuibua dhamira ya ukombozi kwa kulinganisha namna alivyokonda Denge na mifupa mitupu na hivyo kuweza kuonesha namna shida wanazozipata wanaharakati wa ukombozi katika nchi.

Jedwali Na. 4.3.5.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tafsida kwa kupunguza ukali wa maneno. Ukurasa wa 199: **Hakuelewa safari yake ya kuja Dar es salaam inahusiana nini na kupelekwa ndani ya nyumba kama ile iliyokaa kama gofu lililokumbiwa na wakazi wake kwa kuogopa wafu wanaoranda usiku kucha.** Data hii ya tamathali ya semi ya tafsida imeweza kuibua dhamira ya ukombozi kwa kuficha na kupunguza ukali wa maneno kwa kusema “kwa kuogopa wafu wanaoranda usiku kucha” hivyo data imeweza kuonesha namna wanaharakati za ukombozi wanatakiwa wasiwe na khofu ya kitu chochote katika mapambano yao.

Jedwali Na. 4.3.6.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tauria kwa kutumia maneno yenye tahajia moja lakini yakiwa na maana tofauti ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 207: **Msiwe na wasiwasi Mambo ndiye anayejua mambo hayo, atatueleza.** Data hii ya tamathali ya semi ya tauria imeweza kuibua dhamira ya ukombozi kwa kutumia maneno yenye tahajia moja lakini yakileta maana tofauti na kuonesha namna wanaharakati za ukombozi walivyo na mbinu mbalimbali za kujikomboa.

Jedwali Na. 4.3.7.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya shitizai kwa kutumia maneno yanayokusudia kuleta maana iliyokinyume au kinyume na ukweli ulivyo ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 60: **Sikiliza Sista, hawa wakoloni na vijibwa vyao ni mtu ni watu wapumbavu kabisa, kwao kila mtu mkoministi.** Data hii ya tamathali ya semi ya shitizai imeweza kutoa dhamira ya ukombozi kwa kuwaita wakoloni na vibaraka wao ni

watu wapumbavu na kuonesha namna wanavyowadhhalilisha wapigania uhuru kwa kuwaita wakomenisti ili kuwavunja moyo na kuwagawa.

Jedwali Na. 4.3.8.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya dhihaki kwa kumuweka mtu katika hali duni kupita kiasi ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 117: **Huseni alicheka sana na kusema, tokea lini Karimjee Club wakaingia watu kama nyinyi? Kwani hamjui kwamba nyumba ile ni ya watukufu tu?** Data hii ya tamathali ya semi ya dhihaka imeweza kuibua dhamira ya ukombozi kwa kuonesha dharau kwa lengo la kumuweka mtu katika hali duni kupita kiasi na kuweza kuonesha namna ya wanaharakati wa ukombozi wasivyokata tamaa na kuwa majasiri kuingia sehemu yoyote.

Jedwali Na. 4.3.9.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya takriri kwa kuyarudia rudia maneno zaidi ya mara moja kwa lengo la kusisitiza jambo. Ukurasa wa 60: **Sikiliza Sista, hawa wakoloni na vijibwa vyao ni watu wapumbavu kabisa, kwao kila mtu ni mkoministi. Ukidai haki yako wewe koministi. Ukisema ukweli wewe koministi. Ukipinga utawala wewe koministi...** Data hii ya tamathali ya semi ya takriri imeweza kuibua dhamira ya ukombozi kwa kulirudia neno koministi zaidi ya mara moja kwa lengo la kutaka kuwarudisha nyuma na kuwagawa wapigania uhuru.

Jedwali Na. 4.3.10.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya tabaini kwa kusisitiza jambo kwa kutumia maneno ya ukinzani ili kuipamba kazi ya fasihi na kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Ukurasa wa 101: **Wao wanavutia**

kule na sisi tunavutia huku na katika mvutano huo, hapana suluhisho linaloweza kupatikana isipokuwa kuwa huru. Data hii ya tamathali ya semi ya tabaini imeweza kuibua dhamira ya ukombozi kwa kutumia maneno yenye mvutano na kuweza kutoa ujumbe unaowataka wanaharakati ya ukombozi kutorudi nyuma katika ukombozi wa nchi.

Jedwali Na. 4.3.11.2 linaonesha data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi ya msisitizo bayani kwa kutumia maneno yenye kuonesha ushindani wa mawazo. Ukurasa wa 59: **Hakujua aanzie wapi lakini kwa ghafla aliuliza. Ati wewe msaliti! Msaliti! Denge alistuka na kushangaa. Msaliti nimemsaliti nani? Aliuliza.** Data hii ya tamathali ya semi ya msisitizo bayani imeweza kuibua dhamira ya ukombozi kwa kutumia maneno yenye kuonesha ushindani wa mawazo na kuweza kuwahamasisha wanaharakati za ukombozi wasirudi nyuma katika kutafuta uhuru wa nchi.

4.5.2 Hitimisho

Sehemu hii mtafiti amejadili dhamira zilizojitokeza kutokana na tamathali za semi za waandishi wote wawili kupitia vitabu vyao teule. Katika kujibu swali la namba tatu la utafiti huu lenye kusema “Ni dhamira zipi zinazojitokeza kwenye tamathali za semi katika riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n’kuvute*” ndipo mtafiti akapata jawabu ya swali hilo kwa kuweza kuziorodhesha dhamira ishirini na mbili zilizotokana na tamathali za semi kumi na moja. Hata hivyo baadhi ya dhamira zimeweza kuibuliwa kutoka kwa waandishi wote wawili na nyingine kuonekana kwa mwandishi mmoja tu. Kama jedwali lifuatalo linavyoonesha:

**Jedwali Na. 4.5.2.1 Linaonesha Dhamira Zilizojitokeza Kwenye Tamathali za
Semi Katika Riwaya za Kichwamaji na Vuta n'kuvute**

Na.	Dhamira	Kichwa maji	Vuta n'kuvute
1	Uongozi mbaya	5	11
2	Mapenzi ya nje ya ndoa	4	10
3	Umasikini	2	14
4	Mapenzi kwa wanafamilia	10	3
5	Uchawi na ushirikina	6	-
6	Umoja na mshikamano	4	10
7	Ulevi wa kupindukia	6	6
8	Mapenzi ya kweli	5	22
9	Chuki na uhasama	6	8
10	Unyanyasaji wa wanawake	3	17
11	Kufanya kazi kwa bidii	-	7
12	Usaliti	-	9
13	Malezi mabaya kwa watoto	5	5
14	Ujasiri na ushujaa	1	6
15	Wivu wa kupindukia	-	6
16	Upendo	9	7
17	Imani ya kidini	2	-
18	Upendo kwa viumbe hai	2	1
19	Umuhimu wa ndoa	1	2
20	Uasharati	13	6
21	Umuhimu wa elimu	7	1
22	Ukombozi	2	17

Chanzo: Data za Utafiti katika Riwaya ya *Kichwamaji* (2016)

4.6 Hitimisho

Kujumla katika sura hii, mtafiti ameanesha tamathali za semi alizoweza kuzikusanya kwa mbinu ya maktabani na kuweza kuziorodhesha kwa njia ya

majedwali ishirini na mbili (22) ndani ya tamathali za semi kumi na moja (11). Kisha mtafiti amebainisha dhamira ishirini na mbili (22) kutoka katika tamathali za semi hizo.

Katika sura hii utafiti umebainisha kuwa waandishi wote wawili wamefanana katika utumizi wa lugha katika kipengele cha tamathali za semi, kwani tamathali za semi zilizoibuliwa na mtafiti zimetumika na waandishi wote wawili.

Hivyo utafiti umeweza kubaini kuwa waandishi wa riwaya za Kiswahili wa Tanzania bara na wele wa Tanzania visiwani wanalingana kwa kiasi fulani katika matumizi ya lugha. Na hili mtafiti amelibaini kwa kutumia mbinu ya utafiti linganishi. Ingawa kuna tofauti ndogo ya utumizi wa tamathali za semi kwa waandishi hawa teule, kwani yule wa Tanzania bara imebainika kutumia tamathali za semi kidogo kulinganisha na yule wa Tanzania visiwani na hili limetokea kutokana na udogo wa riwaya ya *Kichwamaji* ambayo ina kurasa 196 wakati ile ya *Vuta n'kuvute* ina kurasa 247.

Kwa ujumla, katika sura hii, utafiti ulibaini kuwa waandishi wa riwaya teule wamefanana katika matumizi ya tamathali za semi na hakuna tofauti kati yao katika utumizi wa tamathali za semi. Na kwa upande wa dhamira utafiti umebainisha dhamira ishirini na mbili zilizoibuliwa na mtafiti kupitia tamathali za semi zilizowasilishwa na waandishi teule.

SURA YA TANO
MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Utafiti huu umebainisha matumizi ya lugha katika kipengele cha tamathali za semi kwa waandishi wawili tofauti kwa kupitia vitabu vyao teule navyo ni *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*. Utafiti umefanikiwa kuonesha tamathali za semi kumi na moja ambazo ndizo zilizotumiwa na waandishi wote wawili na kuweza kubainika kwa mfanano uliopo wa watunzi wa riwaya hizo katika kipengele cha tamathali za semi. Na kupitia tamathali za semi hizo utafiti umeibua dhamira ishirini na mbili (22) kutoka katika majedwali ishirini na mbili kwa kupitia kiunzi cha mkabala wa nadharia ya simiotiki na ile ya udhanaidhi.

5.2 Muhtasari

Utafiti huu ulihusu kuchunguza matumizi ya lugha kutoka katika riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kufanya tathmini kwa kuchunguza matumizi ya tamathali za semi jinsi zilivyotumika kwa waandishi wawili teule nao ni E. Kezilahabi aliyeandika riwaya ya *Kichwamaji* (1974) na Shafi A. Shafi aliyeandika riwaya ya *Vuta n'kuvute* (1999) katika nyanja ya utafiti linganishi ili kubaini jinsi waandishi hao walivyofanana na kutofautiana katika matumizi ya lugha katika kipengele cha tamathali za semi.

Utafiti huu uliongozwa na malengo mahsusi matatu ambayo yalijibiwa na maswali matatu. Malengo hayo ni; Kubaini mifanano iliyopo ya tamathali za semi katika riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*, kubaini tamathali za semi zinazotofautiana

katika riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute* na lengo mahsusi la mwisho ni kuainisha dhamira zilizojitokeza kwenye tamathali za semi katika riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*.

Tatizo la utafiti huu limetokana na mtafiti kutaka kuelewa ni kwa kiasi gani waandishi wa riwaya kutoka Tanzania bara wanavyotofautiana ama kulingana na waandishi wenzao wa riwaya kutoka Tanzania visiwani katika kuitumia lugha ya fasihi katika kazi zao. Na kama inavyoeleweka kwamba waandishi wengi wa kazi za fasihi kutoka Tanzania bara Kiswahili huwa ni lugha yao ya pili ukilinganisha na waandishi wengi wa kazi za fasihi wa Tanzania visiwani ambao Kiswahili huwa ni lugha yao ya kwanza. Kwa hiyo, tatizo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza matumizi ya lugha yalivyotumika kwa waandishi Kezilahabi mwenye asili ya Tanzania bara na Shafi A. mwenye asili ya Tanzania visiwani. Kwa kupitia tatizo hilo, mtafiti ameweza kubaini kufanana kwa waandishi hao katika kipengele cha tamathali za semi isipokuwa wametofautiana kwa idadi ya matumizi hayo.

Katika utafiti huu mbinu ya utafiti imejadiliwa kwa kina katika sura ya tatu. Katika sura hiyo, imebainishwa kuwa walengwa wa utafiti huu walikuwa ni watunzi wa riwaya ya *Kichwamajii* (1974) iliyoandikwa na Kezilahabi na riwaya ya *Vuta n'kuvute* (1999) iliyoandikwa na Shafi A. Shafi waandishi hawa wameteuliwa na mtafiti kwa sababu ndio watunzi wa riwaya teule. Sampuli ya utafiti huu iliteuliwa kwa kutumia mbinu ya uteuzi wa madhumuni maalumu. Data za utafiti huu zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji wa machapisho. Na hii ilikuwa ni mbinu kuu ambayo ilimsaidia mtafiti kuchambua tamathali za semi zilizotumiwa na waandishi wote wawili.

Tasnifu hii ilikuwa na maswali matatu ambayo yameweza kupata majibu kulingana na tamathali za semi zilizoibuliwa pamoja na dhamira zilizojitokeza kutokana na tamathali za semi hizo. Maswali ya utafiti huu ni hayo yafuatayo:-

- (i) Ni tamathali za semi zipi zinazofanana katika riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*?
- (ii) Ni tamathali za semi zipi zinazotofautiana kati ya riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*?
- (iii) Je! Ni dhamira zipi zinazojitokeza kwenye tamathali za semi katika riwaya za *Kichwamaji* na *Vuta n'kuvute*?

Kupitia maswali hayo, utafiti uliweza kulijibu swali la kwanza kwa kuonesha namna waandishi wote wawili walivyofanana katika matumizi ya tamathali za semi, kwani waandishi wote wawili wametumia tamathali za semi kumi na moja nazo ni:- tashibiha, tashihisi, sitiari, mubalagha, tafsida, tauria, shitizai, dhihaka, takriri, tabaini na msisitizo bayani.

Pia katika kulipatia jawabu swali la pili la utafiti huu, mtafiti amebaini kupitia tamathali za semi alizozikusanya kutoka kwa waandishi wote wawili ni kuwa wote wametumia tamathali za semi za aina moja, hivyo hakuna tofauti katika matumizi ya tamathali ya semi.

Kwa upande wa swali la tatu la utafiti huu, mtafiti ameweza kulipatia jawabu kwa kuibua dhamira ishirini na mbili (22) ambazo zote zimeibuliwa kutoka kwa waandishi wote wawili. Dhamira hizo ni kama hizi zifuatazo:- uongozi mbaya,

mapenzi nje ya ndoa, athari za umasikini, mapenzi kwa wanafamilia, athari ya uchawi na ushirikina, umuhimu wa umoja na mshikamano, ulevi wa kupindukia, mapenzi ya kweli, chuki na uhasama, unyanyasaji wa wanawake, kufanyakazi kwa bidii, usaliti, malezi mabaya kwa watoto, ujasiri na ushujaa, wivu wa kupindukia, upendo, imani za kidini, upendo kwa viumbe hai, umuhimu wa ndoa, uasharati, umuhimu wa elimu na ukombozi. Ingawa dhamira hizo zimetokana na tamathali za semi kumi na moja (11) zilizotumiwa na waandishi wawili teule lakini zimetofautiana kutokanana na tamathali za semi ambapo baadhi ya dhamira ziko kwa waandishi wote wawili, na baadhi ziko kwa mwandishi mmoja tu.

Kwa ujumla kulingana na data zilizokusanywa za matumizi ya tamathali ya semi zinaonesha umahiri wa waandishi hawa wawili katika kipengele hicho cha tamathali za semi. Kwa mujibu wa mbinu ya kukusanyia data, mbinu ya kimaktaba iliyotumiwa katika utafiti huu imedhihirisha matumizi mbalimbali ya tamathali za semi na kuzionesha kwa njia ya majedwali kulingana na idadi ya tamathali za semi na mwisho kuibua dhamira mbalimbali kutokanana na majedwali hayo.

5.3 Mapendekezo

Utafiti huu umehusika na kuchunguza matumizi ya lugha katika riwaya ya *Kichwamaji* na riwaya ya *Vuta n'kuvute* ikiwa ni utafiti linganishi. Utafiti umeweza kuonesha namna waandishi wa riwaya hizo walivyofanana katika kipengele cha matumizi ya tamathali ya semi na mwisho kuibua dhamira mbalimbali zilizo na umuhimu mkubwa kwa jamii ya waswahili. Hivyo inadhihirika wazi kuwa waandishi wa riwaya teule wamefanana katika uandishi wa kazi zao kwa kuingiza tamathali za

semi zilizo sawa isipokuwa wametofautiana katika kuibua dhamira zinazotokana na tamathali za semi zilizotumiwa na waandishi hao.

Katika utafiti huu mtafiti ameshughulikia suala la tamathali za semi tu ingawa kuna vipengele vingi katika matumizi ya lugha katika kazi za fashihi. Hivyo mtafiti ameacha pengo kubwa kwa watafiti wengine ambao kwa upande wao wanaweza kuchagua kipengele kingine miongoni mwa vipengele vya matumizi ya lugha na kuanza kuvishughulikia kwa upande wao.

Kupitia matokeo ya utafiti huu, mtafiti anapendekeza kufanyike kwa utafiti mwengine zaidi kuhusiana na waandishi hawa wawili hasa katika matumizi ya lugha kwa upande wa vipengele vyengine vya lugha. Mtafiti anatoa wito kwa wanafunzi wa ngazi tofauti kuangalia kwa kina utafiti huu na kisha kubaini pengo liliopo na kulifanyia kazi katika kazi za utafiti. Aidha mtafiti anapendekeza kupita dhamira zilizoibuliwa kutokana na tamathali za semi zifanyiwe utafiti kwa kulingana na jamii husika.

5.4 Hitimisho

Katika sura hii, mtafiti ameeleza kwa ufupi yale yote yaliyojadiliwa katika utafiti huu. Kisha kuelezea yale yaliyopatikana kupitia mbinu ya maktabani tokea katika kutafuta data, kuzichambua hadi huziwasilisha na kuonesha matokeo ya utafiti kwa ujumla. Mwisho mtafiti akaonesha mapendekezo ya kazi yake ya utafiti kwa lengo la kuwaongoza watafiti wengine watakaofanya utafiti katika nyanja hii.

MAREJELEO

- Adam, O. A. (2014). “Kuchunguza Dhamira za Kijamii na Kiutamaduni katika Riwaya ya Kiswahili.” Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam, Tanzania
- Andrews, R. (2003). *Research Questions*. London: MPG Books.
- Asha, K. H. (1981). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. Zanzibar: Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni.
- Baraza Kuu la Waislamu Tanzania BAKWATA, (1996). *Elimu ya Dini ya Kiislamu Shule za Sekondari, Kidato cha Nne*. Dar es Salaam. Tanzania Publishing House.
- Baraza la Kiswahili Zanzibar BAKIZA. (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.
- Creswell, J. W. (2009). *Research Design (3rd ed.)*. London: SAGE Publication ltd.
- Dino, F. (2002). Module on Barthes: Five Codes Introductory Guide to Critical: Theory. Retrieved on 11th January, 2016 from: [http://www.purdue.edu/guide to theory/naratology/modules/barthes codes.html](http://www.purdue.edu/guide/to_theory/naratology/modules/barthes_codes.html).
- Fadhili, F. E. (2013). “Kuchunguza Dhima ya Mtindo Katika Tamthilia.” (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam, TZ
- Kezilahabi, E. (1974). *Kichwamaji*. Nairobi: Sitima Printers Stationers Ltd.
- Kezilahabi, E. (1983). “Utunzi wa Riwaya na Hadithi Fupi” katika Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili namba 3. Dar es Salaam. Tanzania.
- Khatib, M. S. (1986). *Mulika Namba 18. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Dar es Salaam.

- Kharifa, H. M. (2013). "Kufanana na Kutafautiana kwa Maudhui na Fani Kati ya Methali za Kitanzania na za Kilibya." Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam, Tanzania.
- Kiango, J. G. na Mdee, J. S. (1995). *Utafiti na Utungaji wa Kamusi*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kothari, C. R. (2002). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International (P) Ltd.
- Leech, G. N. (1969). *A Linguistic Guide to English Poetry*. New York. Longman Group Inc. Limited.
- Low, N. (2011). "Athari ya Lugha katika Kuibua Dhamira. Mifano Kutoka Nyimbo za Kizazi Kipya Zinazohusu UKIMWI." Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Tanzania.
- Madumulla, J. S. (2009a). *Riwaya ya Kiswahili, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Nairobi: Sitima Printers and Stationary.
- Madumulla, J. S. (2009b). *Riwaya ya Kiswahili, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Nairobi: Sitima Printers and Stationary.
- Mdee, J. S., Njongu, K. na Shafi. A. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21*. Nairobi: Longhorn Publishers ltd.
- Mhilu, G. G. na wenzake. (2010). *Kiswahili Kwa Shule za Sekondari. Kidato cha Tatu na Nne*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.
- Mlacha, S.A.K. (1989a). "The Use of Methaphor in Kezilahabi's Novel: *Rosa Mistika*". Katika Kiswahili. Juzuu Nambari 56. Dar es salaam. TUKI
- Mlacha, S.A.K. (1989b). "The Use of Methaphor in Kezilahabi's Novel: *Rosa Mistika*". Katika Kiswahili. Juzuu Nambari 56. Dar es salaam. TUKI

- Mlacha, S. A. K. na Madumulla, J. S. (1991a). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press
- Mlacha, S. A. K. na Madumulla, J. S. (1991b). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Mohamed, M. A. na Senkoro, F.E.M.K. (1987). *Tahakiki*. Dar es Salaam: Printpark (Tanzania) Limited.
- Mohochi, E. S. (2000). "Usimulizi wa Riwaya ya Nyongo Mkalia Ini" Katika Nordic *Journal of African Studies* 9 (2), 23 – 41.
- Mosha, P. G. (2013). "Usawiri wa Muhusika Padri Katika Riwaya za Kezilahabi" Chuo Kikuu Dar es Salaam.
- Msokile, M. (1992). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Muhammed, S. A. (1981). *Misingi ya Nadharia ya Fasihi*. Zanzibar: Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni.
- Muhando, P. na Balisidya, N. (1976). *Fasihi na Sanaa za Maonesho*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mulokozi, M. M na Kahigi, K.K (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani yetu*. Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Mulokozi, M. M. (1996a). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mulokozi, M. M. (1996b). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mulokozi, M. M. (1996c). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

- Mulokozi, M. M. (2010). "A Survey of Kiswahili Literature: 1970-1988." Current Research Interest: Kiswahili Language and Literature, Writing and Publishing. University of Dar es Salaam Institute of Kiswahili Research. Dar es Salaam, Tanzania.
- Mussa, F. K. (2007). "Mchango wa Suala la Ukombozi katika Riwaya za Shafi A. Shafi." Zanzibar, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.
- Mwamanda, J. (2008). *Nadharia ya Fasihi Uchambuzi na Uhakiki*. Dar es Salaam: JPD Company and General Supplies Ltd.
- Mwangoka, N. (2011). "Motifu za Safari na Msako Katika Makuzi ya Wahusika wa Riwaya za E. Kezilahabi." Chuo Kikuu Dar es Salaam, Tanzania.
- Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Ruanda: Augustana College. Rock Island.
- Njogu, K. na Chimerah, R. (1999a). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Njogu, K. na Chimerah, R. (1999b). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Ponera, A.S. (2014). *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.
- Richard, M. (2002). *Mchango wa Waandishi wa Riwaya katika Fasihi, Uandishi na Uchapishaji*. Dar es Salaam. Dar es Salaam University Press.
- Rugebandiza, A. (2011). "Matumizi ya Ishara katika Riwaya za S. Chachange: Makuadi wa Soko Huria na Almasi za Bandia." Chuo Kikuu Dar es Salaam. Tanzania.

- Rwegoshora, H. M. M. (2006). *A Guide to Social Science Research*. Dar es Salaam. Mkuki na Nyota Publishers.
- Salem, B. M. (2013). "Mahusiano ya Lugha na Vipengele Vingine vya Fani katika Tamthilia." (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Sakkos, T. (2008). "Existentialism and Feminism in Kezilahabi's Novel Kichwamaji." *Katika Kiswahili Forum* 15(2), 51-61.
- Sanz, A. na Romero, D. (2007). *Literatures in Digital Era: Theory and Praxis*. Cambridge Scholars Publishing, Newcastle, NE5 2JA, UK.
- Sauda, U. (2007). "Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Uganga Zanzibar." Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar.
- Senkoro, F. E. M. K. (1977). "Riwaya ya Kiswahili na Maendeleo ya Umma." *Tasnifu ya Uzamili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Senkoro, F. E. M. K. (1984). *Fasihi*. Dar es Salaam: Univesity Press and Publicity Centre.
- Senkoro, F. E. M. K. (2006). "Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano baina ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi." Kioo cha Lugha. Juzuu Nambari 4.
- Senkoro, F. E. M.K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: Kautu Limited.
- Senkoro, F. E. M. K. (2011a). *Fasihi*. Dar es Salaam: Kautu Limited.
- Senkoro, F. E. M. K. (2011b). *Fasihi*. Dar es Salaam: Kautu Limited.
- Senkoro, F. E. M. K. (2011c). *Fasihi*. Dar es Salaam: Kautu Limited.
- Shayo, M. K. (2011). *Usawiri wa Mimba na Watoto wa Nje ya Ndoa katika Riwaya: Nyota ya Rehema na Vuta n'kuvute*. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Shumbusho, G.N. (2003). *Research Report Writing Skills*. Morogoro: Department of Research and Publications Mzumbe.

- Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni TAKILUKI, (1997). *Malenga Wapya*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili TUKI, (2004), *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. East and Central Africa, Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Thung, J. (2010). *Mastering PTE Education*. Nairobi: Oxford University Press.
- Uwe, F. (2007). *Designing Qualitative Research*. New delhi: SAGE Publications Inc.
- Wamitila, K. W. (1999). "What in a Name Towards Leterary Onomastics in Kiswahili Literature." *Kyallo Wadi Wamitila's Journal*. AAP60:35-44
- Wamitila, K. W. (2002a). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Phoenix Publishers Ltd. Nairobi.
- Wamitila, K.W. (2002b). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Phoenix Publishers Ltd. Nairobi.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publications Ltd.
- Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.
- Wamitila, K. W. (2006). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.
- Wamitila, K. W. (2007). "Narative Structure and Metaphor: Towards a new Aesthetics of the Kiswahili Novel." in *Kiswahili Vol 70*. Dar es Salaam: IKS.
- Zepetnek, S. T. (1998). *Comparative Literature Theory, Method, Application*. Amsterdam: Printed in The Netherlands.

VIAMBATANISHO

Kiambatanishi 1: Tamathali za Semi Katika Riwaya ya *Kichwamaji*

Tamathali za Semi ya Tashibiha

1. Nilipokuwa njiani nikirudi nyumbani nilisikia sauti za walevi wakiimba kama kwamba wakilia.
2. Kwa nini msichana mzuri kama wewe hupendi kuolewa? Nilimuuliza. Ilikuwa kama kwamba nilipasua mtungi uliokuwa umejaa maji ya huzuni
3. “Ashama” alinambia. Niliashama kama kinda la ndege kiotani.
4. Kwa vyovyote nilipaswa kutoa wazo langu kuhusu muziki. Sikuweza kuhutubiwa kama mtoto mdogo.
5. Tegemea alijaribu kujikinga kwa mikono. Na hilo ndilo lilikuwa kosa lake kubwa. Alishikwa mara moja na kutupwa chini kama gunia, miguu juu.
6. Alikufa bila ya vidole vya mkono na mguu. Nyanya yake alikuwa mchawi wa kustaajibisha. Alikufa macho mekundu kama umeme.
7. Wazee wote karibu wamekwenda. Ajabu ndio hio. Wazee wanafuatana mmoja baada ya mwengine, alisema. Wanapasuka tu kama kuni.
8. Tegemea naye pombe ilipomwingia maneno yalitiririka na kufuatana kama shanga kwenye uzi.
9. Matumaini yetu yalifutika kwa urahisi kama mwalimu afutavyo mandishi yake ubaoni ambayo bado hayajanakiliwa na wanafunzi.
10. Gari halikuweza kusimama upesi. Yule bwana alikanyagwa, hapo hapo akafa. Kichwa chake kililia kama bunduki kilipopasuka.

Tamathali ya Semi ya Tashihisi

1. Hofu kubwa ilinishika na pombe yote iliruka. Niliona mwisho wa maisha yangu hapa duniani.
2. Upande wa magharibi sikuweza kuona vizuri kwa sababu jua ambako lilikuwa linatua lilinichoma machoni kwa mionzi.
3. Nilipotazama chini juu ya jiwe niliona mijusi wakiota jua nao walinisalimu kwa kutingisha vichwa.
4. Alikuwa amefunikwa mwili mzima isipokuwa uso ndio uliokuwa umewachwa wazi ukidai machozi mengi zaidi.
5. Siku ya tatu Kalia pia alitusaidia; lakini hata hivyo shamba lilikuwa bado linatutazama.
6. Shetani naye ana bahati nzuri, kwani ninafikiri kwamba wanawake wazuri wengi huenda motoni na shetani huwafaidi. Siku ilijileta wenyewe.
7. Tulisimama karibu tukitazama upande wa kaskazini; tuliinama na majani yalilia kati ya meno ya visu vyetu vikali.
8. Siku ya pili Sabina alikuja na birika la maji, kwani siku ya kwanza tulishikwa na kiu ya maji.
9. Bata alipigapiga kidogo miguu yake na roho ikamtoka. Nilipokuwa namtoa manyoya wale bata waliendelea kunitazama.
10. Bata alipigapiga kidogo miguu yake na roho ikamtoka. Nilipokuwa namtoa manyoya wale bata waliendelea kunitazama.
11. Kwa hiyo mtu anaamini kwamba Mungu yupo ni yule aamuaye kwa kufuata milango ya fahamu zake. Kwake fahamu zinatawala bongo.
12. Mimi naona kwamba sababu kubwa ni kwamba ndoa imepoteza maana yake.

13. Nilipofika Chuo Kikuu barua ya Sabina niliikuta kweli imeningoja.
14. Wakati wa jioni hewa yenye baridi huvuma kutoka ziwani kuja kuvipoza na kuvipa mawazo vichwa vya wanafunzi.
15. Maneno hayo yalitukata maini sote wawili, nami sikutaka kuzungumza ingawa nilikuwa na maswali ya kumwuliza.
16. Baada ya kula nililala kitandani. Hata hivyo sikuweza kuondoa wasiwasi. Usingizi ulikataa kuja.
17. Mwezi mmoja ulipita, wa pili ukamezwa, tukapata habari kutoka nyumbani kwamba mahindi yalikuwa yamekwisha vunwa na kuuzwa.

Tamathali ya Semi ya Sitiari

1. Mimi uwanja wa mpira, kwangu majani hayaoti.
2. Sabina –nikwambie mtoto wangu- ni tunda baya na nisingependa wewe ulile.

Tamathali ya Semi ya Mubalagha

1. Tulikwenda kwa vidole mpaka mlango wa nyuma, tukajibanza ukutani.
2. Nilijiona kwamba nilikuwa na uwezo wa kuokoa maisha yake kwa tendo moja dogo tu ambalo lilikuwa halihitaji hata tone moja la jasho. Nilijiona mungu mdogo.
3. Kazimoto; alinistua, ubaya wako ni kwamba unafikiri mno; mara zengine unakuwa kama unaota; mara zingine kama mwehu.
4. Huu ndio uzuri wa uchoraji na upakaji rangi wa siku hizi. Picha moja inaweza kuwa na maelezo elfu au zaidi.

Tamathali ya Semi ya Tafside

1. Nilikata shauri kutumia njia yoyote ili kumpata huyu msichana, siyo kumpata tu kwa siku moja, isipokuwa mpaka nihakikishe kwamba tumbo lake lilikuwa zito.
2. Nunda mla watu alipojiweka tayari kumlalia, yule mwanamke alimshika sehemu za chini. Nunda alilia kama beberu.
3. Huu ugonjwa wa vijana kuanza mchezo mbaya wangali umri wa miaka kumi na miwili na mara zingine kujazana mimba ovyo na kuharibiana maisha.
4. Sasa tumwone anatembelea fimbo kwenda kuchungulia kaburi.
5. Nilipopata barua mbili. Moja ilikuwa imetoka nyumbani kwao Sabina. Nayo ilikuwa ikiuliza kijanja kama Sabina alikuwa amekwisha pata cho chote ndani ya tumbo lake,

Tamathali ya Semi ya Tauria

1. Aliomba toba lakini mwanamke hakumwacha mpaka majirani walipokuja. Wakamkuta Kalia! Macho mekundu, analia kama beberu.
2. Hivi muziki wa Kiafrika unakupendeza nini? Unalia mbu! mbu! mbu! tangu mwanzo mpaka mwisho, mwishoe unaleta mbu ndani ya nyumba.
3. Kila siku Sabina, alifoka, wengine wanaita wake zao Maggy, Betty; wewe kila siku Sabina! Sabina! Unataka kusabina nini. Mapenzi gani hayo!

Tamathali ya Semi ya Shitizai

1. Mimi mwenyewe, ingawa alikuwa jirani aliniona taka ya mwisho hasa kwa kuwa alinizidi mwaka mmoja kwa umri.

2. Njiani tukirudi Sabina alisema, sikuamini kwamba wewe utaweza siku moja kuwa mtu mzima. Siku hizi hata wewe umeota ndevu!
3. Usemayo ni kweli, lakini ninavyoamini mimi mwanamume asipooa akili zake pia zinakwenda tenge kidogo.
4. Galoni mbili tu! Pombe ya huku si kama ya kwenu Ukerewe. Mke wangu ananiambia kila siku kwamba pombe ya kwenu inaleweshwa sana. Ya hapa ni maji, yatawezaje kuleweshwa?

Tamathali ya Semi ya Takriri

1. Mnazungumza na mwehu! Alisema kwa kelele. A! anasema hakuna Mungu. Hakuna Mungu! Mtoto wa nani? Mababu na mababu wamekwenda; wamechukuliwa na nani?
2. Kama jambo la gauni limekuudhi vaa suruali yako uende zako! Gauniii! Gauni! Gauni limekuwa gauni. Vaa suruali uende zako! Leo hufani jambo lolote nami. Yaani unanifikiria mimi maskini omba-omba gauni!
3. Kazimoto, ndugu yako ha, ...ako kati... katika hali mbaya sana, umkute, umkute!
4. Mimi siwezi kulima! Kama ni chakula mtaninyima! Tegemea alijibu. Utalima! Mimi nimesema siwezi! Nimesema utalima na utalima!
5. Mtoto wangu akiharibika maishani. Lawama ni yangu. Lazima nimsaidie. Lazima kabisa nimsaidie.
6. Desemba iliingia. Wanafunzi wakawa wamekwisha funga shule. Krismasi ikawa Krismasi. Krismasi itafika! Krismasi karibu!

Kiambatanishi 2: Tamathali za Semi Katika Riwaya ya *Vuta n'kuvute*

Tamathali ya Semi ya Tashibiha

1. Eh! Basi wewe umeingia kama shetani moja kwa moja mpaka kitandani na kuanza kumwalia mtoto wa watu kama umeona ajabu gani sijui.
2. Waliingia vichochozoni, Salum mbele Roger nyuma anafuata tu kama mkia.
3. Tokea kuhamia kwa Mwajuma, Yasmin hakuwa mtokaji. Alikuwa hendi harudi. Yeye na ndani na ndani na yeye kama mwari.
4. Moyo wa Yasmin ulichanua kama ua kwa furaha kwani fursa kama ile alikuwa anaitamani siku nyingi...
5. Dansa ilikuwa imestawi na wachezaji walikuwa wakitimka kama wehu.
6. ...kwa ghafla alistukia kijana mmoja amemsimamia mbele yake anayumba kama mpopoo unaopigwa na upepo.
7. Alicheza mpaka wapigaji walipopumzika na hapo tena alipoanza kumtafuta Yasmin ambaye alimkuta amejibanza palepale pembeni amesimama kama mlingoti.
8. Yeye alikuwa akipenda kuvaa shati jeupe na suruali ya kipande nyeupe, soksi nyeupe zilizomfika mpaka magotini na viatu kila wakati vilikuwa viking'aa kama kioo.
9. ...ushoga baina ya Yasmin na Mwajuma ulivyozidi kustawi mfano wa bustani iliyokuwa ikitiliwa maji kila siku.
10. Walikuwa kama chanda na pete.
11. We Denge! Alisimama na kuangalia nyuma alihema kama punda aliyechoka.

12. ...alimwona Mambo amekumbatia kipande cha mwanamke, kajaza, mweusi kama mpingo, meno meupe kama bafta.
13. Denge kuja kunijazia makorokocho chumbani, chumba chenyewe kama kifuu, kucha mtu halali kwa ghasia za panya.
14. Yasmin alizichana nywele zake vizuri akazizongazonga na kuzifungia juu zikawa kama sega la nyuki.
15. Mwajuma tokea hapo macho yake remburembu, si kwambii tena na zile pegi mbili tatu alizokunywa, macho yake yakielea tu kama popoo za kitendawili maarufu, zenye kuvuka mto.
16. Jasho linamtoka, anapuma kama ng'ombe anayeburura gari...
17. Aligonga mlango na suti nene iliyovuma kama mlio wa tarumbeta ilijibu come in.
18. Mweupe kama safura, rangi aliyoipata kwa kule kukaa kwake ndani sana
19. Alihisi akikiuka miiko aliyopewa na Koplo Matata huenda akajikuta tena katika janga kubwa mfano wa moto wa jahanamu.
20. Aliamrisha huku vipande vya nyama vimo mdomoni anavichakua na mashavu yake yalikuwa manene, akawa kama bunju aliyevimba.
21. Inspekta Wright alirudi nyuma ya kiti chake, anapumua kama mbogo aliyekasirika.
22. Siku ile Inspekta Wright alikuwa mkali kama moto na maskini Koplo Matata, alizungushwa kama pia, mara nenda huku mara nenda kule.
23. Afandi, alisimama sawasawa kama mlingoti.
24. Askari kanzu walimsaka kama mhalifu na hapo kwake n'do njia ya kawaida...
25. Tumbo lilikwisha kuwa kubwa limeumuka kama aliyemeza hamira.

26. Mwajuma chini Yasmin juu. Nguo zimewapanda mpaka mapajani kila mmoja anapiga mikambi kama chatu waliokatwa vichwa.
27. Inspekta Wright nae akamtazama kamishna, wakawa wanatazama tu kama majogoo walio kwenye medani ya mapigano.
28. Aliwekwa katikati ya askari wawili wote wamekasirika nyuso wamezikunja kama waliomeza shubiri.
29. Wafungwa walizongea kama nzi wanapouzonga mzoga...
30. Alikuwa hendi harudi, yumo ndani tu kama kizuka, kwa sababu ya wivu aliokuwa nao Shihabu.
31. Kaza mkono basi kama mwanamme, umelekea kama mwanamke, ...
32. Inspekta Wright alimtazama Denge akaona jinsi uso wake ulivyokoboka, amekonda kama aliyemezwa na chatu.
33. Denge alipenya mlangoni kama mshale akampiga kikumbo askari mmoja na alipoanguka wengine wakapata mwanya wa kupenya.
34. Kuna huyo Hulka, mjuba, ana mdomo mchafu kama choo...
35. Mambo alimweleza. Siye tena yule Mambo anayechekacheka ovyo kama bahuli.
36. Buheti sura ilimbadilika moyo wake ukachanua kama asumini...
37. Alikuwa yu-hoi, nguvu zimwemwisha, ananuka kama fungo.
38. "Usicheze na bahati," akajiona kweli ana bahati wanaume wanamtetemekea kama Malkia wa Misri.
39. Na alipojaribu kuliangalia tena lile gari hakuliona kwani lilipita kama umeme...

40. Huo ilikuwa usiku wa Mwajuma. Alikula kungumanga zikampata, macho mekundu kama tipitipi, akaghani na kucheka.
41. Sasa ni mtoto mkubwa wa miaka mitatu. Kitoto kizuri, kishamba kwisha kazi, mchangamfu, maneno kama chiriku.

Tamathali ya Semi ya Tashihisi

1. Maneno yalimkwama yakawa hayataki kutoka kinywani mwake. Hakujuua aanzie wapi lakini kwa ghafla aliuliza, Ati wewe msaliti?
2. Ukenda hapo utamkuta Bashiri yuko katikati ya mlima wa machungwa, yamemzunguka huku na huku.
3. Alikuwa amekaa barazani jua limeshapanda, limejimwaga mwaa.
4. Somoyeee. Sauti yake ikajaa nyumba nzima, kukifukuza kimya kilichokuwemo mle ndani.
5. Hapa nilipo akili si yangu, hayo unayonielea yamekivuruga kichwa changu.
6. Mimi mwenyewe siku moja wakati narudi baharini nilikuta gari ya polisi imezikwa kichakani imejaa askari ndani na nna hakika walikuwa wakiisubiri mashua yangu.
7. Upepo ukaanza kuvuma kutokea kusini ambako uliburura mawingu mazito yaliyosambaa na kuufanya mwezi ushindwe kutawanya nuru yake juu ya uso wa bahari.
8. Aliwaza labda amweleze au aiweke siri ile moyoni mwake huku ikimla na kumtafuna pamoja na kumuondolea raha ya maisha.
9. Shilingi mia sita zilikuwa zikimwasha, na alitaka kumthibitishia shoga yake aliyemfadhili siku nyingi...

10. Shughuli zote za maandamano zilimalizika saa saba mchana na baada ya hapo watu walitawanyika kila mtu akashika njia yake.
11. Migogoro ile ya mawazo iliuvuruga moyo wake akayaona maisha yameanza kumuelemea, yanamsukuma sukuma na kumyumbisha bila ya yeye mwenyewe kujua yanampeleka wapi.
12. Juu ya dari yalining'inia mapankaboi mawili na yanapowashwa hulifukuza joto lote...
13. Majumba hayo yamesimama tokea enzi na dahari yameikabili bahari yakiiangalia ikijaa na kupwa.
14. Maisha yanakwenda tena yanakwenda mbio hakuna awezaye kufukuzana nayo.
15. Zile nishai ndogondogo alizokuwa nazo, baada ya kumaliza chupa ya wiski aliona kama zinamtesa badala ya kumletea furaha.
16. Wakati wanakula, Huseni na Mambo wanagombana na visu na nyuma...
17. Alikunjua kirago kimoja akalie lakini alipokikunjua kunguni walikuwa wakiendeshana mbio kama wenye kucheza foliti.
18. Chumba kilibadilika ghafla na kimya chote alichokikuta Denge tokea asubuhi kikatoweka na chumbani mle mkawa vurugu tupu.
19. Chumbani mle watu wakaanza kuwa hawaonani na mbu wakaanza kujiandaa kwa karamu yao ya usiku.
20. Alipotupa macho juu ya meza, Denge aliona chungu ya barua zilizopandiana akamwuliza Mambo, barua za nani?
21. Akaingia ndani taratibu na chumba kikaimeza harufu nzuri ya manukato aliyojipaka.
22. Mji ulikuwa jii, umejinamia utafikiri umefikwa na msiba.

23. Aligeuka akamtazama Yasmin, bado amelala, akawaza jinsi kifo kilivyomkosea chupuchupu.
24. Furaha na statere yote iliyokuwemo ndani ya chumba kile ikayayuka chumba kikajaa majonzi.
25. Usiku ule ulikwa mwema uliobarikiwa nyota nyingi na mwezi kamili na vyote hivyo vilikuwa vikicheka nao vikawakarimu nuru.
26. Hewa ya kutoka nje ilipigana kikumbo na ile itokayo ndani kwa kugombea nafasi ya uwazi wa dirisha.
27. Alikwenda mpaka karibu yake akamtazama Denge kwa jeuri na kumwambia, Najua inzi nasema nini?
28. Chumba kilichokuwa na wingi wa mapenzi na maneno matamu, hivi sasa alikiona kidogo kama kifuu. Kinambana na kumletea udhia.
29. Akili yake ilikuwa mbali na pale kilipo kiwiliwili chake, akiwaza na kujiuliza maisha sasa yanampeleka wapi.
30. Wafungwa wote walijipanga, wakahesabiwa na kupekuliwa, wakaingizwa vyumbani kwenda kutosheleza njaa ya kunguni na mbu waliokuwa wakiwasubiri kwa hamu kubwa.
31. Alisema Buheti, sasa furaha yake imezidi, arusi inabisha hodi.
32. Ule ulikuwa usiku wa kiza, kote kweusi totoro, kiza kimejitandaza kwa mapana na marefu mtaani kimya.
33. Wale wafungwa walikuwa wanavishukuru vile vichaka vilivyowafadhili kivuli kizuri kilichowanusuru na jua kali...

34. Alinyanyuka alipachika bunduki yake begani na kuelekea pale kichakani, lakini alipofika alikuta mti mkavu umevaa kofia, hauna wasiwasi umetulia vilevile, Denge ametoweka.

Tamathali ya Semi ya Mubalagha

1. Alivuma nchi nzima kwa ukali wake uliochanganyika na utovu wa huruma.
2. Zahma za mkondo wa Mwana wa Mwana ambazo alidhani akisafiri kwa meli ataweza kuziepuka, zilimvuruga, akalewa bahari akawa hana udole.
3. Mwajuma na Yasmin walikua hawaonani, machozi yanawatiririka, wanakohowa kama wagonjwa wa pumu, pilipili imepata moto.
4. Ukenda huko utamkuta Bashiri katikati ya mlima wa machungwa yamemzunguka huku na huku.
5. Alitishwa akaogopa, hofu ikajaa tele ndani ya moyo wake, ikazagaa chumba kizima akawa ameelemewa na uzito wa mashaka. Alijiona kama aliyetoka kwenye adhabu ya jahanamu.
6. Hapa nilipo akili si yangu, hayo unayonielea yamekivuruga kichwa changu.
7. Mwajuma na Yasmin walikwisha wasili chumbani kwa Denge kama kawaida kilichafuka kama mlikuwamo watu wakipigana ndani. Magazeti yametawanyika chumba kizima...
8. Huna wakati unafanya kazi gani? Hata ungelikuwa na kazi ya kupaka mbingu rangi.
9. Ilikuwepo meza kubwa ya mzunguko wa yai na meza hio imezungukwa na viti vizuri vyenye mto laini ambayo mtu angeliweza kuikalia hata kutwa bila ya kuchoka.

10. Koplo Matata alianza kulia na kumshangaza Yasmin kwani yeye bado kumwona mwanamme, mtu mzima mwenye nguvu zake, kulia kama mtoto mdogo.
11. Ama leo. Tulikuwa hatuna nafasi hata ya kumeza mate. Denge wee, Denge wee,
12. Wakaanza kupakua bidhaa walizoingiza vyumbani, nazo ni sigireti, bidhaa muhimu kuliko dhahabu au fedha kwa wanaoishi gerezani, mwenye nazo ndio tajiri.
13. Hatari! Denge alisema. Sio hatari tu, ni mauti hasa. Alisema yule mfungwa akimaliza kuziweka sawa nywele za Denge.
14. Mambo alikuwa na msururu wa maswali ya kumuuliza Denge kuhusu maisha ya gerezani...
15. Mambo aliuliza, kama mtu aliyestuka, amekodoa macho. Barua zote hizi zilizojaa chumba kizima iwe hana lolote la kusema?
16. Mwajuma akamkumbatia na kumbusu Yasmin kwa furaha utafikiri aliyekwenda ahera akarudi.
17. Karibu. Nani? Yasmin, alijibu Mwajuma. Anajua sauti ya Yasmin hata akiwa ndani ya shimo.
18. Unamwona yule? Akionesha kidole mbele yake, yule aliyevaa kofia nyeusi, yule tunamwita gwiji la gereza; kakulia humu humu, anazeeka humu humu na nafikiri atafia humu humu.
19. Bwan Badi leo umetuletea machungwa? Mambo alimrukia kwa swali. Tena machungwa yenyewe matamu kama asali, alijibu.

20. Nafikiri ingelikuwa kila ninayemnyoa namtoza pesa, basi ningelikuwa milionea sasa.
21. Usicheze na bahati, akajiona kweli ana bahati. Wanauma wanamtetemeka kama Malkia wa Misri
22. Siku hio aliacha yake yote akamkalia dago. Tokea saa sita alikuwa barazani amekaa anamsubiri.
23. Walimkuta nje akicheza na watoto wenzake, amejaa vumbi, shati na suruali aliyoiavaa ni dongo tupu, nguo zote nyekundu kwa udongo wala huwezi kujua zilikuwa na rangi gani hapo mwanzo.

Tamathali ya Semi ya Takriri

1. Darajani ni maarufu kwa misururu ya mafukara wanaoranda sehemu hiyo na makopo yao mikononi wakipita madukani na kuomba, Yalla Masikini, Yalla Masikini.
2. Unan'tazama huku unacheka, unacheka, unacheka nini kinachokuchekesha, mimi nakuuliza wewe unan'tazama halafu unacheka
3. Denge mpenzi wangu, mimi nakupenda, tena nakupenda sana siwezi kwenda kinyume na wewe hata siku moja...
4. Nyumba ya Denge ilizungukwa na askari na Inspekta Wright alikuwa akitoa amri tu. Wewe ... simama hapa wewe hapa, wewe kule! Kijasho kinamtoka.
5. Koplo Matata akaanza kulalamika. Mwanamke wewe! Mwanamke wewe! Sitokusahau maisha yangu! Umenifukuzisha kazi!
6. Yasmin tafadhali niokoe mwenzako, niokoe kutoka katika bahari ya mapenzi niliyozama. Sina zaidi ila nasubiri jibu lako.

7. Na weye nawe na Denge wako, kila uambiwalo, Denge, Denge unafikiri Denge atakupa nini?
8. Maisha yanayoyoma. Yanayoyoma, yanayoyoma na wakati ndio huu. Yasmin akanong'ona peke yake hajui ananong'ona na nani.
9. Ndani ya vyumba vya hoteli hizo alilala, akalala, akalala kwa starehe. Penye joto akahisi baridi na penye baridi akahisi joto.
10. Ama leo. Tulikuwa hatuna nafasi hata ya kumeza mate, Denge weee, Denge weee, haya huyo, leo amekuja.
11. Kazi hiyo unatakiwa uifanye lini? Leo usiku wa leo. Lo! Usiku wa leo? Ndio usiku wa leo. Usiku wa leo utawezaje kuyasambaza makaratasi haya Unguja na Pemba?
12. Walikaa gerezani wote wakiwa na matumaini kwamba labda kesho watatolewa, kesho ikafika ikapita, ikawa huenda ikawa labda keshokutwa, nayo ikafika ikapita, ikawa huenda mtondogoo, nayo ikafika ikapita.
13. Lakini Denge umesikia yaliyowafika na huko Pemba? Walisombwa wakatiwa gerezani kama mbuzi. N'do barabara. N'do barabara! Barabara watu kufungwa.
14. Yasmin alijigaragaza ndani ya mikono ya Denge, akiapa. Sitorudi Abadan, sitorudi Abadan.
15. ..zima moto wakamzuia, hataki kushikwa anapigana nao kama mtu aliyechagawa, anapiga kelele, mke wangu weee! Mke wangu weee! Hapana aliyesalimika katika ajali ile.
16. Yasmin ju ya kitanda, ameshika tama. Akamwambia. Sitorudi Abadan. Sitorudi Abadan. Mimi wako wa daima na milele.

17. Kumbuka jinsi ulivyoshiriki. Kumbuka jinsi ulivyoshiriki katika kumwendesha kapa Koplo Matata. Kumbuka jinsi ulivyotusaidia kuwababaisha polisi kwa yale makaratasi waliyotaka uyatie nyumbani mwetu. Kumbuka hayo yote pamoja na pendo lako kwa ndugu yetu Denge.
18. Na mimi nimefunga safari kutoka Mombasa kuja kukupa pole Yasmin. Pole Yasmin. Pole Yasmin, pole, aliingilia kati Bukheti akasema kwa sauti ya huruma.
19. Yule aliyevaa kofia nyeusi, yule tunamwita gwiji la gereza; kakulia humu humu, anazeeka humu humu na nafikiri atafia humu humu.
20. Mbele ya duka hilo amesimama muuza vibakuli vya bati, akipiga kelele kuvutia wanunuzi. Vyote shilingi vyote! Vyote shilingi vyote! Kimoja naongeza, ameshika vibakuli vinne mkononi.
21. Kazaneni kama wanaume, alipiga kelele, kushoto, kulia, kushoto, kulia, kushoto... aliamrisha kama mwenye kucheza gwaride la wananchi.

Tamathali ya Semi ya Tabaini

1. Mwisho Bwana Raza alimwomba mjomba wa Yasmin aseme na mpwawe, amlani shetani, awaze nyuma na mbele na arudi.
2. Uzuri na ubaya siyo unaoamua kupenda au kupemdwa, pia siyo unaoamua kupendwa au kutopendwa ...
3. Koplo Matata alitoka kwa haraka na kiasi cha kufumba na kufumbua alirudi na jalada mkononi na kumkabidhi Inspekta Wright.
4. Wao wanavutia kule na sisi tunavutia huku na katika mvutano huo, hapana suluhisho linaloweza kupatikana isipokuwa kuwa huru.

5. Mambo alikuwa kijana mwenye kupendeza. Tambo lake lilikuwa la wastani, si mfupi lakini hakuwa mrefu sana. Kadhalika mwili wake haukuwa mnene lakini si mwembamba wa kuwa dhaifu.
6. Furaha iliyoje aliyokuwa nayo Yasmin kwani siku nyingi hakushika pesa nyingi kama zile. Njiani alikuwa akipanga na kupangua...
7. Hii ni kazi ngumu, ina matatizo mengi na inahitaji kujitolea muhanga na mimi ni miongoni mwa hao waliojitolea muhanga kufa, kupona, potelea mbali.
8. Kwa ule wasiwasi wake iliomfanya mara akae, mara asimame, mara aende mara arudi, ile suruali yake ndefu ya kijivujivu haikuweza kutulia vyema kiunoni na mara kwa mara ilimbidi aivutevute kuiweka sawa.
9. Majirani walipokuja kuwaamua kila mmoja alikuwa yu hoi. Wakapeana shuku kwa muda wa siku tatu. Kwa Yasmin zile zikawa siku tatu za shaka na mashaka, anaelea mperampera, hajui atokako, hajui aendako.
10. Humo mlikuwa mmejaa watu, kelele, hakuna anayesikilizana na mwenzake. Wahudumiaji wanakwenda na kurudi sahani wamezibeba mikononi.
11. Denge alikuwa na hisia za kutatanisha baada ya kusoma barua ile. Alihuzunika kwa kumkosa Yasmin na alifurahi kuwa Yasmin amepata mtu wa kumstiri.
12. Denge alimtazama Mambo akatikisa kichwa, akitoa ishara ya kutokubaliana naye. Mwanamke, alisema, mwanamke si kitu cha kunyang'anya au kunyang'anywa. Si kitu cha kunyang'anyiana.
13. Denge alichukua ile sahani akaenda mpaka kiragoni, akakaa, ile sahani ameiweka mbele yake anaitazama. Halua si halua, mseto si mseto, ugali si ugali.

14. Yasmin... Alikuwa hendi harudi, yumo ndani tu kama kizuka, kwa sababu ya wivu aliokuwa nao Shihab.
15. Alihisi kama kwamba mlangoni pale, kwa ghafla, yamechanua maua machangamfu ya yungiyungi yaliyoyapoza na kuyaburudisha macho yake ambayo kwa muda mrefu yalinyimwa mandhari ya mwanamke, si mbaya si nzuri.
16. Yasmin alilalamika. Nakwambia kaniweka ndani kama mwari, hata huyo mwari ana afadhali, sina shoga sina jirani, sina jamaa, mimi na ndani na ndani na mimi, siendi sirudi.
17. Yasmin amejinamia anawaza, peke yake chumbani. Denge hatorudi tena. Kama atarudi basi sio leo wala si kesho, wala si keshokutwa, si mtondogoo, kwani aende huko alikokwenda yeye, aghalabu hukawia kurudi.
18. Yasmin anaelewa vyema kwamba maisha ya kimaskini ni ya bahati nasibu. Mara uko chini umezama mara uko juu unaelea, unasukumwa huku na huku na mawimbi ya maisha.
19. Mara tu baada ya mume wangu kufa. Denge niliyempenda, nikategemea kuishi naye akachukuliwa. Si wangu. Hapa nilipo nipo hohe, hahe sina mbele, sina nyuma, siko kwake siko kwangu. Nadhani nataabishwa na radhi za wazazi wangu.
20. Bukheti anapokutana na Yasmin moyo wake huchanua ukajaa furaha. Mle ndani walimokaa mawazo yao yakigongana. Ya Yasmin yakaenda mbele na kurudi nyuma, ya Bukheti yako mbele, tena mbele sana kwenye ndoa yake na Yasmin.

21. Suruali aliyoivaa ni ya rangi ya kaki, haipo juu wala haipo chini, si refu wala si kaptura, ni msurupwete tu uliyoyapita magoti yake.